

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 17 Juni, 2014

(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa kumi na tano, na leo ni kikao cha thelathini na nne. Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, kama ilivyo ada tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na swali la kwanza asubuhi ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo. Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

Na. 249

Kuhusu Kujenga Viwanda Kwenye Maeneo ya Wananchi Katika Mji wa Himo

MHE. AUGUSTINE L. MREMA aliuliza:-

Katika Mji wa Himo kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makazi ambapo sasa Serikali inataka kutumia maeneo hayo kuweka viwanda.

Je, ni nini athari za viwanda kujengwa kwenye makazi?

Je, Serikali itakuwa tayari kuwafidia wananchi ambao makazi yao yataathirika?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za kujenga viwanda kwenye Makazi ni pamoja ifuatayo:-

Kwanza, taka za viwanda kama vile moshi, vumbi, maji taka, joto na kelele za mashinne zitakazosababisha maeneo ya makazi yasiwe tulivu.

Pili, hatari za kiusalama mfano kuzuka kwa moto viwandani, kuvuja kwa gesi au kulipuka kwa matenki ya kuchemshia vimimika;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tatu, uchafuzi wa vyanzo vya maji kusipokuwa na udhibiti wa uhakika katika mabaki ya kemikali zinazotumika viwandani; na

Nne, mwingiliano wa shughuli za uzalishaji mali na makazi ambao husababisha uchovu kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, B, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imetenga na kupima ardhi katika mji wa Himo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo eneo la makazi. Kiwanja namba 16 Kitalu F ambacho awali kilikuwa kimepimwa kwa ajili ya *Tourist Camping Site*, kilibadilishwa matumizi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kidogo (*light industry*) kinyume na taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi hii inatambua kuwa tarehe 12 Mei, 2014, wakati Waziri wa Nchi, Makamu wa Rais Mazingira alipokuwa anahitimisha hoja ya Bajeti ya ofisi yake kwa mwaka 2014/2015 alilitolea ufafanuzi suala hili kwa kueleza kuwa mmiliki wa kiwanda hakuwa na hati miliki ya kiwanja husika, jambo ambalo lilisababisha baraza la hifadhi na usimamizi wa Mazingira, yaani NEMC kutofanya tathmini ya athari ya mazingira katika eneo hilo.

Kwa kuzingatia hilo, NEMC kupitia barua yake ya kumbukumbu namba NEMC/640/1.Vol1/9 ya tarehe 9 Mei, 2014 imemtaka mmiliki wa kiwanda kusimamisha shughuli zake mpaka atakapokidhi taratibu za kisheria.

Aidha, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia kumbukumbu barua namba CA91/329/01/A/87 ya tarehe 29 Januari mwaka 2013 ilimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuhakikisha ujenzi unaofanywa unaondoshwa kwa sababu haukupata kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kwa mkurugenzi wa mipango miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri tayari imekwisha mwandikia mmiliki wa kiwanda kwa barua ya kumbukumbu ya UTH/2013/13/F ya tarehe 28 Januari, 2014 kumtaka kulipa faini ya asilimia mbili ya Shilingi milioni mia nne na arubaini na tisa laki tisa na kumi na tisa mia tatu na sitini na mbili ambayo ni thamani halisi ya maendeleo yaliyofanyika.

Hi ni kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 34 (1) cha sheria ya mipango miji ya mwaka 2007 na sheria ya ardhi ya mwaka 1999. Kwa hiyo, suala la fidia kwa wananchi itategemea tafiti itakayokuwa imeonesha kama wananchi watakuwa wameathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maelekezo haya ili kuepusha athari za uwekezaji huo kwa wananchi na mazingira kwa ujumla.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Pamoja na hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu yake ya msingi anasema kiwanda Namba 16 kitalu F ambacho awali kilikuwa kimepimwa kwa ajili ya *Tourist Camping site* kilibadilishwa matumizi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kidogo (*light industry*) kinyume na taratibu za kisheria, namwomba Waziri anieleze huyu afisa ardhi aliyehusika na hili jambomo kinyume na taratibu za sheria wamechukuliwa hatua gani; la kwanza.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

La pili anasema, kwa mujibu wa hii barua aliyoitaja hapo, sihitaji kuinukuu, huyo mkurugenzi kuhakikisha ujenzi uliofanywa unaondoshwa, kwa sababu haukupata kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji.

Kwa kuwa jambo hili ni la muda mrefu na kiwanda kinafanya kazi, sasa hivi kinatengeneza pombe, jengo halijaondoshwa, naomba kujua, unipe tarehe na wananchi wa Njia panda wajue kwa sababu malalamiko ni makubwa; kitaondoshwa lini? Nipe tarehe Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninatoka Mkoa wa Kilimanjaro, na eneo hili linalozungumzwa nalifahamu, na Mheshimiwa Mbunge ambaye anafuatilia jambo hili ninajua kwa sababu jambo hili amekuwa analifuatilia kwa muda mrefu. Hapa nime-site, nimeeleza kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais imesema nini kuhusu jambo hili. Nime-site tena, nimeeleza kwamba Waziri wa Ardhi Profesa Anna Tibaijuka amesema nini hapa. Mimi natoka kwenye Serikali hiyo hiyo ya hao hao unaowataja hapa.

Hapa mimi sitengenezi majibu mengine mapya, mimi hapa mkitaka twendeni kwenye hansard mtakuta haya majibu niliyotoa hapa yamo mle ndani, yamewekwa mle ndani. Kwa hiyo, mimi hapa sitengui torati, hapa ninaimarisha torati; hiyo tuelewane kabisa, kwa sababu mimi nitai-contradict Serikali hapa halafu nitaonekana mtu wa ajabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mrema amekuwa anafuatilia jambo hili na ndiyo maana unamsikia anashukuru. (Makofi/Kicheko)

Mimi sikufanya kazi kubwa, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hii, anaitwa Mponji. Mponji wakati anaingia pale Mponji amekuta jengo limeshajengwa pala na kila kitu kimeshamalizi, kazi yote imeisha, yaani jengo, na hivi tunavyozungumza kiwanda kile kinafanya kazi kule.

Ukitaka kuvunja lile jengo sasa issue haiwi hivi kama anavyosema hapa. Cha kwanza, ukitaka kulivunja jengo, ukijenga jengo mahali ambapo hustahili cha kwanza tunaku-save notice, tunakwambia hivi, kalivunje. Anayevunja jengo si Serikali, ni wewe, unaambiwa vunja, unasema mimi sivunji, unaweza ukaenda mahakamani au unaweza ukaamua kwamba unyamaze kimya.

Tunakuambia tuli kwambia tutavunja, sasa tunakupa notice ya pili. Notice ya pili inakuambia nitavunja mimi na nitakupa na cost za kwenda kuvunja lile jengo, ndivyo Sheria inavyosema. Unanyamaza kimya, hukufanya jambo lolote. Mara ya tatu mimi nakuja nalitwanga jengo chini. Nikilitwanga chini nakupa na gharama zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yaliyotolewa hapa yalisema kwamba huyu bwana apelekewe gharama kwa sababu alishapiga katika hatua. Zilipopigwa asilimia mbili zikaja milioni mia nne na arubaini na saba, ndizo hizi zinazozungumzwa hapa.

Sasa kwamba hapa sasa katika hali hii tunayozungumza ya kimgogoro mimi nitasema tarehe hii mnakwenda, watasema huyu Naibu Waziri alikuwa mzima kabisa wakati anajibu swali hili?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tumemwagiza Mkurugenzi Mtendaji, nimezungumza naye asubuhi hii, na Rage alikuwepo na Ngonyani alikuwepo wakati nazungumza naye, tumemwambia ni lazima umpelekee barua, uelekeze haya maelekezo ya Serikali yanayozungumzwa hapa. Wako hapa, ni mashahidi nakupa na mashahidi, kwa sababu watu wengine wanafikiri nimetoa, mtu yeyote akisikia nimesema na Mkurugenzi amuulize kwamba nimemwambia nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tunalichukua kwa uzito mkubwa, hapa kuna *investments*, kuna mambo mengi tunayaangalia hapa, tusije tukafika mahali tukaonekana *tuna-frustrate investments* na vitu vingine.

Lakini ninataka kusema, anayosema Mheshimiwa Dkt. Lyatonga Mrema ni kweli na yamejibiwa na Serikali hapa na sisi tutafuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba jambo hili linakwisha na jambo hili linakwenda kama anavyolisema Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema.

Sasa kuhusu hizi fidia nyingine anazosisema itategemea na NEMC, NEMC hawakwenda pale, NEMC hawakwenda pale Naibu Spika, NEMC hawana taarifa yoyote. NEMC wakienda pale wataangalia hizo athari kama tulivyoeleza hapa, watatuambia, wakituambia sasa tutajua tutafanya nini.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, na swali linalofuata ni la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa Mbunge wa Lupa, kwa niaba yake Mheshimiwa endelea, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. (*Makofi*)

Na. 250

Kuhusu Matokeo ya Uchunguzi wa Ubadhilifu Katika Uendeshaji wa Ushirika Wilayani

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MHE VICTOR K. MWAMBALASWA) aliuliza:-

Mkuu wa Wilaya ya Chunya aliunda Tume kuchunguza ubadhilifu katika uendeshaji wa Ushirika wa Tumbaku Wilayani na Matokeo ya uchunguzi huo yamewasilishwa kwa mkuu wa Wilaya.

Je, ni nini matokeo ya uchunguzi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Wilaya ya Chunya aliunda Tume mbili, tarehe 18 Novemba, 2010 aliunda Tume ya kuchunguza malalamiko ya wakulima wa zao la Tumbaku kukatwa fedha zao kimakosa kiasi cha Dola za Marekani milioni mia tatu na themanini na tatu laki nne na kumi na nane na senti themanini na tatu kutoka kwa akaunti ya vyama vya msingi vya mazao, yaani AMCOS, kutokana na mikopo ya pembejeo waliyokopa katika benki ya CRDB. Tume ilibaini kwamba makato hayo yalifanyika kimakosa.

Makato halisi yaliyokatwa kimakosa yalikuwa ni Dola za Kimarekani 298,300.00 na si Dola za Marekani mia tatu na themanini na tatu milioni mia nne na kumi na nane na point themanini na tatu. Serikali iliagiza fedha hizo zilipwe kwa wakulima na zimekwisha kulipwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Oktoba, 2012 iliundwa Tume na kuchunguza na kutathmini mwenendo wa biashara ya tumbaku Wilayani Chunya, matokeo ya uchunguzi yalisomwa mbele ya Baraza la Madiwani tarehe 12 Desemba, 2012 na matokeo yalionesha mambo yafuatayo. Kwanza, wajumbe wa Bodi na watendaji wake hawana taaluma ya kuendesha majukumu yao.

pili, baadhi ya wasafirishaji wakishirikiana na wafanyabiashara walionekana kutokuwa waaminifu, wakibadilisha tumbaku safi wakati ikisafishwa, kwa lengo la kudanganya kuwa wakulima ndio wanaofanya hivyo ili baadaye wakulima wakatwe malipo yao. Tatu, kutokuwepo kwa ukaguzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia matokeo haya ya uchunguzi Serikali Wilayani Chunya imeagiza mambo yafuatayo:-

Kwanza, COASCO ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwenye AMCOS ili kukabiliana na ubadhilifu unaofanyika kwenye vyama vya Ushirika;

Pili, hatua zichukuliwe kuwapeleka watendaji katika Chuo cha Ushirika cha Moshi;

Tatu, elimu itolewe kwa wakulima ili kuimarisha ubora wa zao la tumbaku;

Nne, Chama Kikuu cha Ushirika yaani CHUTCU kuwa makini katika ugawaji wa pembejeo kwa kuzingatia takwimu za mgao wa pembejeo kwa kila chama kwa msingi wa kuondoa migogoro katika vyama hivi; na

Tano, Serikali kuendelea kudhibiti utoroshaji wa tumbaku kwenda nchi za jirani kwa kuweka vizuizi kwenye barabara kuu; na

Mwisho, Halmashauri ya Chunya kuwapatia usafiri maafisa wa Idara ya Ushirika ili waweze kumudu shughuli zao za kila siku.

MHE.DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa kiasi hiki cha Dola za Marekani ni zaidi ya Dola mia mbili tisini na nane (Dola 298) zinazotokana na AMCOS kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu. Lakini tatizo hili limeanza tangu Novemba 2010, na hii Tume iliundwa mwaka 2012 Novemba. Sasa leo hii Mheshimiwa Naibu Spika ni mwisho wa Juni, 2014, ni muda mrefu sana, nilikuwa nahitaji Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze hapa kuliko kutupa haya majibu tu ya kisiasia.

Jambo gani la msingi ambalo hatua ya uhakika imechukuliwa kwa ajili ya kuwapa adhabu wote waliosababisha jambo hili?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa huku ndani hapa kwenye hili Bunge tunakuja kufanya siasa hapa, yaani mtu ambaye hafanyi siasa hapa *then* hajui kwamba amefuata nini humu ndani. Hapa ndipo kwenye mtambo wa siasa, hapa, hapa ndipo penyewe, siasa hapa ndipo mahali pake hapa; na *politics* ni *reflection* ya *economics* na *economics* ina *reflection* na *politics*.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Uliza Marekani uliza mahali popote, mimi huwa nasikia watu wanasema unaleta mambo ya siasa hapa, tungeleta nini hapa, hapa tumekuja kuleta siasa hapa. Hapa katika *developing countries* unazungumza *is all about allocation of resources*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nijibu hapa, najibu swali hili, tena najibu swali hili wala sijibu kisiasa wala sijibu kiuchumi, nataka nijibu swali hili.

Mheshimiwa Rais alikwenda pale Tabora akakuta matatizo kama haya. Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akamwagiza IGP aende pale, na awachukulie hatua watu wote ambao walihusika na hii choko choko ya tumbaku pale Sikonge kwa akina Mheshimiwa Said Nkumba. Haya majibu yalikuwa ni ya kisiasa hayo?

Anapoelekeza waende pale. Mimi nimezungumza na Mkuu wa Wilaya, tena tumshukuru Mkuu huyu wa Wilaya, Mkuu huyu wa Wilaya akagundua kwamba hela hizi Dola 283 zimepotea. Amehakikisha zimepatikana na amehakikisha kwamba wakulima wamelipwa hizo hela zao. Hayo ni majibu ya kisiasa hayo? Wamelipwa hela zao pale, walikuwa wanadai milioni mia tatu na themanini na tatu, Dola hizo, wamelipwa hapa laki tatu na themanini na tatu.

Mimi nataka niseme hivi, tunampongeza Mkuu wa Wilaya ya Chunya kwa kazi nzuri aliyoifanya pale. Sasa hivi ameamua kwamba anaweka mageti, ata-check tumbaku yote inayopita kwenda nchi za jirani, na yeyote tutakayemkamata hapa, nataka nikuambieni, lazima tutamfikisha katika vyombo vya Sheria. Hao wote waliohusika hapa, ninayo mimi ile ripoti yote, ninayo kubwa hivi.

Tutaifanyia kazi na tutahakikisha kwamba hawa jamaa wote wambao walihusika na mpango huo wote tutawachukulia hatua. Majibu haya si majibu ya kisiasa, majibu haya ni majibu ambayo yanajielekeza kwenye matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanri. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwanri si tu kwamba ametoa jibu bali ametoa jawabu. Tunaendelea na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka. Mheshimiwa Clara. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 251

Kuhusu Ulipaji Malimbikizo ya Mishahara

MHE. CLARA D. MWATUKA aliuliza:-

Sharti mojawapo katika kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishini pamoja na kukubali cheo au daraja.

Je, imewahi kutokea kwa mtumishi yeyote kukataa cheo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kulazimisha kukubali cheo au daraja kabla ya kurekebisha mishahara wa mtumishi ulifutwa kwa waraka wa Katibu Mkuu Kiongozi namba moja wa mwaka 2010 unaohusu uwajibikaji katika kusimamia rasilimali watu, unaoelekeza kufanya marekebisha ya mishahara mara tu baada ya mtumishi kupandishwa cheo. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waraka huu ulifafanua zaidi waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma namba moja wa mwaka 2009, kuhusu udhibiti ongezeko la madeni ya Serikali kwa watumishi wa Umma, unaowaagiza waajiri kuacha mara moja utaratibu utaratibu wa kuwapandisha vyeo watumishi bila kuwepo kwa ikama na Bajeti ya Mshahara, au kurudisha nyuma tarehe za waliopandishwa vyeo.

Watumishi wanaopandishwa vyeo wajaze nafasi zenye fedha na cheo walichopandishwa kianze mwezi ambao uamuzi wa kupandishwa cheo hicho ulifanyika.

Aidha, mtumishi apewe barua yake mara tu anapopandishwa cheo. Barua isingoje mpaka mwisho wa mwezi uishe na kulazimika kuwa na malimbikizo yatokanayo na mshahara wa cheo kipyaa. Kupandisha watumishi vyeo bila kuwarekebisha mishahara yao kwa wakati ni upungufu wa kiutendaji ambao ni lazima ukomeshwe mara moja. Kwa hiyo, sharti la kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi bila kukubali cheo lilifutwakwa waraka nilioutaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa katika kumbukumbu zetu hakuna mahali kulipooneshwa kwamba kuna mtumishi aliyewahi kukataa cheo. *(Makofi)*

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Waziri. Kweli nimeridhika na majibu yake, na kwamba ninashukuru kwa hao waliobakia. Maana mimikwa kweli niliumia. Niliuliza swali hili kwa sababu niliambiwa wakati Binti yangu alifariki wakati alishaomba, alikuwa amedai na kuwekwa kwenye *list* ya kupandishwa cheo, na daraja pia. Sasa baada ya kufa mwenyewe, mimi ndiye nilikuwa mrithi na ndiye niliyekuwa ninafuatilia masuala ya mirathi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipofuatilia ofisini kwake mmoja wapo wa wafanyakazi wenzie, aliniambia, ni kweli akuwa miongoni mwa waliostahili kupandishwa daraja na cheo.

Lakini sasa hatuwezi kufanya lolote kwa sababu ni nani atakayekubali cheo hicho. Akiandikiwa barua, ninani atakayethibitisha au kukikubali cheo hicho? Kwa kweli niliumia. Maana hasa ilipelekea ya kwamba mafao yake sasa walitoa katika kufuatia ngazi ile ya mshahara iliyokuwa ya nyuma bila kuangalia kwamba hivi sasa huyu alistahili apandishwe cheo kingine.

Je, hivi sasa hao watakaofuata au yeye sasa siilikuwa ameishaonewa kwamba hakupata ile haki aliyostahili. Sasa ikiwezekana apewe? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimemwelewa Mheshimiwa Clara Mwatuka. Ni kweli hapo zamani, ilikuwa lazima mtumishi kama umepandishwa cheo, lazima uandike barua ya kukubali cheo ndipo urekebishiwe mshahara. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Lakini kwa sasa hivi, kwa mfumo wa taarifa za Watumishi na mishahara ambao tumeufunga sasa hivi, ni kwamba Mfanyakazi anapopandishwa cheo tu mara moja anaingizwa kwenye mfumo mwezi huo huo na anapata malimbikizo yake.

Sasa kwa *issue* ya yeye. Inachotakiwa Mkuu wa Utumishi katika nchi hii ni Mheshimiwa Rais, kwa hiyo unaleta ili atoe kibali. Sisi tunapitisha atoe kibali maalum kwa marehemu kulipwa *arrears* zake au hayo mafao yake kulingana na cheo ambacho alitakiwa apate kwa wakati huo. Kwa hiyo, yalete kwangu hayo malalamiko. Mimi nitayafanyia kazi. Nitayapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ambaye anayo hiyo *exemption* ya kutoa kwa watumishi kama hao. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, wapo walimu ambao wamepandishwa Madaraja na Wamepandishwa vyeo lakini hawajarekebishiwa mshahara. Sijui anawaambia nini Walimu hawa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI: Mheshimwia Naibu Spika, mimi niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge, kwamba tangu tuanze kufunga huo mfumo uliopo sasa hivi, wa taarifa za Watumishi, pamoja na mishahara pale Utumishi, kuanzia mwaka 2012, tatizo hili halipo. Kama lipo litakuwa ni uzembe wa Watendaji katika Halmashauri husika au katika taasisi husika.

Kinachotakiwa akipata barua mwezi huo huo. Kama ni kabla ya tarehe 9 ambapo *Pay Roll* imefungwa. Barua yake wana i-scan waniingiza kwenye mfumo *Automatic* Mshahara wake unabadilika. Sasa hilo ndilo linalotakiwa kufanywa na waajiri. Sasa kama kuna uzembe ambao umefanywa na watendaji.

Lakini kwa kweli *System* yetu kwa sasa hivi imefanya vizuri sana, niwahakikishe Waheshimiwa Wabugne kwamba hata suala la mishahara sasa hivi angalao limepungua kwa kiasi kikubwa, na malimbikizo sasa hivi niliyo nayo. Malimbikizo ambayoyanatakiwa kulipwa ni kama shilingi bilioni 5 tu. Kwa mwaka mzima tumelipa shilingi bilioni 45 ambazo ziko kwenye *foleni* ni bilioni 5 tu ambazo tutalizipa hivi karibu. Kwa hiyo tatizo limepungua kwa kiasi kikubwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Diana M. Chilolo, nilikuona swali la mwisho kwenye eneo hili.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa Watumishi hupandishwa vyeo kwa kufuata vigezo mbali mbali, ikiwemo umri kazini, uadilifu na mengine. Na kwa kuwa wako Walimu ambao wamepita umri wa kupandishwa vyeo, kama ilivyoelekezwa kwenye ajira yao.

Je, Mheshimiwa Waziri atasema nini ili Walimu hao huko waliko wasikie, waweze kujua jambo la kufanya ili wawezekupandishwa vyeo vyao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, natumaini umempata Mheshimiwa Diana M. Chilolo. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais Mejimenti ya Utumishi wa Umma, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RASIS, UTUMISHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mwalimu Diana Chilolo, ambaye ninampongeza sana katika kutetea haki za Walimu yuko mstari wa mbele. Ni kweli lipo tatizo kidogo la Walimu ambao wamepitiliza muda wao wa kupandishwa cheo kulingana na ikama ambayo tumeiweka.

Tatizo lilopo ni kwamba sasa hivi kwa mfumo tulioufunga, lazima mwajiri ahakikishe ya kwamba wakati wa Bajeti, anaiangiza Watumishi wote ambao wanatakiwa kupandishwa vyeo kwa mwaka husika. Asipoingiza kwenye mfumo ina maana kwamba akiingiza katika ya mwaka mfumo wetu unakataa, una-*reject*.

Kwa hiyo mimi nitoe wito kwa waajiri wote kuhakikisha kwamba wanaingiza wakati wa Bajeti, majina ya watumishi wote au idadi ya Watumishi wote ambao watapandishwa cheo ili wapate *approval* kabla ya Bajeti kuingizwa humu Bungeni.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Uchukuzi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Elizabeth Machangu.

Na. 252

Utaratibu wa Mabasi ya Masafa Kuingia Katika Vituo vya Mabasi ya Halmashauri za Wilaya Nchini

MHE. BETTY E. MACHANGU aliuliza:-

Hivi karibuni *SUMATRA* ilipeleka Waraka Kumb. Na. CD 226/267/01 wa tarehe 27 Februari, 2012 kwamba hakuna haja ya mabasi yanaokwenda masafa marefu tokea mikoani kwenda Dar es Salaam kuingia kwenye vituo vidogo vya mabasi kwenye Halmashauri za Wilaya, wakati vituo hivyo vilijengwa kwa gharama.

Pia ni vyanzo vya mapato kwa Halmashauri hizo. Mfano mzuri wa kituo kilichoathrika sana na uaratibu huo ni kile cha Njiapanda kwenye barabara ya Dar es Saalam – Moshi – Holili – Moshi ambapo Waraka huo wa *SUMATRA* una pingana na sheria ndogo za Halmahauri.

(a) Je, Serikali haioni kuwa Waraka wa *SUMATRA* unarudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa kuikosesha chanzo cha mapato, lakini pia kuleta usumbufu kwa abiria kuvizia mabasi barabarani?

(b) Chanzo cha Mapato kwa kituo cha Njiapanda – Moshi – Himo – Holili yalikuwisha ainishwa kwenye Bajeti ya 2014/2015. Je, Serikali itakuwa tayari kuilipa Halmashauri ya Moshi kiasi hicho kitakachokosekana kama fidia kwa mwaka 2013/2015?

(c) Kwa agizo la *SUMATRA*, ni wazi kuwa vituo hivyo vidogo havitatumika tena. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa fungu la fedha kwa ajili ya ulinzi wa vituo hivyo ili kuzuia wizi unaoweza kujitokeza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, samahani kwa kutamka jina lako visivyo. Hivyo ndivyowalivyoniandikia hapa, walidhani Betty ni Elizabeth. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Machangu, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama hivi ifuatavyo:-

(a) Waraka wa *SUMATRA*, haulengi kurudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya yote yote ile nchini, ikiwemo ya Moshi, kwa kuwa mabasi yatoayo huduma ndani ya mikoa, bado yanalazimika kutumia vitu vyote vya Wilaya na miji hivyo kuondoa haja ya abiria kuvizia mabasi barabarani. Waraka huo unayahusu mabasi ya masafa marefu ambayo yameelekezwa kutumia viuto hivyo pale panapokuwa na abiria wa kushuka au nafasi ya kuongeza abiria kwenye basi hilo.

(b) Waraka wa *SUMATRA*, ulizingatia kuwa Halmashauri zitaendelea kukusanya mapato yatoakanayo na tozo za matumizi ya vituo katoka katika mabasi yatoayo huduma ndani ya mikoa, na pia Mabasi ya masafa marefu yanayoingia katika vituo hivyo, kwa lengo la kushusha au kupakia abiria. Kwa kufanya hivyo Halmashauri zitaendelea kukusanya mapato kutoka katika vituo hivyo.

(c) Vituo vidogo vilivyopo katika Halmashauri mbalimbali nchini, vitaendelea kutumiwa na mabasi yenye leseni za kutoa huduma za usafiri ndani ya mikoa kwa kuwa bado yanalazimika kusimama katika vituo vyote vya wilaya na miji, na mabasi ya masafa marefu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yanalazimika kusimama katika vituo hivyo, ikiwa abiria aliye ndani ya basi atahaji kushuka au basi likiwa na nafasi ya kuchukua abiria zaidi.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo huu unaruhusu basi kulipa ushuru kwenye kituo cha kwanza au cha pili, au kama basi linashusha au kupakia abiria.

Je, Serikali haioni kwamba mfumo huu unatoa mwanja wa mabasi haya kukwepa ushuru?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Idara za Serikali zimekuwa zina migongano wakati mwingine. Kwa sababu wakara huu ulienda kwenye Halmashauri za Wilaya bila kushirikisha Wakurugenzi, na ndio maana kukatokea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuiuliza Serikali, ni lini wataweka mkakati wa ku-reconcile hizo, yaani kuondoa migongano kati ya Idara na Idara kwa ajili ya utekelezaji mzuri zaidi? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo ukizingatia kwamba Waraka huu kwa kweli, umeathiri Halmashauri hata pale Kibaigwa tumejenga *Stand*, mabasi hayapiti katika *stand* hiyo kwa sababu waraka.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Betty Machangu, na nyongeza yako, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, mabasi haya ya masafa marefu, yaani yanayosafiri kutoka mkoa mmoja na kwenda mkoa mwingine, endapo halitakuwa na abiria anayeshuka katika kituo cha wilaya fulani, na hawana nafasi ya kuingeza abiria kwenye basi hilo. Hawalazimiki kusimama kwenye kituo hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilitokana na ukweli kwamba, safari hizi zilikuwa na utitiri wa vituo ambavyo havihitajika kwa mabasi husika. Matokeo yakwenye Mabasi walianza kudai kupandisha nauli ilikufidia hizi tozo wanazoenda wakitoa kila kituo wanacholazimika kusimama njiani. Ndiyo maana Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa Nchi Kavu na Majini, wakaka na huu waraka kuondoa tozo ambazo siyo za lazima kwa mwenye basi.

Kwa hivyo habari ya mabasi kukwepa kulipa ushuru, hili ni suala la usimamizi tu. Vyombo vyetu vya kusimamia usafiri wa barabarani, kwa maana ya Polisi na *SUMATRA*, wanaelekezwa tu kuendelea kuhakikisha ya kwamba basi kama litataka kupandisha abiria lifanye hivo kwenye kituo cha mabasi.

Basi likitaka kushusha abiria lifanye hivyo kwenye kituo cha mabasi na katika kufanya hivyo watalazimaika kuingia mahali ambapo ushuru wa Halmashauri au Mamlaka yote utakuwa unatozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu kushirikisha Wakurugenzi wa Halmashauri, kabla ya Waraka wowote kutolewa Wadau hushirikishwa katika majadiliano ili kufikia uamuzi juu ya Waraka unaotarajiwa kutolewa.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed, swali la nyogezwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kusema kweli mimi ninaunga mkono majibu ya Naibu Waziri mia kwa mia. Mimi ni mmoja wapo ninayedhurika sana, kama ninatoka Mbeya kwenda Dar es Salaam. Tunaingia kila Kituo, tunapoteza muda, na kama ni unyonyaji kwenye mabasi, Mheshimiwa ninaunga mkono majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri mia kwa mia. Hakuna swali ninalouliza. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Kwa vile hakuna swali. Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Henry D. Shekifu.

MHE. HAROUB M SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haroub kuhusu utaratibu.

MHE. HAROUB M. SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba utaratibu wa kiti chako kama Wabunge wanaruhusiwa kuunga mkono kauli za Serikali badala ya kuuliza maswali katika kipindi hiki.

NAIBU SPIKA: Wabunge wanaruhusiwa kama wana majibu, kukazia majibu katika maeneo wanayo yafahamu. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nikubali kwamba majibu ya Naibu Waziri ni mazuri sana. Lakini katika suala hili la kodi na utaratibu wa uwiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika kushika kodi, liko tatizo baada ya kuondoa zile kodi, zenye matatizo au zenye kero kwa wananchi kunako mwaka wa 2004 zilipoondolewa na Serikali ikakubali kufidia, mpaka hivi ninavyozungumza sasa kodi hizi hazifidiwi.

Moja ni kutokana na mwingiliano kati ya maamuzi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Serikali inatamka nini katika kurejesha hela ambazowalikubali kuwafidia Halmashauri ili Halmashauri zipate mapato? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Henry Shekifu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalipa fidia kwa Halmashauri zote nchi kutokana na kodi zenye kero zilizoondolewa mwaka huo 2004, kupitia *un conditional grant* inayotolewa kwa Halmashauri zote. *(Makofi)*

Na. 253

Malipo ya Bima kwa Ndege iliyopata Ajali

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. RACHEL R. MASHISHANGA) aliuliza:-

Mwaka 2012/2013 Serikali ililipwa Bima ya Ajali ya Ndege aina ya *Dash 8-Q 300*, Shilingi 12.2 Bilioni baada ya kupata ajali mwezi Aprili 2012 na kati ya fedha hizo, shilingi 10.6 Bilioni ilisema kuwa ingelipa malipo ya awali kwa ndege mbili:-

(a) Je, ni ndege za aina gani zimelipiwa malipo hayo ya awali?

(b) Je, ni lini ndege hizo zitawasili nchini ili zianze kazi kupunguza adha za usafiri wa anga hasa kwa Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Kigoma?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Mpaka kukamilika kwa malipo hayo, Serikali itakuwa imetumia fedha kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Robert Mashishanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama na hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwelikatika Bunge la Bajeti, mwaka 2012/2013, Serikali iliahidi kuwa itaendelea kutekeleza mkakati wake wa kuimarisha ATCL, kwa kununu ndege mbili kwa kutumia fedha ambazo ATCL ililipwa Bima kutokana na ndege yake aina ya Dash 8-Q 300 kupata ajali mwezi Aprili, 2012. Kulipa malipo ya awali kwa ndege mbili, aina ya Dash 8-Q 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Bima kutokana na ajali hiyo, zilizolipwa ni kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.1. Kiasi cha fedha hizo zilitumika kulipa deni la Bima ya Ndege. Kununua vipuri, kulipia Injini ya Dash 8-Q 300 iliyokuwa kwenye matengenezo Italia.

Kukodi ndege ya aina ya CRJ 200, na sehemu ya fedha hizo zilikamatwa na wadai wa ATCL, hivyo ATCL, imebaki na kiasi cha Dola Milioni 3.4, ambazo zitatumika kufanya malipo ya awali ya ndege mbili aina ya Dash 8 Q-400 zenye uwezo wa kubeba abiria 78 kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa ahadi hiyo mwezi Machi, 2014 Serikali imeanza mchakato wa kununua Ndege mbili aina ya Dash 8 Q-400 kwa utaratibu wa kununua kwa kukodi yaani (*Lease Purchase Basis*).

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya ndege hizi ni Dola za Kimarekani milioni 35 kwa bei ya soko. Fedha za kumaliza malipo yaliyobaki zitataka kwenye uendeshaji wa ndege hizi na mkopo wake utalipwa kwa kipindi cha miaka kumi (10).

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuahuru, ninaomba sasa niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Naibu Waziri anakiri kwamba katika Bunge la Bajeti, 2012/2013, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, alilitaarifu Bunge hili na aliahidi kwamba zile pesa ambazo zingelilipwa na Bima zingelinunua ndege na hivyo tukawa tuna subiri kwa hamu sana kupata ndege hizo. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia kwamba Mheshimiwa Waziri au Wizara yake walilidanganya Bunge kwa sababu waliahidi kwamba zile fedha za bima zingelinunulia ndege, na ndege hiyo mpaka leo hii hazijanunuliwa na sasa hivi wamebadilisha matumizi.

Swali la pili, kwa kuwa ndege hiyo iliyoanguka pale Mwanza, mpaka leo hii iko pale uwanjani na hivyo, inaonyesha madhari yetu inakuwa mbaya, na Mheshimiwa Naibu Waziri, juzi akijibu swali hili alisema Seikali, wenye jukumu la ile ndege ni watu wa Bima.

Je, Serikali sasa inawambai nini hawa watu wa Bima ili waweze kuondoa ndege ile pale kwenye uwanja wa Mwanza? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Waziri anayekuja hapa mbele kwa makusudi kudanganya Bunge. Haina manufaa yeyote kwa Waziri kusimama hapa na kusema habari ya uongo. Isipokuwa kilichotokea ni kwamba, ni kweli matumaini yetuyalikuwa fedha zile zikilipwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zitatumika kulipa hiyo *instalement* ya kwanza kama tulivyokuwa tume *plan* na kuzungumza na wale watu wa *Bombadier*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea, baada ya fedha hizo kuingizwa kwenye *account* za ATCL, kwanza zikakutana na amri ya Mahakama zikachukuliwa sehemu kubwa ya hiyo pesa.

Kwa hivyo mazunguzoya kulipa ule mkupuo wa kwanza kama yalivyokuwa yametarajiwa yakashindikana. Yakaingia mambo mengine matumizi ambayo Mheshimiwa akipenda tutamwonyesha mengi yalivyokuwa yanadaiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema ili uwekezaji mzuri katika ATCL *ufanyike*, ni lazima kwanza tuondokane na madeni ya ATCL, vinginevyo tunakuwa katika mashaka ya namna hiyo *every other time* tunapojaribu kufanya uwekezaji ndani ya ATCL. Kwa hiyo Serikali hatukulidanganya Bunge.

Fedha za ATCL zilizobaki tume *renegotiate* sasa hii milioni 3,500,000 wenzetu wametukubaliana tukikamilisha vipengele vichache vilivyobaki tunaweza kuanza kununua ndege hizo kwa mtindo wa kukodi kwa kulipa, ndiyo maana utaratibu sasa umebadilika inabidi tukodi tuendeleo kulipa huku tunatumia ndege mpaka itakapokamilika malipo yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mandhari ya viwanja vyetu kutokana na ndege zilizoharibika pale. Nilikwishasema, dhamana hii inakuwa kwa wenye ndege hiyo ambayo ni Makampuni ya Bima yalivyokuwa yamekweka Bima kwa ajali za ndege hizo.

Sasa hivi hilo ni jambo la majadiliano kati yao na mamlaka ya viwanja vya ndege kwa sababu ndege hizo zinavyoendelea kubaki pale mamlaka za viwanja vya ndege inawatoza kwa hiyo itakapofikia kwamba fedha zinakuwa nyingi basi TAA watajua la kufanya na hizo ndege.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Sanya, swali la mwisho la nyongeza!

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, zipo ndege binafsi zinazo *operate* baina ya Dar es Salaam na Dodoma kwa gharama kubwa mno kiasi ambacho gharama hizo ni sawa na kuondoka na Rwanda Air kutoka Dar es Salaam kwenda Kigali na kurudi Dar es Salaam.

Na kwa kuwa, katika swali la msingi Mheshimiwa aliyeyuliza swali ameuliza namna gani shirika hili litasaidia kuweka safari za mikoa na mikoa nchini Tanzania.

Je, shirika hili lina mpango gani sasa hivi wa alau kupunguza gharama za ndege kwa ku-*operate* ndani ya nchi kutoka Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Kigoma na kurejea *rout* hiyo ili raia wafanyabiashara na watu mbalimbali waweze kusafiri kwa urahisi badala ya kutozwa gharama kubwa sana ambazo zimepita kiasi?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ni kweli kwa sasa gharama za kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa ndege ni kubwa kwa kulinganisha. Lakini nitumie nafasi hii kusema kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana kuwashawishi wafanyabiashara wenye kufanya biashara ya usafiri wa anga kuanza kuleta ndege zao Dodoma na maeneo mengine ya mikoani. Niseme tu kwamba kwa sasa kampuni moja ya *flight link* iko katika hatua za mwisho mwisho kabisa za maandalizi ili kuanzisha safari ya ndege kubwa yenye kuweza kubeba abiria 30 kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwenda Arusha kurudi Dodoma na baadaye Dar es Salaam.

Ni kwa matarajio hayo kwamba gharama za usafiri kwa Dar es Salaam Dodoma zitapungua hata kufikia 50% ndege hii aina ya *Embrae 190* itakapoanza kufanya kazi katika rout hiyo niliyoitaja.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Anne K. Malecela kwa swali la mwisho la nyongeza kwa asubuhi hii!

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, mataifa yote yanatumia ndege zao kutangaza vivutio vya utalii kama vile ambavyo Air Tanzania wanatangaza Twiga na kadhalika.

Sasa naomba kuuliza kwamba kuna ndege ya *Kenya Airways* ambayo inaruka na inatangaza Mlima Kilimanjaro. Kwa kuwa, Mlima Kilimanjaro ni Mlima wa Tanzania na sasa ndege ya *Kenya Airways* ndiyo inayotangaza Mlima Kilimanjaro kama vile ni mlima wao.

Je, Serikali inasema nini katika suala hili ambalo siyo sahihi kabisa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, majibu! Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa majibu kwa Mheshimiwa Mama Kilango, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kumeonekana ndege ya Jamhuri ya Kenya yaani *Kenya Airways* ina alama ya Mlima Kilimanjaro, lakini si kosa. Si kosa kwa sababu hakuna mtu aliye *patent* matumizi ya Mlima huo katika Ndege, kama sisi tungekuwa tumefanya hivyo kabla yao ingekuwa ni sawa sawa.

Lakini pia, ili ufanye hivyo ni lazima utumie ujuzi wa *intellectual property* na zipo aina kama tano hivi za hayo. Moja ambayo haihusiki *nicopy right* ambayo inatumika kwenye vitabu na kwenye mambo ya muziki au mambo ya sanaa kwa ujumla wake. Lakini ya pili ni *patent*, sasa ukifanya *patent* ni lazima uwe umegundua wewe na una *information* ya *formation* ya Mlima Kilimanjaro, hiyo nayo huwezi kufanikiwa.

Ya tatu ni *trade mark*, kwamba unatumia Mlima Kilimanjaro ya sura ya Mlima Kilimanjaro kutenganisha vifaa na bidhaa ambazo zinafanana kwamba hizi zinatoka Tanzania na kwa hiyo zinatumia Mlima Kilimanjaro. Lakini vifaa hivyo kwa mfano huo sasa ziwe ni ndege, hatujawahi kufanya hivyo.

Nyingine ni *industrial* ambayo pia haihusiki hapa. Lakini ya mwisho ni geographical, kwamba bidhaa hizi ambazo zina nembo hii zinatoka mahali fulani kwa mfano *Champaign*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tanzania uandike Campaign haitakuwa Campaign kwa sababu Campaign inatoka Ufaransa. Samahani kwa kutumia mfano huo wa ulevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, matumizi ya alama hiyo kwenye ndege ya Kenya hayana madhara kwa Tanzania ni kama vile unavyosema njoo Kenya uone Mlima Kilimanjaro, na pia hiyo haina madhara kwa sababu ni kweli kwamba ukienda Kenya unaweza kuuona Mlima Kilimanjaro.

Lakini kubwa sasa ni kwamba sisi wenyewe tusingojee mpaka watu wengine waanze kwani na sisi tunatakiwa kutumia huo mlima kama tunaona kwamba utatufaa katika matumizi ya biashara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo majibu yangu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anachotuambia ni kwamba tuache kulalamika.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Malolle, Mbunge wa Dodoma Mjini!

Na. 254

Ujenzi wa Kiwanda cha Ndege cha Msalato

MHE. DKT. DAVID MCIWA MALLOLE aliuliza:-

Serikali ilipokuja na mpango wa ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Kimataifa ililazimika kuwahamisha wakazi wa eneo hilo ili kiwanja kijengwe hapo na kuwalipa fidia lakini wako baadhi ya watu ambao hawajalipwa fidia yao hadi sasa.

(a) Je, ni lini wananchi wa vijiji vya Nzuguni, Mpamaa na Msalato watapewa fidia yao?

(b) Je, Serikali inatambua idadi kamili ya wananchi wanaodai fidia hiyo na kiasi cha fedha kinachodaiwa?

(c) Je, ni lini ujenzi huo utanza?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Malolle, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Wananchi wa Vijiji vya Nzuguni, Mpamaa na Msalato walishalipwa fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa kupisha mradi wa kiwanja cha ndege cha Msalato mwaka 2008 na tayari wameshahama. Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.0 ili kulipa fidia kwa mashamba 980, yaliyochukuliwa baada ya malipo ya fidia ya kwanza.

(b) Serikali inatambua idadi kamili ya wananchi wanaodai fidia ya mashamba katika eneo la Nzughuni ambayo ni 980 na kiasi cha fedha kinachodaiwa na wananchi hao kinafikia shilingi bilioni 3.0.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Serikali inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mikopo ya riba nafuu kutoka Taasisi mbalimbali za fedha pamoja na sekta binafsi ili kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. David Mallole, swali la nyongeza.

MHE. DKT. DAVID MCIWA MALLOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri hasa yale ya kukubali kwamba wapo wananchi 980 ambao fidia zao za mashamba bado hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile sasa ni miaka saba tangu wananchi hao wa vijiji vya Nzuguni, Mpamaa na Msalato wakiendelea kudai fidia za mashamba yao na sasa hivi ni watu wengi kwa sababu kama wapo watu 980 ukisema tu kwamba kila mmoja ana familia ya watu 3 au 4 si chini ya wananchi 3000 ambao wameathirika sana kutokana na mashamba hayo kutokulipwa fidia.

Na kwa kuwa, Serikali mpaka dakika hii katika majibu haya haijaonyesha wazi kwamba wana mikakati gani inayoonyesha kwamba wanatafuta fidia hii ya bilioni 3 ili kuweza kuwalipa wananchi hao.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kusimama sasa kuweza kuwasaidia wananchi wa vijiji hivyo kuelewa kwamba fidia hiyo ya bilioni 3 itakuwa imeshatafutwa na kulipwa kwao hadi lini?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa David mallole Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimesema wananchi waliokuwa kwenye maeneo yale matatatu niliyoyataja walikwishalipwa fidia ya makazi yao na baadaye ikaonekana kwamba eneo la uwanja wa ndege linahusisha na mashamba 980, mashamba 980 na ndiyo hayo Serikali inatafuta fedha ya kuwalipa fidia wananchi hao.

Kwa sasa wananchi hawa wanaendelea kutumia hayo mashamba na ndilo jambo walilokuwa wakifanya kwenye maeneo hayo.

Kwa hiyo, madhara ya kutotumika mashamba kimsingi hayapo, tunafahamu kwamba kuchelewa kulipa fidia kunaongeza riba katika fidia hiyo na jambo hilo tutalifanya mara fedha itakapopatikana kwamba wananchi watalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo na Wizara ya Fedha Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, kwa niaba yake Mheshimiwa Magolyo Maige.

Na. 255

Makampuni Makubwa Kutojiunga na Soko la Hisa Tanzania

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (K.n.y. MHE. RICHARD MGANGA NDASSA aliuliza:-

Suala la uwazi na ukweli katika biashara ni kitu muhimu katika kulipa kodi stahili na ndiyo maana *TRA* ikaanzisha *TIN Number* na sasa *Electronic Fiscal Divides (EFD)* kwa kila mfanyabiashara.

Je, ni kwa sababu zipi katika ukweli na uwazi zinazofanya baadhi ya kampuni kubwa za simu (*Tigo, Airtel, Vodacom*) *NBC, Madini, Serengeti, Bakhressa Group, Cocacola, Pepsi* na kadhalika kutojiunga na Soko la Hisa Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Jimbo la Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida za uwazi na ukweli zinazotokana na kampuni kujiunga na Soko la Hisa, uamuzi wa kujiunga au kutojiunga kwa kampuni kubwa au ndogo kwenye soko la hisa ni wa kampuni husika yaani *individual corporate decision*. Hii inamaanisha kwamba, makampuni hujiorodhesha kwa hiari kwenye masoko ya hisa ili kuongeza mitaji kama ambavyo yamekuwa yakitumia vyanzo vingine hususani mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu na tija iliyopo katika mfumo wa soko la hisa, Serikali imeweka vivutio mbalimbali kwa kampuni ambayo kwa hiari, itajiorodhesha katika soko la hisa.

Kwa mfano, kodi ya pato la kampuni yaani *Corporate tax* iliyojiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ni 25% tu ya badala ya kodi ya kawaida ya 30%

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa uendeshaji wa masoko ya mitaji nchini (Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – *CMSA* na Soko la Hisa la Dar es Salaam – *DSE*) imekuwa ikitoa ushawishi kwa kampuni kubwa na ndogo kuweza kutumia fursa ya upatikanaji wa mitaji kuipitia mfumo huu wa masoko ya mitaji.

Lengo ni kuongeza kiwango cha uwazi na ukweli, pamoja na kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi mpana. Aidha, juhudi hizi za Serikali bado hazijazaa matunda kwa kiwango kikubwa kwani hili ni suala endelevu na linahitaji uelewa wa dhana nzima ya umuhimu wa soko la mitaji.

MHE. EZEKIEL MAGOLYO MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nim shukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa swali hasa ni uwazi na ulipaji wa kodi wa hiari kwa Watanzania au wadau wote. Ninaomba katika msingi huo sasa niulize maswali mawili.

Kwanza, moja ya kigezo au moja ya njia inayotumika na Serikali katika kuhamasisha watu katika kulipa kodi ni matumizi ya mashine za *Electronic Fiscal Divides* na katika matumizi ya vifaa hivi yamekuwepo matatizo makubwa sana kutoka kwa wafanyabiashara kutokana na bei kubwa wanayouziwa ambayo ni zaidi ya mara tatu ya bei inayouziwa au inayo patikana kwa vifaa hivyo huko China.

Nataka kuiuliza Serikali kwamba ina mpango gani wa kudhibiti bei ya hivi vifaa EFDs ili viweze kupatikana kwa bei nafuu na hivyo wafanyabiashara waweze kuvitumia?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Pili, kwa kuwa, msisitizo wa Serikali hivi sasa ni kulipa kodi kwa kila Mtanzania na kwa kuwa kodi inatokana na kufanya kazi na kwa kuwa kumekuwepo na tatizo kubwa la upotevu wa muda na matumizi mabaya ya nguvukazi hasa kwa vijana wa mijini na vijijini ambao mara nyingi wamekutwa wakitumia muda vibaya kwa kucheza karata, pool au vitu vingine ambavyo siyo vya uzalishaji.

Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti matatizo au tabia hizi ili kufanya nguvukazi yote itumike vizuri na hivyo kuweza kupatikana au kuwawezesha Watanzania wote kulipa kodi na hivyo kusaidia kusukuma maendeleo?

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU LAMECK MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme hili suala la mashine, nampongeza kwanza Mheshimiwa Maige kwa kutambua umuhimu wa kodi na ulipaji wa kodi kwa hiari.

Hili suala la bei za mashine linatafsiriwa tofauti, kwanza mashine hizi zimewekwa order na Mamlaka ya Mapato kufuatana na mahitaji ya hapa Tanzania kwa hiyo inawezekana kuna mashine maeneo mengine zikawa na bei tofauti na hii, hilo wala hatuna haja ya kubishana. Kwetu hapa Tanzania ni kufuatana na mahitaji ya matumizi ya hizo mashine tunavyotaka kuzitumia.

Kwa hiyo, Serikali hatua ilizochukua hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri mtakumbuka tulielezea kwamba kuna hatua ambazo tulishachukua za kushusha bei, lakini tumechukua nyingine za kuondoa ushuru wa fedha kwenye uingizaji wa mashine hizo. Zote hizo ni jitihada za Serikali za kupunguza bei kwenye mashine hizo.

Lakini jambo lingine ni kama vile Serikali inawakopesha wafanyabiashara kwa sababu tumesema yeyote atakayenunua mashine na kuitumia, akapokwenda kupigiwa hesabu ya kodi anayostahili ataondoa kwanza gharama ya fedha aliyotumia kununulia mashine hiyo.

Lakini kuhusu hili la namna ya kuhamasisha watu waweze kutumia vizuri nguvukazi iliyopo, Serikali ndiyo maana ina mpango mpana kama ambavyo mliouna alipowasilisha Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia mambo ya mipango.

Tunapohusisha sekta mbalimbali za uzalishaji tunategemea ni dhahidi kwamba nguvukazi hii itakwenda kushiriki katika shughuli za uzalishaji pamoja na mipango mingine mingi ikiwemo ya kupeleka umeme vijijini kama ambavyo ulielezea jana pamoja na mipango mingine ya Serikali.

Kwa hiyo, lililopo kwa kweli kwenye hili la kutumia mashine ni waombe sanasana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, ni lazima na sisi tuingie katika matumizi ya mashine kwa sababu wenzetu tunaowatolewa mfano kama Kenya, Rwanda, Malawi na hata Zambia wamerasimisha sana sekta binafsi na ndiyo hata sekta binafsi ndiyo maana hata makusanyo yao ya kodi ni makubwa ukilinganisha na wingi wao wa wananchi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Peter Serukamba, swali la mwisho la nyongeza!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru! Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Soko la Hisa la Dar e salaam (DSE) pamoja na makampuni yanaingia kwa hiari lakini yapo makampuni hapa kama *Airtel* ambayo kuna *shares* za Serikali ni 40% kuna kampuni kama *NBC* kuna *share* za Serikali ambazo tunaambiwa zimeanza kuwa *diluted* kwa sababu hatuwekezi. Hivi Serikali ni lini sasa angalau *share* hizi za Serikali zitaletwa kwenye soko hili la hisa ili soko hili liendelee kushamiri?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU LAMECK M. MCHEMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Serukamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili suala la Soko la Hisa kuna mambo mawili makubwa. Jambo la kwanza ni kweli kabisa kuna harufu ya kuficha vitu kuhusu baadhi ya makampuni ambayo yangefaa yawe kwenye *list* lakini hayajajiorodhesha kwa sababu ukiangalia motisha zilizowekwa kwa makampuni ambayo yamejiorodhesha.

Kwanza *corporatetax* ya asilimia 25 badala ya 30, kuna *zero capital gain tax* badala ya asilimia 10, kuna *zero stamp duty* badala ya asilimia Sita, kama bado kuna makampuni yana-*opt* kutokujiandikisha unaona kabisa kwamba pale kuna giza.

Sasa niseme, pamoja na kwamba ni ya hiari kwa haya ambayo Serikali bado ina hisa ndani yake, wakati ninachangia Bajeti ya Wizara Mama niliagiza *TR* akutane na Wizara za Nishati na Madini pamoja na Mawasiliano ili kuweza kuitafsiri zile sheria ambazo ziliishapitishwa; Sheria ya Madini ya 2010 na ile ya Mawasiliano ya mwaka 2010 ili kuweza kuzitungia Kanuni ambazo zitatusaidia kwa haya makampuni ambayo bado Serikali ina hisa ndani yake ili yaweze kuingia katika uandikishwaji huu.

Nadhani tumetumia vishawishi, maadamu tunataka mapato na uwazi, tutafika hatua nyingine tutaweka kwenye taratibu hizi za kikanuni ambazo zitatusaidia kuweza kuyabana makampuni ili kuweka uwazi na kuweza kupata mapato.

Kwa hiyo, kwenye haya ambayo yanahusu mapato kwa kweli hatutaenda ka kubembelezana.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana kwa majibu ya uhakika, naona Wapinzani wote hakuna aliyesimama hata mmoja. Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh.

Na. 256

Wakulima Wanaoidai Serikali

MHE. KIDAWA HAMID SALEH aliuliza:-

Iko taarifa kwamba Wakulima wanaoidai Serikali kwa kuwakopesha Mahindi kwa Wakala wa Hifadhiya Chakula (NFRA):-

- (a) Je, deni hilo ni kiasi gani?
- (b) Je, ni lini deni hilo litalipwa?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Je, ni mikoa gani inaoongoza kwa kuwa na deni kubwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuendeleza kilimo nchini, ukiwemo mpango wa ruzuku ya pembejeo, uzalishaji wa mazao hususan mazao ya nafaka umekuwa ukiongezeka kila mwaka hadi kufikia tani milioni 5.3 za mahindi na hivyo taifa kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 118 kwa mwaka 2013/2014.

Aidha, kwa mwaka 2013/2014 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilinunua kiasi cha tani 219,377.2 sawa na asilimia 109.8 ya lengo la kununua tani 200,000 za nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wafanyabiashara binafsi kununua nafaka kwa bei ndogo kuliko bei ya NFRA wakulima wengi walipeleka nafaka katika vituo vya ununuzi vya NFRA hivyo kulazimika kupokea Mahindi yote yaliyokuwa katika vituo vya ununuzi hata baada ya kusitisha zoezi la ununuzi na hivyo kupokea ziada ya tani 19,377,282 za nafaka zenye thamani ya shilingi bilioni 9.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanda za ununuzi wa NFRA za Dodoma, Arusha, Songea na Sumbawanga zinazohusisha mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa na Katavi ndizo zilipokea mahindi mengi kutoka kwa wakulima na mawakala na hivyo kuwa na madeni makubwa ya wakulima na mawakala yaliyofikia shilingi 9,345,241,405 hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko kubwa la nafaka katika vituo vya ununuzi ukilinganisha na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina lilisababisha madeni kwa wakulima na mawakala katika maeneo yote ya ununuzi wa nafaka nchini yaliyofikia shilingi bilioni 25.4 Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 16 Aprili, 2014 Serikali kupitia NFRA ilikuwa imekamaliza ulipaji wa madeni yote na hivyo haidaiwi tena na wakulima au mawakala waliouza Mahindi NFRA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukweli kuwa NFRA siyo soko mbadala wa soko huria na haina uwezo wa kibajeti wa kununua mazao yote yanayozalishwa nchini, Serikali itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji wa masoko endelevu ya mazao ya kilimo nchini.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuruhusu uuzwaji wa mazao nje ya nchi kwa utaratibu, kuimarisha miundombinu ya masoko ili kuruhusu usafirishaji na uhifadhi wa mazao na kuboresha mfumo wa kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa mbalimbali za masoko kwa wakulima. (Makofi)

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ambayo yameleta faraja kwa kuwa Wakulima wamelipwa.

Kwa kuwa moja kati ya vyanzo vya mapato vya Halmashauri ni CESS inayotozwa kwenye Mahindi na anayetakiwa kulipa tozo hii ni mnunuzi, na kwa kuwa kuna taarifa kwamba Serikali inadaiwa malipo haya na Halmashauri mbalimbali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, Serikali itatueleza ni kiasi gani cha deni inalodaiwa kama ni CESS?

Je, ina mpango gani wa kulipa madeni haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hilo kwa kifupi Naibu Waziri Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Zambi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ambayo mpaka sasa Halmashauri zinaidai Serikali kama sehemu ya CESS ni shilingi 5, 726,370,993.50 hilo ndilo deni ambalo Halmashauri zinaidai Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba ni lini sasa Serikali italipa deni hilo. Serikali inatarajia kulipa deni hili mara fedha zitakapopatikana kutoka Hazina. Lakini pia kupitia mpango wa NFRA kuuza mahindi kwenye Shirika la Chakula, maana yake tunategemea fedha zinapopatikana basi NFRA wanaweza wakalipa madeni haya na tulitegemea kama masuala yakienda vizuri basi mara baada ya Bajeti hii kupita madeni haya ya Halmashauri yanaweza yakalipwa.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

Na. 257

Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Pangale

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza:-

Zabuni ya utengenezaji wa barabara sehemu ya Tabora hadi Pangale ya kilomita 30 iliistangazwa.

Je, ni lini kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utanza?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mkataba wa ujenzi wa barabara ya Tabora – Usesule (Pangale) kilomita 30 kati ya TANROADS na Mkandarasi *China Chongqing International Construction Corporation* ulisainiwa tarehe 31 Machi, 2014. Hivi sasa Mkandarasi yupo hatua ya kukusanya mitambo (*mobilization*) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo. Ujenzi wa sehemu ya barabara hiyo unakadiriwa kuchukua miezi 20. (*Makofi*)

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara zinazoendelea kujengwa mkoani Tabora nyingi zimeishavuka ule muda wa mkataba uliopangwa, na jambo hili

Nakala ya Mtandao (Online Document)

linasababisha hasara kubwa kwa Serikali kwa sababu kuna fedha za ziada zinazolipwa. Sasa ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwa barabara hii na nyingine nchini, Serikali imejipanga vipi ili kuhakikisha kwamba, barabara zote zinakamilika kwa muda ambao unapangwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa barabara inayotoka Sikonge kuelekea Kipili iliishahamishiwa kwa Meneja wa Mkoa wa Tabora kwa muda wa miaka Saba sasa, lakini mpaka sasa hivi sehemu ya Kiloleli – Kipili bado imebaki kama pori tu na Serikali haipeleki fedha za kutosha.

Je, Serikali inaadhi nini katika barabara hii?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali imeingia mikataba na Makandarasi mbalimbali nchini katika kukamilisha ujenzi wa barabara. Katika mkoa wa Tabora peke yake tuna mikataba ya kilomita 356 na mikataba hii ilikuwa imesainiwa mwaka 2011/2012 lengo letu likiwa kwamba ndani ya miaka mitatu iwe imekamilika. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge ieleweke kwamba, mikataba iliyopo mkoa wa Tabora sehemu kubwa inajengwa kwa fedha za ndani za Serikali. Kwa hiyo, kama hali ya Serikali kupata mapato itapungua basi kutakuwa na ucheleweshwaji wa namna yoyote wa kukamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba, ndani ya mwaka wa fedha 2014/2015 sehemu kubwa ya miradi hii itakuwa imekamilika. Mpaka sasa mkoa wa Tabora umeishapata kilomita 120 kati ya kilomita 356 ambazo zimeishakamilika kwa kiwango cha lami. Katika swali lake la pili kuhusu barabara ambayo ilichukuliwa na TANROADS, naomba Mheshimiwa Nkumba anipe nafasi niweze kujua nini kimejiri kama hiyo barabara haijaweza kutengewa fedha katika mwaka huu wa fedha.

NAIBU SPIKA: Twende swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge la Wizara ya Maji. Ni swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, kwa niaba yake Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliguna wakiashiria kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, ameruka swali)

Aah, nimeliruka swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, samahani!

Na. 258

Askari Polisi Kutembea na Silaha (Bunduki)

MHE. RIZIKI OMAR JUMA aliuliza:-

Silaha ya Bunduki hutumiwa zaidi na Askari Polisi katika lindo maalum kwa wakati maalum:-

Je, kwanini askari hao hutembea na bunduki kwa masafa marefu zaidi ya nusu kilomita kwenda kituo kingine cha kazi au kuwasindikiza Mahabusu Mahakamani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya Ulinzi na Usalama likiwemo Jeshi la Polisi vimepewa mamlaka ya kisheria ya kubeba na kutumia silaha za moto na za baridi.

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura 322ya Sheria za nchi sambamba na Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (PGO. 276) vinaanisha uwezo na taratibu za kukabidhiwa na kutumia silaha zikiwemo za moto kwa askari katika utekelezaji wa majukumu yao. Sheria na Kanuni hizo zinaruhusu askari kubeba silaha wanapokuwa kazini katika mazingira ya eneo la kituo chake cha kazi. Hii inatokana na mafunzo maalum waliyopewa katika ulinzi wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kwamba askari anapoonekana amebeba bunduki ni sehemu ya wajibu wake kisheria.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamajibu yake, lakini ninaomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mara nyingi baadhi ya askari hutumia fursa hiyo ya sheria kwamba ni sheria kubeba siraha hutumia fursa hiyo kuwachukua mahabusu/watuhumiwa kutoka kituo cha Polisi hadi Mahakamani na ambao ni watuhumiwa pengine wa makosa madogo madogo tu kama wizi wa kuku kwa kuwachukua na pingu na bunduki, huwaongoza hadi Mahakamani kwa njia ya miguu jambo ambalo linaonesha kumdhaliisha na kumuadhibu mtuhumiwa kabla hajatiwa hatiani.

Je, Serikali inaonaje kumtoa mahabusu kwenda naye Mahakamani kwa kutumia gari badala ya kutembea kwa miguu na silaha jambo ambalo linaleta sura mbaya kwa mtuhumiwa ambaye hajatiwa hatiani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Ulimwengu wetu huu wa leo umebadilika sana, askari wanapokuwa pamoja (*in group*) wanapotembea na silaha angalau inakuwa na afadhali, lakini wakati mwingine tumeshuhudia askari mmoja peke yake anatembea na silaha jambo ambalo linaweza likaletwa madhara kwake au kwa watu wengine kwa pengine ama silaha kuporwa na badala yake ikaenda kutumika vibaya na majambazi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaonaje suala hili tukaliangalia vingine ama kama ni kurekebisha sheria au tukalitafutia utaratibu mwingine? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kumswaga mtuhumiwa kwa miguu barabarani!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ni kweli inaweza ikatokea kuonekana mahabusu wamefuatana na askari mwenye bunduki na pengine ana pingu, lakini kiutaratibu hiyo inatakiwa iwe imetokea kwa nadra sana. Mahabusu wote wanatakiwa wasafirishwe kwenda mahakamani kwenye magari maalum, na uchukuaji wa silaha katika kuwapeleka ni sehemu ya kuhakikisha kwamba, wao wanalindwa kwa sababu baadhi ya mahabusu pia wamewakosea watu na wanawatafuta hata ili wawadhuru. Kwa hiyo, isionekane kama ni udhalilishaji kuliko pengine kuhifadhi maisha ya mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba kisheria askari mmoja haruhusiwi kutembea na bunduki. Utaratibu wa kipolisi ni kwamba silaha inailinda silaha, lazima pawe na angalau bunduki mbili kwa maana ya askari wawili ndiyo wanaweza kutembea na silaha. Kama imetokea kuonekana askari peke yake ni jambo la ajabu na likitokea tena tuambizane ili tuchukue hatua. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

Na. 259

Maeneo ya Vyanzo vya Maji Kupewa Kipaumbele cha Huduma

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI) aliuliza:-

Sera ya Maji inatamka bayana kuwa eneo lenye Chanzo cha Maji litapewa kipaumbele katika kuwafikishia huduma za maji wananchi wa maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali itasambaza maji katika vijiji vya Kata ya Mugango na vijiji vyote ambavyo bomba la maji la Kiabakari – Butiama limepita?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliweza kutekeleza mpango wa muda mfupi wa kukarabati mradi wa majisafi wa Mugango - Kiabakari ambao umechakaa. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, kiasi cha shilingi milioni 250 zilitumwa. Fedha hizo zilitumika kwa kununua pampu, mabomba na viungio vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu Wizara imeajiri Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya kina ya usanifu uliokamilika mwaka 2011 na kuandaa vitabu vya zabuni.

Mradi huu unahusisha miji midogo ya Mugango, Kiabakari na Butiama pamoja na vijiji ambavyo vimepitiwa na bomba kuu. Baada ya hatua hii, kibali kitaombwa kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) kwa ajili ya kutangaza zabuni za ujenzi wa mradi huo.

Tayari makubaliano ya kutoa fedha za ujenzi wa mradi huo wenye gharama ya dola za Kimarekani milioni 30.69 umesainiwa kati ya Serikali ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kiarabu ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi (SFD).

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya mapitio ya kina ya usanifu na kuanza kazi za ujenzi wa mradi. Ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi. *(Makofi)*

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Naibu Waziri kwa namna anavyofuatilia vizuri miradi ya maji, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kabisa Sera ya Maji nchini inatamka bayana kuwapatia wananchi maji waishio umbali wa kilomita 5.8 kutoka chanzo cha maji, na kwa muda mrefu wananchi kutoka Kata za Etaru, Negini, Nyakatende, Tegeluka, Kiliba na Mlangi ambao wako umbali wa Kilomita mbili (2) mpaka Nne(4) tu kutoka chanzo cha maji hawana maji safi na salama.

Je, Waziri haoni sasa ipo haja ya kutumia fedha hizo kwa ajili ya kuwapatia wananchi hawa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, fedha zinazotamkwa kwenye swali la msingi zinategemewa kutoka kwenye Benki ya Kiarabu. Endapo fedha hizo hazitapatikana kwa wakati.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaahidi nini Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitegemea mradi wa Mugango – Kiabakari mpaka Butiama? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba, ni Sera yetu ya Maji kwa maana ya kuwapatia wananchi huduma ya maji ambao hukaa katika chanzo kwa mita 400. Nataka tu nimhakikishie kwamba Kata alizoitaja Mheshimiwa Kirigini za Tegeruka, Kiriba, Itaru na Mlangi zitakuwepo katika mpango huu wa muda mrefu wa kutoa maji katika Mugango - Kiabari mpaka Butiama. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kwamba watapatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhusu kauli ya Serikali na hasa makubaliano ya Benki ya BADEA na Serikali endapo fedha hizo hazitotoka. Nataka nimhakikishie tu kwamba, tunaheshimu sheria na makubaliano. Tayari Serikali na hao wahisani tumeshatiliana sahihi juu ya kutoa hizi fedha. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi ambao Mheshimiwa Rose Kirigini amewaulizia swali wakae tu kwa mkao wa kutoa ushirikiano kwa Serikali mara mradi huu utakapotekelezwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuwa muda hauko upande wetu naomba sasa tuendeleo na matangazo kama ifuatavyo:-

Kwanza, ningependa kuwatambulisha wageni. Tunao wageni wa kutoka nchi jirani ya Kenya kutoka Bunge la County ya Taifa Taveta nchini Kenya ambao wako kwenye Gallery ya Spika pale na nitawataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Maganga Meshack Maghanga ambaye ni Spika wa Bunge la Taita Taveta, Bunge la County. Mheshimiwa Chrispus Masaga Tondoo, Naibu Spika wa County hiyo hiyo ya Taveta; Mheshimiwa Cromwel Mwariga Baridi, Kiongozi wa Shughuli za Country Bungeni. Karibuni sana. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Pia yupo Mheshimiwa Ronald H. Sagurani, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwenye Bunge hilo la County ya Taveta. Ahsante sana wanaopiga makofi huko ni Wapinzani wenzako. (Makofi)

Mheshimiwa Jason Tuja Mwamodenyi ni Mnadhimu Mkuu wa Country hiyo; Mheshimiwa Godwin Mwamodo Kilele, Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani. Karibuni sana. (Makofi)

Pia wako Wabunge Mheshimiwa Hope Sanguli Mwakio, Mheshimiwa Haris Keke Nganga, Mheshimiwa Reuben Kipampi Tiges, Mheshimiwa Raymond Yowel Mwangola, Mheshimiwa Flumence Mshila Mndwadimisha, Mheshimiwa Naima Saleh Ahmed, Mheshimiwa Paul Waweru Mwangi. Karibuni sana. (Makofi)

Pia wamefuatana na Katibu wa Bunge lao la County ya Taveta ambao ni Ndugu Michael Bidii Ngala pamoja na *Principle Hansard Editor* kutoka County hiyo Ndugu Milka Nyambura Mwarigha. Karibuni sana ndugu zetu kutoka nchi jirani ya Kenya na hasa County ya Taveta ambayo tunapakana nayo, ni majirani kabisa wanapakana na Jimbo la Mheshimiwa Profesa Maghembe hapa ambaye ni Waziri wetu wa Maji hapa nchini. Naambiwa kule Taveta mnaongea Kipare kama huku Tanzania. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni wawili wa Mheshimiwa Pindi Chana ambao wanatoka Chuo cha Mipango, Ndugu Donatha Mlowe na Ndugu Omar Omari, pale mlipo simameni. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), Ndugu Geoffrey Lepana kutoka Marekani, *State of North Carolina* ambaye ni Mwenyekiti wa Watanzania wanaoishi kwenye State hiyo ya *North Caroline*. Karibu sana Ndugu Lepana, utupelekee salamu kwa Watanzania wenzetu walioko huko *North Caroline* na Marekani kwa ujumla wake. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa James Mbatia wawili, Ndugu Tuju Martin Danda, Msaidizi wa Mwenyekiti wa Taifa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya NCCR-MAGEUZI; Ndugu Rodrick Mmanyi, Kamishna wa Mkoa wa Kilimanjaro wa Chama cha NCCR-MAGEUZI. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, ni viongozi wa CHADEMA 12 kutoka Kata ya Mkonze, Tawi la Miganga wakiongozwa na Kamanda Ludovick. Wale wageni wa Mheshimiwa Kasulumbayi 12, pale mlipo. Karibuni sana, ni wawili tu sio 12. Ahsante sana. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa James Daudi Lembeli kutoka Jimboni kwake, ni watatu Mheshimiwa Dowa Magingi, Diwani Kata ya Nyankende; Ndugu Shija Felician, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Shinyanga; Ndugu Paschal Ntale, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Kahama. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes kutoka Jimboni kwake ni Ndugu Justin Fidelis, Diwani Kata ya Nyakabanga, karibu pale ulipo Mheshimiwa Diwani yuko pale. Padri Israel Fidelis kutoka Shirika la Damu Takatifu ya Yesu; Ndugu Severian Saulo, Mwenyekiti Kitongoji cha Kanoga, Kijiji cha Buhora. Karibuni sana. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga ni Ndugu Felician Kigawa, Diwani Kata ya Mngeta, Wilaya ya Kilombero. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na Wana-AZAKI 40 wanaofanya Maonyesho katika viwanja vya Bunge. Wana-AZAKI wale ambao mpo hapa mlioandaa Maonyesho katika Uwanja wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowatangazia jana yako Maonyesho kwenye *Car Park* yetu ambao yameandaliwa na Wana-AZAKI wasiopungua 65 wa Mashirika mbalimbali. Nawaomba kwa wakati wenu kila mmoja akitoka au wakati wa mchana atembelee mabanda yale aone kazi nzuri inayofanywa na Wana-AZAKI, Bunge linakupongezeni sana na karibuni sana Dodoma. Maonyesho haya yanakwisha kesho, kwa hiyo, jitahidi kati ya leo na kesho kuweza kuhudhuria. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 43 kutoka Chuo cha Mafunzo ya Sayansi ya Afya Kolandoto Shinyanga. Wanafunzi wale kutoka Kolandoto Shinyanga simameni. Karibuni sana sana, wote wale mnaotoka Kolandoto Shinyanga, Chuo kile ni kizuri sana, kinafundisha masuala ya afya tunawataki kila la kheri katika masomo yenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia naomba niwatambulisha wageni wangu ambao wanatoka Kongwa, tukianza na wale walioko pale kwenye *Gallery* ya Spika, mwakilishi wa Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka Kongwa, Mheshimiwa Godwin Mkanwa, naomba usimame. Katibu wa CCM wa Wilaya ya Kongwa, Ndugu Ali Kidunda. Katibu wa Siasa na Uenezi kutoka Kongwa, Mheshimiwa Julius Lepumwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Katibu Msaidizi Ndugu yangu Masimami Javan; Katibu wa Uchumi, Ndugu Mussa Chiwanga; Katibu wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Kongwa, Ndugu Asia Alamga; Katibu wa Wazazi Rose Mlaki, na Katibu wa UWT Kongwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Pamoja nao viongozi hawa wa Wilaya, wamekuja viongozi wa CCM kutoka Kata zote 22 za Kongwa ambao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata wote, Makatibu Uenezi wote na Makatibu wa Kata wote. Pale mlipo naomba msimame viongozi kutoka Kongwa. Mnakaribishwa sana Bungeni, mnamwona Mbunge wenu kazi anayoifanya, anafanya kazi nzuri sana Bungeni. *(Makofi)*

Kwa wale wasioifahamu Kongwa niwaambie tu kwamba, vitongoji vyote vya Kongwa viongozi wake ni CCM; Wenyeviti wote wa Vijiji Kongwa, ni CCM, Madiwani wote Kongwa ni CCM; Mbunge wa Kongwa ni CCM, kwa hiyo, kule hakuna makandokando. Nawapongezeni na karibuni sana Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile nina matangazo ya kazi. Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, saa 7.15 mchana kuna kikao katika ukumbi Na. 227.

Kamati ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, mnaombwa mkutane saa 5.00 asubuhi mara baada ya maswali, ukumbi Na. 227. Itakuwa ni mara tu baada ya kumaliza matangazo haya.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mwelekeo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa kama tunavyokumbuka kwamba kinachoendelea mbele yetu ni majadiliano kuhusu hotuba aliyotuletea Mheshimiwa Stephen Wassira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kuhusiana na mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Lakini pia hotuba ya Bajeti iliyosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ambayo inahusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kwa hiyo, naomba sasa tuendelee na uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Peter Serukamba, ajiandae Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. Mheshimiwa Serukamba!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika Wizara ya Fedha. Kwanza niwapongeze, lakini nimeisoma vizuri hotuba ya Waziri wa Fedha. Nina mambo mawili, matatu ambayo ningependa nichangie. La kwanza, ni matumizi ya Serikali. Bado tatizo la matumizi ya Serikali ni kubwa, umefika wakati sasa na naungana na Kamati ya Bajeti kuamua sasa tuanze kupunguza matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuendelea lazima uwe tayari kujinyima. Wako watu wanasema ukikata matumizi ya Serikali baadhi ya Wizara zitashindwa kufanya kazi yake, lakini tumeona bajeti hii inayokwisha mwaka huu, bado kuna fedha hazijakwenda na hakuna Wizara iliyosimama kufanya kazi yake. Fedha za Maendeleo hazijakwenda, hakuna Wizara iliyoshindwa kufanya maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida pia hazikwenda. Kwa hiyo, naunga mkono kupunguza hasa kwenye yale mafungu ambayo ni *unrestricted* ili fedha hizo tuzipeleke kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Reli ya Kati; umefika wakati jamani Serikali tufanye maamuzi. Reli ya Kati maneno ni mengi sana; wako watu wanasema twende kwenye *standard gauge*, watu wanasema twende kwenye *PPP*, kila mtu ana *story* yake. Watanzania wanataka tufanye maamuzi kwenye Reli ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwenda kwenye *standard gauge*, lakini tunakwendaje na reli iliyopo lazima iendeleo kufanya kazi. Reli hii ya leo ili iweze kufanya kazi ambayo ipo lazima tuwe na vichwa 60, tuwe na mabehewa yasiyopungua 274, lakini leo Serikali ina vichwa 21. Tunaomba Serikali angalau tufike vichwa 30 ili reli hii iendeleo kufanya kazi. Wakati reli hii ikiendeleo kufanya kazi na ujenzi wa *standard gauge* uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 gharama ya kujenga kilomita moja ya reli kwa *standard gauge* ilikuwa Dola milioni moja. Naamini leo 2014 gharama itakuwa ni karibu 1.5 *million Dollars*. Sasa kama Serikali wako watu wanasema twende tukakope, sawa, lakini nasema sio lazima tukope fedha zote hizo. Tukikimbilia kukopa sana tutapata matatizo katika kuendesha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Serikali iamue, tunajenga *standard gauge* kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kilomita 200, ukiweka shilingi bilioni 500 tena kwenye bajeti tu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

utaanza hiyo kazi. Wakati unajenga na reli inaendelea, masaa 12 unapitisha reli, masaa 12 unajenga, wenzetu wamefanya. Ukishafika Morogoro unaanza ku-operate standard gauge kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Kwa hiyo ile meter gauge itakuwa inaanzia Morogoro. Miaka mingine unakwenda mpaka Dodoma in the span ya miaka mitano utakuwa umemaliza mpaka kufika Kigoma, mpaka Mwanza mpaka Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuwa unajenga na bado unaendelea kufanya biashara ya reli yako na ukimaliza sasa itakuwa ni cheaper kuliko ukienda hii route ya kukopa mabilioni ya Dola kwa ajili ya kujenga hii reli, halafu usubiri umalize kujenga ndio uendelee. Kwa hiyo, naomba sana Serikali tufanye maamuzi ili tuweze kwenda mbele na iweze kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, property tax. Najuliza Serikali kuna kigugumizi gani kwenye kukusanya kodi ya majengo. Ningeomba Serikali, Waziri wa Fedha njoo na pilot project anza na Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma. Ili uweze kukusanya kodi hii kuna mambo lazima ufanye, tuhakikishe kila mwenye nyumba katika miji hii ana hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwenye nyumba akiwa na hatimiliki, una hakika utapata land rent na una hakika utapata property tax. Sio hayo tu, watu wote wakishapata hatimiliki ya nyumba zao, watu hawa sasa watakuwa wanakopesheka na risk itakuwa imepungua. Risk ikipungua maana yake na entry set zitashuka. Kwa nini hatufanyi sielewi! Ningeomba Serikali wakati inakuja kujibu hapa ituambie tunafanyaje ili kuhakikisha tunaanza kukusanya property tax.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la PPP. Suala la PPP tumelisema sana, toka nimeingia Bungeni huu ni mwaka wa tisa tunaongea habari ya PPP, lakini kila siku tunaambiwa sheria, sheria ikaja, sasa hivi tunaambiwa hapana tunakuja kufanya amendment ya sheria. Hivi tutafanya sheria mpaka lini? Jamani maendeleo yanatusubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya miradi ya bandari, viwanja vya ndege, baadhi ya barabara, baadhi ya miradi ya umeme tungekwenda kwenye PPP ili fedha hizi tuziokoe ziende kusaidia kwenye elimu, kilimo na afya. Kwa nini hatufanyi sijui na tukikaa hapa tunasifia China imeendelea, tunasifia Malaysia imeendelea, Singapore imeendelea, Indonesia imeendelea, India imeendelea, South Africa imeendelea, lakini ukienda kwa wenzetu model yao ya kuendesha economy wanafanya na PPP.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna tatizo gani? Kama PPP hatuwezi, of course najua unapoamua kwenda kwenye PPP lazima uwe na mindset ya kuheshimu wafanyabiashara, lakini kama stahili ya Serikali hii ya kutoheshimu Private Sector hatuwezi kwenda kwenye PPP. Maana kuna watu wanaamini Private Sector ni wezi tu, siamini kama ni hivyo. Hizi nchi ambazo tunazisujudia, nenda Marekani, Marekani wanaheshimu Private Sector.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ule wa mdororo wa uchumi Marekani kiwanda cha magari General Motors ilikuwa inakufa, ni ya Private people. Rais Obama akaamua akaweka mabilioni ku-bail-out kwa sababu gani? Kwa sababu anajua pale kuna kodi, anajua kuna kazi, lakini sisi hapa unaweza ukakuta Waziri anasimama hapa anasema hawa wafanyabiashara hamna kitu. Hii nchi gani hii! Haiwezekani, tuwe hatuheshimu Private Sector. Hatuwezi kuendesha nchi hii kwa sisi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Mashirika zaidi ya 348 nchi hii, tumeyaua wenyewe hapa. Hakuna hata mtu mmoja aliyepo gerezani. Tumeua Mashirika yote, sasa tumesema

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tubadilike, twende kwenye *Private Sector*. Viongozi mnakuja hapa mnasema *Private Sector* haifai, nani amesema, lakini *Private Sector* ya Wazungu ndiyo inafaa, *Private Sector* ya Waarabu ndiyo inafaa, *Private Sector* ya Wahindi ndiyo inafaa. Ukishakuwa *Private Sector* ya Watanzania haifai. Nani amesema? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja hapa ambao watu hawaupendi sana. Ilikuwa *OFIL*, amekuja hana hata shilingi moja, akapewa kitalu, Mheshimiwa Ngeleja huyu anajua hapa. Akapewa kitalu, akatoka akaenda kumchukua Bill Gates, akamwambia njoo mimi nina kitalu. Alipokuja akapata asilimia 25, leo hii ni bilionea na alikuja na *briefcase*. Linapokuja suala la Mswahili, tunasema Mswahili anatakiwa akauze karanga, Mswahili akauze mchicha, nchi gani hii! Huyu *OFIL* leo kwa sababu yeye sio Mswahili ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tubadilisha *mindset* yetu. Hatuwezi kuendesha uchumi huu kwa mawazo ya kuchukia wenzetu, kwa mawazo ya kuchukia *Private Sector*. Kama tukiendelea namna hii, leo Kenya inapiga hatua kwa sababu ya *Private Sector*. Wenzetu wote wanakimbia kwa sababu ya *Private Sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu alisema jana hapa kuwa, walikuja *ILLOVO* hapa tumeingia nao ubia tena 25% tu, wakaomba ardhi tukawanyima, tunaingia mlango huu na kutokea mlango huu. Wakaenda Zambia, wakapokelewa na Makamu wa Rais na Serikali nzima ikawa inawatunza kama watoto wadogo, imewapa ardhi, imewapa *incentives* na leo Zambia ni *second producer* wa sukari in Africa, mtaji ambao ungekuja Tanzania, lakini kwa sababu ya staili yetu, hakuna anayejali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa ya nchi hii tumeamua kuwa wabinafsi sana, tumeamua kuendesha Taifa hili kwa ubinafsi na kila mtu anajifikiria yeye na familia yake. Ndiyo maana *Education* inakufa *we don't care*, Afya inakufa, hakuna anayejali kwa sababu sisi ambao tuko hapa ambao tunafanya maamuzi nikiugua nitakimbia India, nitakimbia *South Africa*, watoto wangu watasoma nje ya nchi, kwa hiyo tumeamua kuwa *too individualistic to the extent* hatuwafikiri wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea habari ya ajira, hakuna na ukisikiliza *statement* ya Serikali *as if* ajira siyo tatizo. Kweli mnasema ajira siyo tatizo, nashangaa sana! Darasa la saba wanamaliza ni wangapi wanakwenda sekondari? Wale waliobaki wanakwenda wapi? *Form Four* wale waliofeli wanakwenda wapi? *Form six* wale waliobaki wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kuwa Taifa letu kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka hamsini ni 91% ya *population*, kama sisi ambao tuko katika madaraka hatuhangaiki na hili kundi *a very young Nation* hatuhangaiki nalo tunaleta Sera tu kwa sababu ni Sera, tunalo tatizo kubwa sana. Wapiga kura kuanzia miaka kumi nane mpaka miaka thelathini na tisa ni 78%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, lakini niombe Serikali ije na majawabu ya matatizo ya wananchi. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa mchango wako. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti. Kwa kuanza nitoe angalizo tu kwa watu wanaoendesha nchi hii kwa *slogan*, sasa hivi wamekuja na *slogan* wanawaambia vijana waache kulalamika. Sasa nawaambia hivi watu hawalalamiki bado watu wana-*fight*, wale vijana elfu waliokwenda

Nakala ya Mtandao (Online Document)

uwanja wa Taifa wakianza kulalamika na kuingia msituni, ndiyo tutajua kuwa wameanza kulalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo napenda kutoa mawazo yangu kwamba, hatutaweza kukuza uchumi wala ajira za Taifa hili kama hatuta-*promote small businesses*, biashara ndogondogo ambazo zinaajiri watu wanne, watano, zinaajiri mpaka juu hapo hamsini, siyo lazima kuwa ajira zote zitoke *Vodacom, Tigo* au Serikalini au Halmashauri tu *promote* hizi biashara ndogondogo. Napenda kusema tuige kule tunakokwenda, tujifunze nchi kama Marekani, ukiweza kufungua hata *McDonald* ambapo utaajiri watu wanne, watano tu unapewa *green card*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaji wa kufungua hicho ki- *McDonald* ni kama Dola laki moja, Dola laki moja na ishirini na tano hapo unafungua ki-*joint* unaajiri vijana wanne, watano, Mmarekani anakupa na *green card* kabisa, anakwambia Mzee kaa, kwa sababu *Small Businesses* ndiyo zinazotoa ajira kwa watu wengi, ndiyo mpango mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachotakiwa kufanya ni ku- *promote small businesses* tuwawezeshe na kuwapunguzia zile kero zao katika kuendesha biashara zao ili wawe na uwezo, badala ya mwenye baa kubwa kulipa watu elfu thelathini kwa mwezi, awe na uwezo wa kumlipa hata laki moja na nusu au laki mbili kama siyo laki tatu, yaani *small businesses* ziweze kwenda hata 70% ya kima cha chini cha mshahara ambacho Serikali inatangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndipo unaweza kupeleka maisha bora kwa wale yaani haitakuwa *issue* kwa mwanafunzi kufanya *part time* kama wanavyofanya Ulaya. Unakuta mwanafunzi wa Chuo Kikuu, lakini jioni unamkuta *Pub* anafanya kazi kwa sababu ujira ni mzuri na mazingira ni mazuri na wale wateja wenyewe wanalipwa vizuri, ni wafanyakazi, wanatoa *tip* nzuri, kwa hiyo, maisha yanakwenda kwenye *businessess* na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba niende kwenye hotuba ya Waziri wa Afya, ukurasa wa 34, kwenye kipengele cha mgawanyo wa fedha katika sekta. Nakwenda kwenye Sekta ya Afya nikinukuu wanasema: "Jumla ya shilingi bilioni elfu moja mia tano na hamsini na nane pointi mbili zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madawa kuzuia magonjwa ya mlipuko, chanjo za watoto, ujenzi wa Zahanati na kudhibiti UKIMWI na Malaria."

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona maslahi ya Madaktari kwa sababu mara nyingi humu ndani tumekuwa tukiongelea matatizo ya afya kutokea upande wa wagonjwa, lakini hatujapata fursa ya kujadili kwa uwazi maslahi ya Madaktari. Juzi nilikuwa Mbeya kwenye Kikao nikaitwa na Madaktari karibu kumi na sita, kumi na nane, nikakaa nao wakaniambia *concerns* zao kuwa, kwa nini mambo haya yakirekebishwa basi huduma za afya zinaweza kuboreka na kila kitu kikaenda sawa.

Moja na hii ndiyo *note book* niliyotumia *straight* siku ile kuandika. Moja, wanasema maslahi zaidi *call allowances*, Madaktari wa Rufaa Mbeya mpaka naongea nao walikuwa hawajapata *Call allowances* kwa takribani miezi sita nyuma. Wakati hizi *call allowances* ndiyo fedha pekee ambazo zinawasaidia katika kujikimu kwa sababu mishahara haiendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananiambia wale mabawana kwamba mtu anapelekwa Mbeya anakaa Hospitali ya Rufaa au Hospitali ya Mkoa mpaka miaka sita hajathibitishwa wakati anatakiwa athibitishwe kwa mwaka mmoja. Baada ya mia sita akithibitishwa mshahara ule wa kuthibitishwa mpaka uje ni miezi tisa mpaka miaka miwili. Mbaya zaidi anapokuja sasa kwamba analipwa halipwi *arrears*, halipwi yale malimbikizo ya nyuma anaambiwa tu kwamba sasa umeanza kulipwa endelea na kazi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama haya sidhani kama Madaktari kweli wanaweza kufanya kazi kwa dhati na huduma za afya zinaweza zikaboreka wakati wao ndiyo msingi wa maboresho yote ya huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za likizo hakuna na hata zikipatikana wanaambiwa kwamba, mwaka huu unakwenda likizo unalipwa, mwakani hulipwi, sijawahi kusikia kitu hiki, ninavyojua ukienda likizo kila mwaka unatakiwa kupata stahiki zako. Sasa hawa wanaambiwa kwamba mwaka huu unalipwa na mwakani hulipwi kwa kweli Madaktari wa Rufaa Mbeya na najua hili lina-reflect kwa Madaktari wote wa nchi hii wa Peramiho na sehemu zote. Pia wananiambia kuwa kuna ucheleweshaji wa kupanda vyeo na mishahara inachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Housing Allowance*, hiki ni kitu muhimu sana kwa sababu zamani sisi tulipokuwa wadogo, Madaktari wote walikuwa wanakaa uzunguni. Mtwara kule walikuwa wanakaa Shangani, Mbeya wanakaa Uzunguni, Arusha sijui wanakaa wapi kwenye nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa nyumba za Serikali zote tumeuza na hatuna sehemu za kuwaweka Madaktari, Madaktari wanatakiwa kupewa *Housing Allowance*, lakini sasa ile *Housing Allowance* japokuwa nakumbuka wakati wa kasheshe ya Dkt. Ulimboka humu ndani nilisikia Waziri Mkuu aliwahi kuthibitisha au ku- *concentrate* kwenye hili suala la *Housing Allowance* kwamba litaendelea kuwepo, lakini kwa sasa hivi kwa wale Madaktari wa Rufaa Mbeya ni kama huruma, kwamba wanaweza wasipewe au wapewe, sasa tunafuata nini?

Mheshimiwa Waziri Mkuu kasema kuwa hiki kitu hakitatoka *Housing Allowance*, lakini fedha haitolewi na kauli zimekuwa nyingi, wengine wanajibu wanasema Serikali inataka kujiondoa, sasa itajiondoa vipi, haiwezekani Serikali kujiondoa katika masuala ya *Housing Allowance* kwa sababu ni sehemu ya msingi ambayo inasaidia kurahisisha maisha au kupunguza machungu ya maisha ya Madaktari hasa pale inapotokea kwamba hata mishahara inachelewa kupelekwa miezi tisa mpaka miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari hawa wanalalamika kuhusu fursa za kusoma, zinatoka kiupendeleo. *Scholarships* mpaka Wizarani sijui kuwe na nani sijui kafanya nini, halafu mnasema kwamba eti watu waache kulalamika, siyo vijana tu wanaolalamika mpaka Madaktari wanalalamika. Wameniita mimi Mbunge wamelalamika kutokana na haya ninayoyasema kwamba kila kitu kwao ni kero fursa za kusoma ni kero, zinatoka kwa upendeleo, hakuna *scholarship* hasa zile za nje ndiyo hawapati kabisa hawa ndugu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye kitabu cha maendeleo, wanazungumzia masuala ya uboreshaji wa hospitali za Rufaa, Hospitali ya Rufaa Mbeya wanazungumzia ununuzi wa Vifaa Tiba na ukarabati wa chumba cha x-ray. *Issue* yetu siyo chumba cha x-ray *issue* yetu ni jengo la x-ray. Kuna jengo pale kubwa kabisa la ghorofa ambalo aliliacha Profesa Mwakyusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya mambo sijui yanakuwaje Profesa Mwakyusa ilibidi akomae tu amalize hata kama wangesema anapendelea kwao potelea mbali kwa sababu haiwezekani yeye yuko pale, ameanzisha kitu kizuri kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda jengo liko pale kabla sijawa Mbunge mpaka leo hakuna hata msumari uliopelekwa pale katika lile jengo, halafu leo unazungumzia ukarabati chumba cha X-ray wakati sisi tuna jengo la ghorofa ambalo siyo tu litakuwa na X-ray bali pia litakuwa na CT SCAN yaani ni kama jengo la mionzi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani leo hii mtu anapata tatizo anatakiwa kupigwa CT SCAN lazima aje apande gari aende Dar es Salaam afanyiwe hicho kitu, wakati tuna Hospitali ya Rufaa kubwa, nzuri, majengo mazuri, lakini haina vifaa, haina huduma nzuri na tatizo kubwa lililopo sasa hivi ni vipimo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa nataka aniambie fedha za kumaliza jengo alilolanzisha Profesa Mwakyusa wakati Waziri, siyo lazima awe Mwakyusa au awe anatoka Mbeya ndiyo lile jengo limaliziwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua kuna mkakati gani wa kuhakikisha jengo lile la mionzi au maarufu kama jengo la X-ray linamalizwa katika mwaka huu wa fedha ili kuondoa kero kwa wagonjwa wa Mbeya, ili kuondoa kero kwa Madaktari wanaofanya kazi katika Hospitali ya Rufaa Mbeya ili wawe na vitendea kazi vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikishamaliza kusema hayo, naomba nishukuru sana, lakini niseme tu angalizo, mimi siyo Mchumi na wala siyo Mtalaam wa uchumi, lakini nina uwezo wa kukaa na kuhoji ninapokaa na watu. Sasa nakaa na rafiki zangu *Bankers*, Maofisa tu nawauliza, hivi kwa nini hizi *interest rate* ambazo tunazungumzia Bungeni hazishuki, ni kubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaniambia Mzee Mabenki hayana mtaji na wao wenyewe wanaazima pesa kutoka katika mashirika mbalimbali kama Mashirika ya Hifadhi, Mashirika ya Hifadhi anasema Mzee nina bilioni mbili hapa kuna Benki inazitaka? Benki gani inakuja, wanasema ndiyo tunazitaka, wanakopesha, kwa hiyo, katika mazingira kama hayo, ni lazima *interest rate* itakuwa ni kubwa kwa sababu wao wenyewe hawana mitaji ya kutosha kwa sababu masharti ya kufungua akaunti ni magumu, vipato vya kupeleka benki hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, muangalie mkakati wa kutanua mitaji ya mabenki na mabenki yawe na fedha za kutosha na hiyo ni namna nyingine ya kupunguza *interest rate* kwa sababu kwa sasa hivi mabenki yanachofanya ni kukopa, wanaazima fedha katika mashirika mbalimbali kama ya Hifadhi ya Jamii na ndiyo wanakuja kutukopesha sisi na ndiyo maana riba inakuwa ni kubwa. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbilinyi. Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Nshunju Mshama!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kusimama tena Bungeni baada ya kutoka katika matibabu nchini India. Nawashukuru wote walioshiriki kuniombea na hatimaye Mungu amenitia nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Saada Mkuya, mwanamke mwenzetu, kwa kweli ametuwakilisha vizuri na amewasilisha bajeti vizuri sana. Mungu aendelee kumtia nguvu na Mungu aendelee kumtangulia. Pia nawapongeza Manaiibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na timu yote iliyoshiriki katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia mambo machache. La kwanza, ni jambo ambalo nimeliongelea kila wakati kwamba, wananchi wa Singida chini ya Uongozi wa Mkuu wao wa Mkoa wamejitahidi sana kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ambayo ni Hospitali ambayo ni ya Kitaifa na wala haitahudumia wana Singida tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia kwamba baada ya juhudi za Mkoa wa Singida, sasa Serikali ingechukua jukumu la kujenga hospitali hiyo hadi kuimalizia. La kushangaza, Serikali inaandaa bajeti, Bunge linapitisha na kinachopitishwa na Bunge ndicho kinachotekelezwa. Mwaka jana Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ilitengewa shilingi bilioni tatu na nusu, lakini

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mpaka hivi sasa ninavyozungumza, fedha ambazo zilikwenda kwa mwaka mzima ni bilioni moja na nusu tu bilioni mbili hazikwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisaidie hizi bilioni mbili zitapelekwa au ndiyo basi bajeti imepita na bilioni mbili zimepotea. Tunaomba sana, pamoja na bajeti hii ambayo tunajadili sasa, ikumbukwe kwamba, tunadaiwa bilioni mbili katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Mwaka huu tumeomba shilingi bilioni tatu na nusu, hivyo Serikali itambue kwamba, inatakiwa kupeleka bilioni tano na nusu kwa Mkoa wa Singida ili kuweza kusaidia kuongeza kasi ya kumalizia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ambayo tunategemea itahudumia Mikoa mitano jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema 'mcheza kwao hutuzwa', hivi kweli kazi nzuri yote hii iliyofanywa na wana Singida chini ya Uongozi wa Mkuu wa Mkoa, kweli Serikali inashindwa kuchukua jukumu hili sasa kwamba hospitali hii sasa ijengwe na Serikali na siyo kuendelea kutafuta nguvu za Wana Singida tena? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali imeona kwamba haina fedha Mkuu wa Mkoa na timu yake walishaongea na Mifuko ya Kijamii, iliongea na NSSF wamekubali kutukopesha, imeongea na PSPF wamekubali kutukopesha, imeongea na PPF imekubali kutukopesha, kinachotakiwa hapa ni dhamana ya Serikali na tunaomba Mifuko hii ipewe dhamana ili Hospitali hii ya Kifahari inayojengwa Mkoani Singida iweze kukamilika na kutoa huduma ya Taifa na siyo huduma ya Wana Singida peke yao. Naongea kwa uchungu sana naomba hili Mheshimiwa Waziri alichukue kwa uzito wa pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nimehama naingia katika suala la Bima ya Afya. Ni kweli kuwa Bima ya Afya ni chombo ambacho kinawasaidia Watanzania wakiwemo wafanyakazi na wananchi kwa ujumla kupata huduma kwa sababu Serikali inachangia nusu na wanachama wanachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza ni kwamba, mwanachama wa Bima ya Afya anatakiwa eti ajaze, ahudumiwe yeye kama mimi ni mama basi mimi na mume wangu na watoto tuliowazaa wane, lakini ikumbukwe kwamba tunalea yatima, wako wengine hawakujaliwa watoto wanalea yatima, wako wengine wana moyo wa huruma wanachukua yatima, wanawalea yatima walioachwa na wazazi wao walishatangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Sheria hii muitazame mara mbili, muilegeze, muwaingize hawa yatima, kwani imeshasemekana kwamba, mtoto ambaye hujamzaa mwenyewe haruhusiwi kuingia kwenye Mfuko wa Bima, hili mnafanya makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, legezeni hii Sheria hatuwatendei haki hawa yatima, mtoto yatima anapochukuliwa na mzazi ambaye hakumzaa akifika anajisikia kuwa huyo ni mama yake, anajisikia huyo ni baba yake. Atakaposikia kuwa yeye kwenye Bima hayupo, hata Mungu sijui kama atatuelewa. Naomba sana Waziri wa Afya, baba yangu sijui yupo au hayupo, hili jambo litazamwe upya, wafanyakazi wanalilalamikia sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika Bima ya Afya, Mwanachama wa Bima ya Afya akipoteza kadi anaambiwa alipe elfu hamsini ndipo apewe kadi. Hivi mnajua kadi zinapoteaje? Mtu anapata ajali kwenye basi alikuwa anasafiri anapoteza kila kitu na hiyo kadi inapotea, leo unataka kumpa adhabu mara ya pili alipie hiyo kadi shilingi elfu hamsini!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuiambie Serikali yetu jambo kama hili tusimuadhibu mtu mara mbili keshapata ajali, kapoteza kila kitu, leo umwombe elfu hamsini alipe kwa sababu kapoteza kadi, hivi kweli mnafikiria kuna mfanyakazi au Mwanachama wa Bima anaweza akaitupa tu kwa makusudi? Haiwezekani, naomba suala hili litazamwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia kwenye VAT kwa ajili ya wafanyakazi. Mfanyakazi huyu anapata mshahara anakatwa VAT 12% hiyo 1% hatujamsadia mfanyakazi huyu. Akienda dukani atanunua bidhaa kwa ongezeko la bei, akienda benki akikopa fedha atarudisha kwa ongezeko la bei, huyu mfanyakazi ni wapi anapata unafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuwafikirie hawa wafanyakazi hii VAT bado ni kubwa sana, ongezeko la bei ni kubwa sana 12%, kumtolea 1% hatujamsaidia mfanyakazi bado tunamuumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu alikuwa anapata posho ya kufundishia 50%, mkasema mmefuta mmeingiza kwenye mshahara. Leo mshahara unakatwa VAT huyu Mwalimu anabaki na nini? Daktari na Muuguzi alikuwa anapata posho ya mazingira magumu sasa hivi imefutwa, mnasema mmeingiza kwenye mshahara, mshahara unakatwa VAT huyu ana daktari na muuguzi anapata nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie hili suala upya, muwaondolee wafanyakazi VAT, VAT wanakatwa kila mahali wanapopita, madukani, mikopo na ndiyo maana wanajiiingiza kwenye mikopo ya mitaani isiyokuwa na kichwa wala miguu, matokeo yao wanapata matatizo. Fikirieni upya kuhusu *Pay As You Earn* ya wafanyakazi, tafadhali sana ndiyo VAT hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na suala hilo hilo la wafanyakazi. Hawa wafanyakazi pamoja na wananchi kwa ujumla, ukiingia kwenye suala la elimu wanachangia; kusomesha, kununua madawati; ukienda hospitali, wakiingia kwenye miradi wanachangia, sasa nataka niulize hivi hawa Watanzania ni kipi ambacho tunawapa bure? Hebu angalieni kitu hata kimoja, kama elimu basi muwape *offer* wasome bure. Kama ni afya ama maji basi wapewe bure. Hata kimoja tu, tuseme kwamba hiki Watanzania wetu tunawapa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na pole sana na kuugua. Mheshimiwa Assumpter Mshana atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere!

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Ntoa shukurani mbele za Mungu na Bunge lako Tukufu kupata nafasi kuchangia katika Wizara hizi zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nipongeze Wizara hii na kuanzia Waziri mwenyewe pamoja na Manaibu wake kwa kazi kubwa ambayo wameanza nayo na inaonesha kwamba kweli hawa vijana kama watasimama na mwanamke mwenzetu, tunaamini kabisa kwamba kutakuwepo badiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote nikiwa nachangia nilikuwa ni mtu wa kulalamika sana, lakini hebu leo nami nitoe shukurani kwa yale yaliyofanyika. Nimshukuru tu Waziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa namna ya pekee alivyonisaidia kufanya barabara zifuatazo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Bukoba (Bukoko-Bweyunge), Kashekya-Bishura, Kakunyu-Kakunyu Juu, Kiyango na Bubale. Namshukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru tena Waziri wa Nishati kwa kunipatia umeme. Katika Wilaya yangu ametenga Vijiji 24, lakini kubwa sana ameweza kunipatia umeme Mtukula ambapo tangu nchi imekuwepo, umeme haujawahi kutokea na sasa wanawasha umeme. Kwa kweli Mungu ambariki na aendeleo kufanya kazi bila kujali kwamba maneno maneno, wakati mwingine yanavunja mifupa lakini ajitie moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Miundombinu, lakini hizi barabara niseme kwamba barabara zangu ambayo ni barabara ya Bunanzi kwenda Minziro imetengenezwa chini ya kiwango; Hamshenye - Turuzinga, Katoma - Kashenye, Gela - Ishunju bado hazijaridhisha. Naomba katika eneo hilo iongezwe na ionekane *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu namshukuru Waziri wa Elimu, Walimu sasa nakudai wa sayansi, lakini Walimu wa kawaida nimepata. Waziri wa Afya ahsante kwa *ambulance* ambayo umenipatia. Waziri wa Maji ahsante kwa Vijiji vya Luzinga, Kata Luzinga, Bugandika, Kilimirile, Ngando na Nsunga. Kwa kweli shukurani ninazo nyingi naweza nikamaliza muda, lakini imeonesha kabisa kwamba ukipiga kelele, ukiendelea kulia kuna siku utacheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la bajeti kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kupunguza gharama za maisha ya wananchi la kwanza. Kupunguza misamaha ya kodi kama alivyoeleza, kuinua viwango vya mapato na kukusanya kodi kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu na utekelezaji wa sera ya Bajeti za Mwaka 2013/2014. Serikali imekusanya shilingi trilioni kumi mbili, bilioni 882 ambayo ni sawasawa na asilimia 70 ya makusanyo ya mapato. Swali, mapato haya hayakukusanywa vya kutosha, lakini nimuulize Mheshimiwa Waziri, katika malengo uliyoweka mwaka huu 2014/2015, una uhakika gani kwamba utakusanya wakati mwaka jana haukukusanya vya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee mwenendo wa mapato ya ndani. Malengo hayakufikiwa kwa sababu ya kutokuwa na ukusanyaji baadhi ya vyanzo vya kodi. Swali, kwa nini viwango havikufikiwa na kwa nini unaamini mwaka huu utafikia viwango hata ukaongeza matumizi ambayo tunakwenda kutumia zaidi ya bilioni 19?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine, mapato yasiyotokana na kodi. Hadi Aprili, 2014 malengo yalifikia 57%. Hii ni mbaya kuliko. Nini sasa kitakachozuia au kitakachofanya au mkakati ulionao wa kuona kwamba mwaka huu 2014, utafikia malengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee misaada ya mikopo ya nje yenye masharti nafuu. Hadi Aprili na napata hizi nipo katika Kamati ya Bajeti, misaada na mikopo ya kibajeti ilipatikana 63%; Mifuko ya kisekta ilipatikana 74%; Mikopo ya misaada na Miradi ya Maendeleo ilipatikana 55%. Swali, kwa nini hali hii ilitokea? Labda wakati Waziri anapokuja atatueleza na sasa nini kinakwenda kufanyika ili tuweze kufikia malengo na kupata hiyo mikopo ya masharti nafuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya kibiashara ya ndani, Serikali ilipanga kukopa trilioni 1.699.9, lakini Serikali ikakopa trilioni 1.803.9 kiasi kilichozidi ni bilioni 104. Je, hiki kiwango kilichozidi kibali kilitoka wapi na kwa nini wanakopa bila kurudi Bungeni kuomba kibali cha kukopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Bajeti ya Mwaka 2013/2014 yametajwa. Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba mafanikio ni ukuaji wa uchumi ambao wananchi hawajauona. Tuseme kuondoa umaskini ni lazima uangalie wananchi, kwa mfano, nikienda

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jimboni kwangu, ndiyo katika takwimu tunaona uchumi umekuwa, lakini ninavyowaona watu wangu bado viashiria vya kuonekana uchumi umekuwa sijaviona na huu uchumi haujaonekana katika mifuko ya wananchi. Mfumuko wa bei kama ulivyosema, lakini mpaka leo kahawa bei ipo pale pale na vyakula sijaona kama kweli mfumuko haupo wa kutosha kuonekana kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo swali katika hili. Je, katika kipindi kilichopita ametuambia kumekuwepo changamoto na changamoto nitazitaja; Mheshimiwa Waziri alisema tatizo la kufanya Bajeti yetu isi-*perform* vizuri kumekuwepo na changamoto. Akasema upatikanaji kwa wakati wa mikopo ya nje yenye masharti nafuu; Kuwepo kwa mahitaji makubwa kuliko kiwango tunachokusanya; Ukusanyaji usioridhisha wa mapato yasiyo ya kodi; Gharama kubwa za uendeshaji wa mitambo ya umeme; Kuongezeka kwa madai ya Wakandarasi na watu waliofanya kazi kabla hawajalipwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, nini sababu iliyosababisha tukutane na changamoto hizo? Katika Bajeti ya mwaka huu inaonekana imeongezeka, Mheshimiwa Waziri ameandaa vipi namna ya kukabiliana na changamoto ambazo ametueleza ili tuweze kufikia malengo ambayo ameyatangaza mahali hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, sera za mapato Mwaka 2014/2015, Serikali inakusudia kukusanya trilioni 12.178 sawa na asilimia 19.2 ya pato la Taifa la 53.7%. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, hizi sera hazikufanya kazi vizuri kwa mwaka uliopita, ana mikakati gani ya kututhibitishia hapa kwamba sera za mwaka huu zitafanya kazi na tutakusanya kadri ambavyo imekusudiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kwa kuwa kengele haijagongwa, naomba kuongea kwamba, mgawanyo wa fedha katika Sekta ya Nishati imepewa trilioni 1.0906, miundombinu 2.1, kilimo moja pointi, elimu 3.46, maji na kadhalika kama tunavyoona kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mgawanyo huu unajumuisha na madeni yaliyopo? Swali lingine madai haya ni kiasi gani na madeni haya yatalipwa kwa namna gani na yatalipwa lini? Ili tuweze kuona kama alivyogawa hizi fedha, je, humo ndani kuna madeni ambayo Serikali inadaiwa? Au ni pembeni? Kama ni pembeni anakwenda kuwalipa lini? Matokeo yake tumekuwa tukiona, Bajeti yetu imeshindwa kufanya kazi vizuri kwa sababu wanapopewa mgao, wanakuta wana madeni. Kwa hiyo, wanaanza kulipa madeni na matokeo yake ndiyo waanze ku-*perform*, kwa maana hiyo hakuna namna yoyote ambayo unaweza uka-*perform* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi sina, lakini naomba niunge mkono hoja, wakati atakapokuja Mheshimiwa Waziri naomba anisaidie kujibu maswali haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Assumpter Mshama. Ndugu zangu wa Kongwa ambao hamumfahamu, huyu ni mke wenu, mtajuana baadaye uko.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatibu Said Haji!

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nichangie katika hii Bajeti kuu ya nchi yetu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, trilioni 19 si jambo la mzaha, *figures* tunazo, lakini kinachotakiwa ni *implementation*. Hatuwezi kufika na hii Bajeti bila *implementation*. *Figures* pia za pato la taifa zinaridhisha, kupanda kwa pato la Taifa kwa asilimia 7% ni jambo jema na la kujivunia, lakini bado tuna changamoto katika uchumi wetu kama nchi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo mengi ya kiuchumi, lakini kinachotakiwa ni ku-*economise* haya matatizo, maana yake tuwe na vipaumbele vichache na tuvishughulikie *effectively* kwa mafanikio au matokeo makubwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna rasilimali chache ambazo pia ni changamoto, lakini tukitumia vizuri rasilimali zetu, kwa mfano, gesi hakika tutaendelea kupiga hatua na hakika tutapandisha pato letu zaidi ya asilimia saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu bado ni changa na nchi inaendelea kama nchi nyingine ambazo zinaendelea. Kwa hiyo, kinachotakiwa ili tuweze kuwa *stable* kwenye uchumi wetu ni lazima tuwe na uchumi wa kati, *integrated economy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Twende maeneo ambayo Watanzania wengi wapo. Kwa mfano, kilimo; tukienda na kuwekeza zaidi katika kilimo, hakika tutakuwa tume-*create* ajira kwa ajili ya vijana wetu. Tukiwa na viwanda vyetu, sio lazima tuwe na *heavy industries*, tuwe na *light industries* tutaweza kuzalisha wenyewe vitu vingi ambavyo tutaviuza nje, tutapata fedha ya kigeni na *reserve* yetu ya *foreign currency* itaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuimarisha rasilimali watu tuliyonayo. Ndiyo muhimu na itakayojenga taifa letu na kuendeleza uchumi wetu. Bila ya kuwa na rasilimali watu, yenye utashi wa kufanya kazi, kupigania na kulijenga Taifa hakika tutakuwa tunapanga mipango ambayo haitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la kodi. Umewahi kusikia Taifa lolote ambalo limeendelea bila ya kulipisha kodi wananchi wake, hakuna! Ukitaka maji safi ni kodi, ukitaka elimu bora, ni kodi, ukitaka miundombinu, ni kodi; ukitaka viwanda viendeleo, ni kodi; ukitaka barabara na reli vyote vinataka kodi, lakini tatizo suala la kulipa kodi Tanzania limekuwa kama ni adhabu. Watanzania hawajaeleweshwa kwamba kulipa kodi ni wajibu wa kila mwananchi, ili tuweze kuendelea na sisi. Tumekaa tunatamani nchi zilizoendelea, mnafikiri wameendelea vipi? Wameendelea kwa sababu ya kulipa kodi. Ukikuta Mji ni msafi, ni kwa sababu wakazi wa Mji huo wanalipa kodi wanachangia usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa ruhusa yako nipitie utaratibu wa walipa kodi wa nchi zilizoendelea. Hii fomu hapa; wananchi huhamasishwa kwa kurudishia kiasi cha fedha wanazolipa kwenye kodi zao. Mfano, kuna fomu kama hii inatumika kwa walipa kodi nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa kwanza wanakwambia *individual income tax return*, hapa *information* zako zinaweka, kipato chako, kama una watoto wanakutegemea, kama umelipa ada ya shule na kama umelipa mikopo ya shule. Ukurasa unaofuatia pia wanakuonesha kwamba kama wewe ni mlipa kodi ambaye huna watoto wanaokutegemea, *information* zako zipo hapa ukurasa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa mwingine unaonesha kama umepata *profit* wewe ni mfanyabiashara mkubwa au wa kati, *information* zako zinakuja hapa zote. Kama wewe ni

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mjasiriamali, Machinga au ni mamantilie wana hii hapa *section* kwa ajili ya watu kama hawa na baada ya kuweka hizo *information* kuna *program* ambayo hufanya *calculation electronically* na kubaini kwamba kodi uliyolipa ni sahihi na pengine unatakiwa kufidiwa, urudishiwe kiasi cha fedha. Ndiyo maana wenzetu wa nchi zilizoendelea, wananchi hawalazimishwi kulipa kodi. Wananchi huenda wenyewe kila mwaka, wanakwenda kudai, wanataka ku-*file income tax* ili wapate marupurupu ya kurudishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tuna Waziri makini na Manaibu wake wote ni makini, wasomi, Wachumi, wana *exposure* wote. Naomba walifanyie kazi hili, ili hatimaye sasa Watanzania waachane na zana za kufikiria kwamba kulipa kodi ni adhabu. Hatimaye sasa Watanzania wawe wanakwenda kwa ma-*agent*, wanaomba fomu za kulipia kodi za ku-*file report*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kodi pekee haitoshi, tunahitaji uzalendo. Narudia tena uzalendo! Watanzania hatuna. Tunahitaji uzalendo ili tuweze kulijenga Taifa letu, kulipa kodi ya kutosha hatimaye tulete maendeleo katika Taifa letu, tunahitaji uzalendo ili tuweze kujenga Taifa letu, vinginevyo hatuwezi. Watu wengi wamekuwa wakilalamika tu kwamba, watu wanatumia fedha za walipa kodi visivyo, je mnalipa kodi? Au ni maneno tu? Watanzania wenzangu tuachane na maneno. Tunapenda maneno bila vitendo, kama wewe unajua onesho vitendo, sio unajisifia tu kwa maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi naomba ninukuu, kuna Mwandishi mmoja alisema kwamba *people don't care how much you know, until they know how much you care*. Maana yake ni kwamba watu hawajali kuhusu ujuaji wako mpaka watakapojua unajali kiasi gani. Kwa hiyo, wale wanaodhani wanaelewa wanajua sana, waweke ujuaji wao kwa vitendo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunapofanya kazi, Watanzania wanaofanya kazi au Serikali inapofanya kitu tujifunze kuwa na ustaarabu wa kawaida wa kuwasifu ili tuwatie moyo, lakini siyo unabeba tu, mtu kakuletea maji, Kwimba wametuletea maji. Kwa nini nisiseme ahsante kwa Serikali yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pinda ametuletea bwawa kubwa Kwimba. Kwa nini nisiseme ahsante kwa Serikali yangu. Kwa sababu hata mimi ni Serikali yangu. Tumeletewa Walimu, Mheshimiwa Majaliwa kaniongezea Walimu 300. Nisiseme ahsante kwa nini? Tuwe na ustaarabu wa kawaida wa kutiana moyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakwambia asante sana kwa shukrani ulizozitoa. Mheshimiwa Khatib Said Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami. Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mungu kunijalia kusimama ili nitoe yangu machache kuhusu bajeti yetu hii. Nianza na utangulizi wa kusema nimefurahishwa sana na lile ulilolisema kuhusu hali ya Kongwa na wageni wako. Nimefurahia zaidi ulivyosifia kuanzia ngazi ya chini mpaka Mbunge wewe kuwa mnatoka Chama cha Mapinduzi. Hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishangaa ya Kongwa subiri ya Pemba. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Konde. Jimbo la Konde kuna Madiwani wanne wote ni Chama cha Wananchi (CUF). Mheshimiwa niko katika Wilaya ya Micheweni ina Majimbo manne ya uchaguzi. Majimbo manne yote ni Chama Wananchi (CUF). Wabunge wote na Madiwani wao. Hilo dogo subiri

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kubwa, natoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, una majimbo tisa ya uchaguizi. Yote ni Chama Wananchi (CUF). Madiwani wote ni Chama cha Wananchi (CUF). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote madogo, la mwisho Pemba Kisiwa kizima. Majimbo yote ya uchaguizi ni Chama cha Wananchi CUF. Watu wa Kongwa lisikieni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishangaa ya Kongwa, subiri ya Pemba yanakuja. Wanasema umeyataka mwenyewe, yanayokupata shauri yako. Sasa turudi kwenye habari kubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, habari ndiyo hiyo. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nalia kwanza na kodi ya wafanyakazi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rage nimekuona. Mpe taarifa Mheshimiwa Khatib.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri jiografia ya Kongwa naielewa na jiografia ya Pemba naielewa. Mwaka jana taarifa ya watu wa sensa inaeleweka. Pemba ili upate udiwani watu 70 wanakuchagua. Kongwa ili upate udiwani watu 10,000 mpaka 15,000. Nilitaka kumpa tu taarifa ndugu yangu, asifananihe Kongwa na Pemba. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kabla hujajibu alichokuwa anasema ni kirahisi tu kwamba, Kongwa idadi ya watu ni wanakaribia 400,000 na Pemba hawafiki laki nne. Endelea Mheshimiwa Khatib! (Makofi)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa ndugu yangu Aden Rage, mwenye asili ya Kisomali, lakini ni Mtanzania halisi. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata China ina watu bilioni kadhaa na Burundi ina watu wasiofika hata milioni 10, lakini Umoja wa Mataifa kiti ni kimoja kwa kimoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Khatib. Endelea, endelea!

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza unitunzie muda wangu na nina uhakika Mheshimiwa Rage amepoteza dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nakisemea hapa ni kuhusu punguzo la asilimia moja kutoka katika kodi ya wafanyakazi. Hili jambo limelalamikiwa na napenda nililalamikie kada ya wafanyakazi Tanzania ndiyo kada pekee ya walipa kodi ambao kwa asilimia mia hawana njia ya kujificha popote. TUCTA wenyewe walipeleka mapendekezo angalau iwe asilimia 11, lakini busara imeonekana ni kupunguzwa asilimia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kweli hili jambo bado naomba Serikali iliangalie kwa makini sana. Wafanyakazi wetu wako katika hali ngumu sana na kwa kusema kweli vishawishi vinaongezeka siku hadi siku. Teknolojia inatuletea ushawishi sasa hivi, mfanyakazi yeyote anataka awe na televisheni flat screen. Sasa mambo haya ya kodi kubwa ambayo anatozwa mfanyakazi inawafanya na wao wafikirie njia nyingine. Mnapowabana huku na wao wanafikiria njia nyingine ambazo siyo za halali katika kujitafutia kipato ili kukidhi mahitaji yao ya lazima. Kwa hiyo, naomba hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nataka nizungumzie suala pia la wazabuni. Jana Mheshimiwa Kidawa alisema sana. Wakati mwingine tunawatafutia Watanzania wenzetu matatizo. Wazabuni wa ndani kwa kweli matatizo yao ni makubwa na vilio vyao ni vikubwa. Ukipitia

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hesabu zote inaonesha jinsi gani Serikali ilivyokuwa haijali katika kuwalipa wazabuni wale wa ndani, jambo ambalo linaleta matatizo makubwa sana na kufikia kama ilivyoelezwa hapa na nasema si ya mfano ni mambo ambayo yako wazi, wanafikia hatua wengine wanachukua mikopo benki kukamilisha zabuni wanazopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake inafikia hatua inakuwa ni tabu sana katika kulipwa jambo ambalo linawaingiza katika matatizo makubwa. Hivi karibuni nilisikia kuna wazabuni wametishia hata kutopeleka vyakula magerezani. Yote hii inatokana na Serikali kutokuangalia. Katika maeneo ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa umuhimu mkubwa ni wazabuni wetu wa ndani kulipwa malipo yao kwa wakati stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizingumzie pia suala ambalo linazungumzwa sana kwamba, kuna utaratibu mpaka sasa unapokwenda madukani na pia umetolewa wito hapa Wabunge msikubali kununua bidhaa bila risiti. Mnapofika dukani mnaponunua ili Serikali ikusanye mapato, lazima tudai risiti. Nakubali nalo hilo, lakini tuangalie udhaifu unaanzia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kwa nini mfanyabiashara anayeingiza mzigo wake wote na ukalipiwa kodi na akatozwa VAT stahiki ambayo badala yake yule mfanyabiashara anageuka kuwa Wakala wa kujirejeshea fedha ambazo amejilipia na inakuwaje awe na uthubutu wa kusema unataka kitu hiki kwa bei hii bila risiti na hiki kwa risiti. Hapa ni dhahiri kwamba udhaifu unaanzia kwa wahusika wanaopitisha mizigo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ingekuwa kodi inakusanywa vilivyo, VAT inatozwa vilivyo, hakuna mfanyabiashara atathubutu kutoa ushauri kwamba bila risiti ni bei hii na risiti ni bei hii. Kwa hiyo, angalieni udhaifu katika vyombo vinavyosimamia kodi katika nchi hii. Kuna udhaifu mkubwa sana katika ukusanyaji wa kodi. Watu wanafikia makubaliano na wafanya biashara kuweza kuikosesha Serikali hii mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Mawaziri ninyi watatu mliopo hapo, mimi binafsi nina imani sana na nyinyi katika moyo wangu, lakini kila ninavyowaangalia machoni mtaweza kweli kukabiliana na hii hali ya kumfunga paka kengele? Udhaifu wa ukusanyaji kodi katika nchi hii ni mgumu sana. Yamewashinda wengi kabla yenu. Mheshimiwa mtaweza?

Mheshimiwa Mwigulu yale makeke yako ulipokuwa pale utayaonesha hapa? Isiwe pale wakati ule tu wa kushughulikia CUF na CHADEMA je, leo utawashughulikia mafisadi papa yaliyojaa katika vyombo hivi? Ili tujenge imani, nimwambie Ndugu yangu Mwigulu, uzalendo si kuvaa skafu kubwa na wala Ushehe si kuvaa jikanzu kubwa. Uzalendo ni matendo yatakayokuthibitisha wewe kama kweli Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kuwawekeneni hapo.

Yale makeke yako Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Malima, onyesheni sasa. Siyo mfanyakazi wa TRA anafanya kosa hapa, adhabu mnamwambia ondoka hapa, kaa hapa. Uhamisho kwa wafanyakazi ni kitu cha kawaida siyo adhabu. Tunaona huu upungufu ambao yako sana. Je, hebu leo nihakikishieni mtaweza? Msipoweza sisi tutaweza. Fuatani ushauri wetu. Ni vizuri sana tunayoyasema kutoa ushauri wa kujenga nchi hii myazingatie. Msiangalie nani katoa ushauri, msiangalie wale ni upinzani, fuatani uzuri wa ushauri wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna udhaifu mkubwa sana katika ukusanyaji kodi. Simamieni vilivyo. Mheshimiwa Saada unalijua doriani. Doriani ukiliangalia baya kwa ngozi yake na harufu yake, lakini tamu ukilila na sisi mnaweza kutuangualia kwa jina tu kwamba ni Wapinzani mkaona sisi ni wabaya, lakini tunawapa vitu ambavyo vitaisaidia kujenga nchi hii. Achaneni na kutuangualia kwa majina kwamba tunaitwa Wapinzani. Wapinzani leo, 2015 tutakaa huko,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

nakuambieni kabisa ishara zote ziko wazi. Ishara zipo anayetaka ni hivyo, asiyetaka shauri yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu mapato. Tunakusanyaje mapato, tunaambiwa tuainishe vyanzo vipya. Bahari yetu tumeitumiaje, Serikali katika kuongezea mapato nchi hii. Leo hebu niambieni kuna viwanda vingapi nchi hii vya kusindika minofu ya samaki inayotokana na bahari? Hivi tuseme hamulioni hili mpaka tuwaambie kwamba kama ile bahari tukiitumia vilivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niambieni mnatoboa madirisha mara dirisha la kilimo, mara dirisha la nini. Hawa wavuvi wana kosa gani? Watoboleeni basi japo tobo dogo waone na wao. Hawa wavuvi wameikosea nini nchi hii? Kila linalokuja mnaangalia hilo, wavuvi wetu ni kwamba wamesahaulika, hakuna msaada. Hebu niambieni mkulima anakopeshwa anasubiri mwaka mmoja kuvuna. Wavuvi mkiwakopesha vifaa vya uvuvi, wanatoka pale wanakwenda kuvulia, wakirudi kaeni katika bandari mkusanye chenu muwaachie chao. Wasaidieni wavuvi wa nchi hii. Hilo nalo hamlioni? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo bahari imekuwa laana kama tumeletewa bahari kila mwaka twende Wapemba na Waunguja na wanaokaa Coast tu kwa kutuua. Ndiyo linalofanyika, hata meli za uhakika za kusafirira hatupati. Bahari kwetu imekuwa ni adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni mambo ya Mwenyezi Mungu. Hapa Mheshimiwa Magufuli alikamata ile meli wamevua wale samaki tuna wa mabilioni. Kwa sababu dunia hii wabaya wamezidi sana kama message Mungu alituletea kwamba kuna mali iangalieni. Leo hebu niambieni ni hatua gani zilichukuliwa kuona kwamba lile ni eneo Mungu ametuonesha kwa ishara kama kuna uchumi mkubwa sana na nyinyi hebu amkeni mlingatie lile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake Wachina wa watu tumewafunga. Hata ile meli tuliyoikamata tumeiacha pia imezama. Hata Serikali hii kudhibiti kale kameli ambacho kingeweza baada ya Mahakama kumaliza mambo yake, ichukuliwe meli ile isaidie kuona kama tunafanyaje katika uvuvi. Pia niliuliza swali hapa siku moja, kwamba, kwa nini tusingeonesha mfano kama hatukubaliani na uvuvi haramu ile meli ikachomwa kama mnavyochoma vifaa vya watu wadogo wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu lilitoka, hatuwezi kuchoma meli. Sasa hamkuchoma angalau dunia ikaona kama tunachukia. Mmeacha imezama ndiyo mmefanya nini? Mmekataa nini na mmefanya nini? Ile meli imezama. Meli yenye mabilioni ya pesa ile imezama. Hivi jamani, Allah Akbar hii nchi hii, haya tu. Yaani unaweza ukasema mpaka ukatamani kulia. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya kwenye matumizi ya Serikali. Hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kusema ununuzi wa magari ya kifahari yale makubwa. Mtazingatia lile suala. Mheshimiwa leo tunachokiona kuanzia Mkurugenzi, Katibu Mkuu, nani wote mashangingi. Angalia hapo, yote ni mashangingi makubwa. Hebu sasa niwape ushauri mmoja, ushauri mna hiari yenu, kuutaka na kutokuutaka, ila mimi nitasema tu nakohoa natema, niliyonayo nayasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja gani Mawaziri wa Serikali, yaani kupewa yale mashangingi. Wao ni Wabunge kama sisi, mkishapewa mkopo wa Bunge kwani haitoshi? Mkishapewa ile nunueni magari ya starehe. Serikali inunue ma-Land Rover yale tena tutamuenzi Mwalimu kununua 109 or 110, yawe sare magari ya Serikali. Waziri ukishakupewa mkopo ule wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ubunge basi nunua gari la fahari unalolitaka. Serikali tuwe na sare magari 110 or 109, ni mazuri tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib muda hauko upande wako. Muda wako umekwisha malizia.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Naam naendelea.

NAIBU SPIKA: Asante sana. Muda wako umekwisha.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, umenizima kwenye mlima.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Khatib. Nikuhakikishie tu maana ulimwelekea Mheshimiwa Mwigulu Nchemba sana. Nikuhakikishie kazi yake, shughuli yake iko pale pale.

Mheshimiwa Cyril Chami! atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko.

WABUNGE FULANI: Amekwenda kwenye Kamati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cyril Chami ametoka amekwenda kwenye Kamati. Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Ismail Aden Rage ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuchangia katika bajeti kuu ya Serikali na Mpango vile vile, lakini ningependa kuanza na suala zima la kodi ya wafanyakazi *Pay As You Earn*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri alitueleza kwamba wamefanya punguzo toka asilimia 13 mpaka asilimia moja. Kiuhalisia kabisa asilimia moja kwa kima cha chini cha mfanyakazi ambao hawawi *taxed*, sasa ambao ni 170,000 ni kwamba wamempa *relief* ya shilingi 1,700 ambao hata mkate huwezi kupata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema na naomba kwa sababu wafanyakazi ndiyo sekta ambayo ina uhakika wa kulipa kodi Tanzania, na-*suggest* twende kwenye *single digit* angalau wafanyakazi wale wa kima cha chini waanze kulipa kuanzia asilimia tisa na pia tuzingatie *relief* kwa wafanyabiashara kwamba wenye *annual income* ya milioni nne ndiyo hawatakatwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukii-*quote* hiyo ni kwamba wenye kipato cha 330,000 kwa mwezi hawakatwi kodi. Tufanye hiyo pia kwa wafanyakazi tuanze kuwakata kodi kuanzia 330,000. Kwa kuanzia asilimia tisa, lakini nilikuwa napendekeza na nikasema *Schedule of Amendment* tukifika kwenye *Financial Bills*. Tuwajali hawa wafanyakazi kuanzia 330,000 mpaka 700,000 wakatwe asilimia tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikapendekeza pia ambayo nitaleta *Schedule of Amendment* kwamba kwa kipato kuanzia 700,000 mpaka 880,000 iwe kwamba wakatwe 35,000 ambazo zinatokana na *deduction* 9% ya kule na asilimia 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikasema kulingana na vile walivyoweka zile *brackets* zao za *tax brackets* kuanzia 880,000 mpaka 1,060,000/= waweze kukatwa asilimia 21 ambayo itaongezeka na 64,000 ambazo zinakuwa *deducted* kwenye *percent* za mwanzo na kipato kinachozidi 1,060,000 waweze kukatwa asilimia 26 kuongeza na 101,000 ya makato ya mwanzo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatoa *relief* sana kwa wafanyakazi. Tuwaone hawa wafanyakazi tu-consider na *inflation rate*. Kama nilivyosema mwanzo kwamba, wafanyakazi ndiyo sekta ambayo inachangia sana yaani wana uhakika wa kukata makato yao siyo kama wafanyabiashara. Tuwazingatie, tuzingatie hizi *tax brackets* zao tuweze kuwapa *relief*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza hapo. Naomba nizungumzie sasa suala zima ya kuweza kupata mapato ya ziada kuweza kufidia hiyo *Amendment* nitakayoleta ya *Tax Brackets* za wafanyakazi. Tunapoteza hela nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vyanzo vingi sana vya mapato ambavyo tukividumisha tutapata hela. Cha kwanza, tuweze kusisitiza kwamba zile Sekta ambazo zinatoa ajira na tumeziainisha kwenye Mipango na kwenye Bajeti yetu, Kilimo, Viwanda, Sanaa na Michezo pia. Tukivikuza hivi tukaweka uwekezaji wa ndani tutapata fedha nyingi sana na tuta-create ajira. Tukisha-create, tukishakuweka ajira, Serikali itapata mapato, lakini pia wananchi watapata kipato ambacho uchumi wetu utakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu mdogo, tumeendelea kuona kwamba Sekta ya Sanaa na Michezo Tanzania haikui, zaidi ya kwamba na ni uhalisia Serikali inaimba siku zote kwamba watawasaidia wasanii kwa maana waimbaji na watu wa filamu kuhakikisha kwamba wanaweka hata Sera ya Hatimiliki yao lakini hamna. Hamna rekodi ambayo ni *vivid* kwamba hii sekta ya filamu inaingiza kiasi gani hamna hiyo kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoa mfano wa nchi kama Nigeria kupitia filamu ya *Nollywood* wanapata hela nyingi sana. Miaka ya nyuma Nigeria ilikuwa inategemea kipato chake cha Taifa kwenye mafuta, lakini leo hii Nigeria pato lake la Taifa kwa asilimia kubwa sana inategemea filamu na mawasiliano. Sasa hivi ninavyoongea Nigeria kwa mujibu wa taarifa za mwaka huu ndiyo Taifa lenye uchumi mkubwa Afrika wakifuatiwa na South Africa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichopelekea vile ni mojawapo ya Sekta ya Filamu ambayo inachangia kiasi kikubwa sana kutoa ajira na kuweza kuchangia pato la Taifa. Vile vile na kilimo kinachangia kwa kiasi kubwa sana Nigeria. Naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iweze kuzingatia vigezo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaangalia sasa kwenye mpango, utekelezaji wa mipango yetu. Kwa mpango wa miaka mitano na ripoti zilizotolewa na Serikali ni kwamba walikuwa wameainisha kwamba watatekeleza miradi 80 ndani ya hiyo miaka mitano, lakini hadi leo tunavyoongea kwa mujibu wa ripoti yao ni kwamba wameteteleza miradi 12, ndiyo inaonekana iko katika hali nzuri ya kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi minne inaridhisha, miradi 51 iko hohe hahe kabisa na miradi 12 haijulikani. Izingatiwe kwamba huu ni mwaka wa nne wakumaliza ule mpango wa miaka mitano. Hatujatekeleza hata mpango mmoja haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi najiuliza na hata niliainisha kwenye ripoti yangu, ukifanya tu hata ile *assessment* ina maana hata huu mpango hauendani na Bajeti halisia, hamna *implementation*, hamna *follow up* yaani hata kama ukifanya *grading* kama ile ambayo tunawafanyia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwalimu, kama zile *grading* tunazotoa kwa wanafunzi, ina maana utekelezaji wa mpango kwa Serikali hii ni ufaulu wa *division zero* na *division four*. Kwa sababu *division one* hamna kabisa mpango ambao umekamilika, *division two* walau ufaulu wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

grade B mipango 12, *division three* wana mipango minne, *division four* wana mipango 51 ambayo hatujui kama itakamilika *within the time given* na *division zero* mipango 12 ambayo wameiweka tu na hii inaleta gharama nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiongea mkiweka mipango msiikamilishe inakuwa na ongezeko la gharama fedha nyingi sana zinapotea kwa sababu hao watu ambao mmewa-assign kufanya hiyo kazi wana-charge gharama zaidi. Kuna *inflation* ina-take charge hapo. Tuwe na mipango, tu-plan kulingana na utekelezaji ambao tunaona tutaufatilia, vinginevyo tutaishia kuwa kwamba tuna-allocate mipango mingi, hatuitekelezi, tunaanza kuweka maulizo mengi je, wanaweka mianya mingi ili ufisadi uweze kupitia hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu kunakuwa hakuna uhalisia, *let's plan*, tu-plan mkishakuwa mmemaliza ku-plan, angalia uhalisia wa bajeti yenu kweli, *within this given time* tutaweza kutekeleza tuliyoya-plan? Kama hamuwezi plan vitu vidogo mvimalize *within the given time*, short of that tutakuwa tunaimba nyimbo za kupoteza fedha za Watanzania. (Makofi)

Kitu kingine ambacho nilitaka niongelee ni kuhusu suala zima la Serikali kucheza na takwimu na kutuambia sisi Watanzania kwamba mambo yanaenda na nikatoa mfano mzuri sana wa kuhusu walivyozungumzia suala zima la utekelezaji wa kupeleka maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma vitabu vya Serikali wanasema kwamba kwa miaka 50 ya uhuru waliweza kuwaunganisha wananchi kati ya 300,000 mpaka 500,000 kwa muda wa miaka 50, lakini kwa mwaka wa 2013/2014 kwa Ripoti za Mpango na za Wizara ya Maji waliweza kuweza kuwafikia wananchi mpaka Aprili 2,390,000. Kwa maana ndani ya miezi sita tu wakaweza kuwaunganishia wananchi 1,890,000 na wakati huohuo Wizara ya Fedha ina-declare kwamba walipeleka 27% tu ya fedha za maendeleo ambazo tulikuwa tumezi-allocate.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema tuwe wahalisia. Kweli kwa miaka 50 kuanzia mwaka 1961 mpaka hiyo miaka 50 imefika mkaunganisha wananchi vijiji 500,000 tu? Ndani ya miezi sita ambayo hamkupata bajeti 100% mlipata 27% tu, mmewaunganishia wananchi 1,890,000? Huu ni uongo na Waheshimiwa Wabunge mnajua uhalisia wa maji, mpaka leo hii huko vijijini hakuna maji kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukemee hii tabia ya Serikali kucheza na figure kutuhadaa sisi tu Wabunge, bali wananchi wa Tanzania ili tu tuone kwamba wanafanya kazi. Hii ukienda kiuhalisia na ninaomba mwisho wa siku tuwe tunaomba tunapata ripoti ambazo *in practical* zimekuwa *evaluated*, twende huko kwenye *field* tuone kweli, wanachokiandika ndio hivyo? Kwa sababu hapa hakuna uhalisia umepata 27% ya bajeti yako. Yet unatuambia ume-connect watu 1,890,000 kitu ambacho kilishindikana kwa miaka 50 iliyopita. Tusiwe waongo, tutoe figure ambazo ni za uhalisia tuweze kujenga nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuisitiza kwamba ni wajibu sasa wa Serikali kuangalia mfano vyanzo vingine kwenye michezo. Tumeona kwamba kwa ripoti ambazo zimetolewa uwanja wa Benjamin Mkapa ulijengwa kwa bilioni 56.4 nafikiri, tukishirikiana na watu wa China, lakini uwanja ule alipokuwa akijibu swali hili hapo mwaka juzi Mheshimiwa Amos Makala alisema kwamba Wizara ya Habari na Utamaduni wamepata takribani trilioni 1.5 mapato, Wizara tu, yet kuna nyingine zimeenda kwenye kodi. Na hapo uzingatie kwamba kuna nyingine zinapotea kwa ubadhififu wa watendaji wasikuwa waaminifu na kutokutumia system ya electronics.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unaweza ukapata tuseme *on average* trilioni tatu tangu ule uwanja ujengwe mwaka 2007 mpaka leo hii, na walitumia bilioni 56.4 tu, je, tukiwa na viwanja hivyo vitano au kumi au 20 hapa Tanzania tutapata mapato mengi sana ambayo yatasaidia kupeleka kwenye sekta nyingine.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kwa hiyo, naomba sana tuwe *creative*, tuangalie vyanzo ambazo vitatuletea mapato tuweze kuvitumia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Matiko.

Mheshimiwa Ismail Aden Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina na Mheshimiwa Cyril Chami atafuata.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuchukua fursa hii kukupongeza Mheshimiwa Naibu Spika, hasa kwa umakini na umahiri mkubwa unavyoliendesha Bunge lako hili.

Mheshimiwa Naibu Spika,....

NAIBU SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa Rage, kuna Taarifa ya Mheshimiwa Amos Makala, sikumuona.

Mheshimiwa Amos Makala, Naibu Waziri wa Maji.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuweka *record* vizuri tu juu ya mtani wangu aliyemaliza kuongea kwamba katika miaka 50 tumewapatia maji Watanzania wapatao 300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba Serikali ilikuwa inapeleka huduma kwa wananchi kwa kila mwaka kati ya watu 300,000 mpaka 500,000. Sio katika miaka 50 tumewapa maji watu 300,000. Kwa hiyo, nilitaka kuweka *record* sawa, lakini pia hakuna ubishi kwamba baada ya BRN kuna miradi 228 imekamilika na watu wanatumia maji na idadi ya watu wanaopata hayo maji ni milioni 2.3 kwa hiyo, hilo halina ubishi. Katika vijiji hivyo na ningemwomba Mheshimiwa Esther Matiko tufanye nae ziara twende katika vijiji hivyo, aone watu wakichota maji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ismail Aden Rage endelea tu.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nakubaliana na Mheshimiwa Amos Makala namuunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha ni kukusanya trilioni 19.649 kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 11.974 ni mapato ya ndani. Wasiwasi wangu uliopo ni kuwa iwapo bajeti hiyo iliyomalizika imeshindwa kufikia malengo ambayo tulikuwa tumeyapanga ya kukusanya trilioni 18.248 tutawezaje kuzitumia hizi?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, nitaomba Waziri atakapokuja atuhakikishie ili aweze kututoa wasiwasi. Mimi ningeishauri Serikali yangu iweke malengo yenye uhakika na kuhakikisha kuwa tunatumia matumizi vizuri kwa vile ndio sera ya Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuongelea pia suala la madeni ya Taifa. Hakuna nchi yoyote duniani iliyoendelea bila kuwa na madeni na lazima tujue historia ya madeni yetu kwa nini yamefikia hapa tulipofika. Tulipata vita ya Idd Amin, tulipata ukame, mabadiliko ya uchumi wa dunia mwaka 2008 na 2009 na hata Marekani kwenyewe, ukisoma kwenye mitandao na ninaona hapa kuna vijana wengi wanatumia *Ipad*, wajaribu kuangalia kwenye kitu kinaitwa *historical data on the federal debt* wataona baada ya Vita ya Pili ya Dunia deni la Marekani lilikuwa 112% ya GDP ambayo ni kubwa sana, kwa sasa hivi imeshuka mpaka 71.8%, *the rest of the world* ni 61.3%, sisi Tanzania tunaogelea kwenye 42 kwa hiyo, *we are doing very well*. Na katika hali kama hii Wizara yetu ya Fedha na hasa wale wataalamu tunawajibika kuwapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwanafalsafa mmoja anasema mfanyabiashara yoyote mwenye akili anatumia fedha za benki au za kukopa kufanya biashara. Anayetumia fedha zake wanasema ni mtu mjinga au mpumbavu. Kwa hiyo, tusingikilize haya maneno ya kwamba tuache kukopa na nini na wakati mwingine nashangazwa na baadhi ya wasomi wetu na hata wanasiasa siku hizi na wenyewe wameanza huo mtindo wa kutaka kuongea kufananisha uchumi wa Tanzania na Kenya. Ukitaka kupima pima kwa tarakimu, sio kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekaa na mdogo wangu Mheshimiwa Khalfan Aeshi hapa, nikitaka kujua homa yake imepanda namna gani sio kwa kumshika kichwa. *I have to give him a thermometer*, ili i-read nielewe homa yake ipo wapi. Kwa hiyo, tuheshimu sana hawa wenzetu hasa watu wa Serikali na hasa hii Wizara ambayo kwa kweli inafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano, sisi tutamaliza Bunge la Bajeti mwezi huu, lakini Wizara ya Fedha kuanzia mwezi wa kumi mwaka huu wanaanza kutayarisha bajeti yetu ya mwaka wa 2015/2016. Sasa sisi Wabunge tunapokuja hapa kwenye Kamati zetu tunajadili ndani ya wiki moja, hatuna *expertise* wa kutosha kama wenzetu walivyo, tunadhani tunakuwa juu yao, hatuwatendei haki hata kidogo. Ni vizuri tukaheshimu ushauri wao ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba wajibu wa Wabunge umeelezwa, kazi za Kamati zetu za Bunge zimeelezwa, inawezekana kuna wakati tuna-over do, kazi yetu sisi ni kushauri, kuelekeza Serikali, lakini wakati mwingine tunafika tunawaita kwenye Kamati zetu hizi viongozi wetu wa Kiserikali na wafanyabiashara binafsi na kuanza kuwadhalilisha mbele ya hawa watu binafsi, *I don't think that is a good trend*. Matokeo yake ni kulidhalilisha Bunge na kuonesha kama kuna kamwanya hivi ka watu kutaka kutumika katika kuleta bajeti mbadala katika Bunge letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye matatizo ambayo yanagusa sana katika Mkoa wangu wa Tabora, kama bajeti inakuwa inalegalega.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule tuna barabara zetu za lami, barabara za lami hizi zimetiwa saina mwaka 2010, tatizo moja ambalo Serikali yangu napenda kuishauri kosa tunalofanya tunaingia mikataba kabla ya kupanga bajeti, sasa hii inatupa taabu. Kwa hiyo, ukishaingia mkataba *that is already a commitment*. Kwa hiyo, unapochelewa kutokuanza kazi na yule ukashindwa kumpa *mobilization fund*, yule anachelewesha mradi na akianza ule mradi kwenye barabara mikataba yao ni mibaya sana kwa Serikali yetu hii changa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu unapochelewesha kumlipa fedha na kama alivyoongea leo Naibu Waziri wa Ujenzi, barabara za Mkoa wa Tabora zote zinategemea Hazina. Sisi hatuna baba mwingine kule zaidi ya Hazina, bahati nzuri mikoa mingine ina wafadhili kutoka nje, lakini mkoa wetu sisi tunategemea Hazina. Kwa hiyo, pesa inapochelewa kuja tunakuwa tunalipa *interest rate* ambayo ni kubwa kuliko ambavyo tunatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine ambalo ni kubwa sana katika Manispaa yangu ya Tabora. Bajeti iliyopita fedha ya maendeleo katika mkoa mpaka ninavyoongea jana ni 60% tu imekwenda huko. Nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie ili angalao kati ya hii 40% iliyobakia hata kidogo iweze kupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea juu ya Manispaa yangu ya Tabora hiyo ndio kwa kweli inaadhirika sana. Kwanza niishukuru Serikali kwenye fedha za *World Bank* mmeweza kututengea *almost 28 billion shillings* kwa ajili ya kubadilisha ule mji wetu na mwaka huu nashukuru kabisa kwamba mmetutengea bilioni 5.6 kwa ajili ya kuanza kutengeneza barabara 13 kwa kiwango cha lami katika mji wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Manispaa ya Tabora mpaka jana imepokea fedha ya maendeleo 39% tu. Mheshimiwa Waziri hebu naomba na hili nalo kwa sababu wewe ni mama, najua una huruma sana na hasa ukizingatia mimi ni kaka yako, ndugu yako hasa. Kwa hiyo, imebakia kama 61% na mimi nina imani siombi zote, chochote utakachopata kitasaidia kuleta mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mamlaka inayofanya kazi vizuri pale Tabora ni Mamlaka ya TUWASA. Na hii nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu mlitupatia fedha kutoka kwenye Serikali ya Uswis dola milioni 6.5 zimeweza kusaidia kupata maji mengi sana sasa hivi pale mjini. Lakini tatizo ambalo TUWASA wanalo ni kudai fedha mashirika ya Kiserikali, kama vile Jeshi la Wananchi, Polisi na JKT. Haya madeni yana takribani kama shilingi bilioni moja, tukipata hizi tutaweza kuacha kukusumbua Profesa Maghembe na ndugu yangu Mheshimiwa Makala, tutaweza kuongeza fedha katika kuleta maendeleo katika Kata nyingine nje ya Tabora Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa si muungwana hata kidogo kama sitatoa pongezi na furaha kubwa kwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mkandarasi ameshafika pale Tabora, vijiji vyangu vyote ameshapima na nimeshapewa ramani na wameshaanza kufanya kazi. Na nilipofanya mkutano nao wale wakandarasi, wamenihakikishia kabla ya tarehe 30 mwezi wa sita mwakani vijiji vyote nje ya Tabora, bahati mbaya ninapoongea juu ya Tabora watu wengi wanaijua Manispaa, lakini mimi nina kata 15 za vijiji. Kwa hiyo, vijiji vyangu vyote vile viko kwenye programu ya kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri, nilimsumbua sana kumuomba guzo za umeme...

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Rage, muda hauko upande wako.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuishukuru Wizara hii kwa kazi nzuri.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, lakini nusu dakika tu Mheshimiwa Rage, kule simba vurugu tupu, wewe ndio Rais, namna gani bwana? Mbona hukugusa hata kidogo?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujua wewe ni mwanachama wangu wa simba, nilitaka kutoa tu taarifa kwamba sijaivunja ile Kamati ya Uchaguzi na leo saa 7.00 mchana nitatoa taarifa yangu nzito kwa nchi nzima. Ahsante sana. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wambura bado?

NAIBU SPIKA: Huyu ni Rais wa Simba, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, tunakushukuru.

Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, atafuatiwa na Mheshimiwa Cyril Chami na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Bajeti Kuu ya Serikali. Tulishazungumzia Bajeti za Kisekta, nilitegemea kwamba masuala yanayohusu majimbo yetu tuliyazungumza sana kwenye Bajeti za Kisekta, huu ni wakati wa kuwashauri wale vijana watatu namna ya kusimamia *Treasury*. *Treasury* ni moyo wa uchumi wetu, *Treasury* kwenu kuwa pale sio *business as usual*, ni uchumi wa nchi.

Kwa hiyo, mimi nimejiandaa kuwashauri hawa vijana, lakini kabla sijafanya hivyo naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, *is hymnogiral speech* ambayo inaleta matumaini. Ametoa mapendekezo ya namna ya kuongeza mapato na kupunguza matumizi, lakini ninakutahadharisha kwamba utapata upinzani mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *system* yetu kuna watu ambao hawataki kuingiliwa kwenye ulaji wao, lakini na wewe naomba uwe ngangari kama alivyo Mheshimiwa Sospeter Muhongo ambaye anapigwa vita sana kwenye mambo ya gesi, lakini yeye anakuwa ngangari na hao vijana wako ninawaamini. Kwa hiyo, kusimamia *Treasury* sio lelemama, nawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini umenifurahisha pia kuzungumzia masuala ambayo nimekuwa nikiyazungumza kwa uchungu kupunguza kodi kwa mishahara ya wafanyakazi, pamoja na kuongeza ile *pension minimum* ya 50,000/=. Naomba sana *that is very serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hayo naomba nije kuwashauri sasa. Katika uchumi wowote wa maana kuna mambo matatu ya kuzingatia au malengo matatu.

Moja, niyataje kwa kiingereza halafu nitayafafanua kwa Kiswahili. Moja ni *efficiency*, lazima kazi zote za kiuchumi zifanywe kwa ufanisi wa hali ya juu, ndio maana ya *efficiency*. Hata kama una rasilimali ndogo uzitumie vizuri ili matokeo yawe makubwa, ndio maana ya *efficiency*. *Maximization of benefits using minimum resources*, ndio maana ya *efficiency*. Je, sisi katika uchumi wetu *are we efficient?* Tunafanya kazi kwa ufanisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana kwa sababu matumizi yetu bado ni makubwa kuliko mapato. *We are not efficient*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *number two, fairness*. *Fairness* kiswahili chake ni labda usawa au haki, kwamba, hizi *minimum resources* ambazo tunazo tuzigawe kwa usawa bila upendeleo, yaani *resources* zigawiwe kwa Wilaya na kwa Mikoa bila upendeleo, lakini pia wananchi ili *resources* hizi ziwe *distributed equitably* kwa wananchi, wananchi tunasema uchumi unaendelea kwa 7%, lakini unawafikia wananchi? Hiyo ndio maana ya *fairness, equitable*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

distribution of resources kwenye Wilaya, kwenye Mikoa na kwa wananchi wenyewe, je, *are we...*, tuna *fairness*?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kuna tatizo bado naona kwamba rasilimali zetu tunagawiwa kwa upendeleo, lakini naamini kwamba ndiyo maana napendekeza kwamba tuwe na Kamati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na *Paymaster General* tu-design mechanism ya kuhakikisha kwamba hizi *little resources* ambazo tunazo ziwe *equitably distributed* kwenye Mikoa, kwenye Wilaya hata Ngara ambako sisi tupo pembezoni tupate fedha za kutosha kama wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu *sustainability* yaani uchumi endelevu. Uchumi wetu ni endelevu? Hauwezi kuwa endelevu kama tunaendelea kuwategemea wahisani, lakini pia zile fedha tunazozipata kutoka kwa wahisani tunazielekeza kwenye yale maeneo ambayo yanachochea uchumi? Lazima tuzingatie jambo hilo. Kwa hiyo *sustainability* ya uchumi, sisi tuna tatizo kuna mtaalam alikuwa wa uchumi Rostow alikuwa anazungumzia *five stages of development*, kuna *take off* ya mwisho, sisi tuna *consume there is consumery before take off*. Tunapenda sana kutumia sana ingawa bado sisi ni maskini. Sasa katika hali hiyo na wakati hatuwekezi tunatumia zaidi hatuwezi kuwa na *sustainability* ya uchumi. Sasa hayo ndiyo nilitaka hawa vijana wangu wayazingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nimesema kuunda Kamati ya kuhakikisha kwamba fedha za maendeleo zinakuwa *equitably distributed*. Huyu mtu anaitwa *Paymaster General* mmemzungumza sana kwenye bajeti yenu, anatoa mafungu kwa *Accounting Officers* (Makatibu Wakuu), lakini hajui namna haya mafungu aliyoyotoa yanavyotumika, mnamuachia mtu anaitwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, yule Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mimi namuita daktari wa upasuaji wa maiti yule *Controller Auditor General* ni daktari wa kupasua maiti kwa sababu yeye anafanya kazi ya *postmortem*, fedha zimeshaibiwa eti anatafuta mwiz.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu muhimu sana ni kufuatilia matumizi. Huyu Bwana Uttoh ndiyo maana ameota mvi nyingi sana yeye kazi yake is a *pathologist* yaani ni *toothless bull dog* kwa sababu hata mapendekezo anayopendekeza hayatekelezwi na Serikali *he is not even a deterrent, deterrent* maana yake ni tishio, wale wezi sugu wanajua kwamba hata akipendekeza mapendekezo yake mengine hayatekelezwa kwa hiyo msimuachie huyu mtu anayefanya *postmortem*, huyu *pathologist* anayeitwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mfuatilie matumizi haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kupanua wigo wa kulipa kodi. Hapa napo napenda nimpongeze Waziri wa Mipango na Uratibu kwamba bado anaona umuhimu wa MKURABITA. Hii sekta isiyo rasmi is a *sleeping giant in terms of taxation*, lakini *we have not taped it*, hatujazingatia ushauri mzuri wa mtu anaitwa Hernando de Soto. Hernando de Soto ni mchumi wa Peru ambaye ametusaidia kuanzisha hi MKURABITA. MKURABITA tukipima ardhi na mashamba yote na hawa wananchi wakapata *legal property and rights* wakaifanya ardhi yao sasa iwe *collateral* na kukopa badala ya kuwa a *dead capital* tutasaidia sana katika kuongeza *taxation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuongeza ajira. Wenzangu wamezungumzia kilimo ni muhimu sana, kama tunaboresha kilimo na umwagiliaji vijana wengi watakaa kule hawatakuja mjini.

Lakini pia viwanda vya nguo vilikufa kwa sababu ya sera mbaya sana za mtu anaitwa Marehemu Reagan na Magreth Thatcher ndiyo tuliwa viwanda vyetu vya nguo. Viwanda vyetu vya nguo tukivirudisha ni *labour intensive*, vitaajiri watu wengi sana. Kwa hiyo viwanda pamoja na sekta isiyo rasmi, pamoja na kilimo itasaidia sana kuongeza ajira.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwashauri kwamba kama wenzangu walivyokwisha sema hizi takwimu mnazozitoa mimi siziamini hata hii GDP *per Capital* kwa sababu *Bureau of Statistics* inahitaji kuimarishwa sana kiutaalamu pamoja na kifedha. Mimi mwenyewe nimehusika kuifanya *Bureau of Statistics* kuwa wakala, mimi ndiyo nimeleta suala la *Executive Agencies* mwaka 1992 kutoka Uingereza na furahi kwamba kuna *Executive Agency* lakini hii *Bureau of Statistics* inafanya *house hold survey* lakini muiongezee *capacity* iwe na uwezo kuweza kuleta takwimu ambazo ni sahihi, ambazo tunaweza kuzitumia katika mambo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Tunazungumzia kuboresha mazingira ya sekta binafsi, lakini tuna tatizo bado la kigugumizi cha kufanya maamuzi (*procrastination*). Nitoe mfano wengine wameshatoa mifano mingine kuna mfano mmoja ile *East African Business Council* waliomba *plot* pale Arusha for the last seven years ili *East African Business Council* wajenge kituo pale na Ujerumani walikuwa tayari kuwapa fedha, wamekosa hicho kibali, wamekosa hiyo *plot* wamekwenda Rwanda wamepewa *plot* sasa hii inatokana na *procrastination*, tunakuwa na kigugumizi kwenye kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kifupi nawashauri hawa vijana na wewe mama ulipoteuliwa mimi kama *senior citizen* nilijiuliza huyu mama anaweza kuvaa viatu vya Waziri Jamal, anaweza kuvaa viatu vya Msuya? Wale Mawaziri wawili ambao mimi niliwaona *very effective* au anaweza kuwa kama Gordon Brown wa Uingereza aliyekuwa *one of the best Chancellor of the Exchequer*?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na *confidence* yake, una *confidence* kubwa sana, lakini nikushauri mambo mawili ya kufanya licha ya *confidence* yako uwe msikuvu, *a good leader is a good listener* hata kama mawazo yanatoka kwenye upinzani kama ni mazuri yachukue. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Malizia Mheshimiwa Ntukamazina.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Jambo lingine ambalo napenda nikushauri *a good leader* ni mtu anayeendelea kujisomea. Muendeleo kujisomea ninyi vijana ndiyo mtakuwa wazuri wa kuwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunakushukuru sana maneno ya mtu mzima hayo.

Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Haroub ajiandae.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Napenda kuanza kuchangia hotuba hii kwa kusema kwanza naiunga mkono na namshukru sana msemaji aliyetangulia kwa sababu ameshauri sana, mimi nitashauri lakini vilevile nitatoa mifano hai ya kuonyesha kwa nini nashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji aliyepita ameongea kuhusu *equitable distribution* yaani mgawanyo wa mapato ambao unaendana na usawa, lakini nataka niseme kwamba *equitable distribution* inakuwa nzuri sana pale ambapo hata yule anayechangia naye

Nakala ya Mtandao (Online Document)

unamuangalia. Haiwezekani mtu akachangia halafu ukamnyima kabisa ukategemea kwamba kesho achangie tena na mwaka kesho achangie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mlima Kilimanjaro ni mojawapo ya hifadhi ambayo inachangia sana katika mapato ya utalii katika nchi ya Tanzania, wengine watakuambia kwamba inachangia zaidi ya nusu, wengine watakuambia inachangia 40%; lakini sijasikia mtu yoyote akasema kwamba Mlima Kilimanjaro unachangia chini ya 38%. Kama kuna mbuga za wanyama 13 Tanzania, Kilimanjaro yenyewe KINAPA inachangia 38%, bado zile reserves nyingine bado hatujahesabu, lazima tukiri kwamba *Kilimanjaro National Park* inatoa mchango mkubwa kwa maana ya mapato ya utalii katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna sheria sasa kwamba wale wananchi wote ambao wanazunguka Hifadhi za Tanzania wanapewa sehemu ya mapato yanayotokana na hifadhi zile, karibu hifadhi zote Tanzania watu wanapata mapato isipokuwa Hifadhi moja tu inaitwa *Kilimanjaro National Park*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru, Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Siha, Wilaya ya Hai, Wilaya ya Moshi na Wilaya ya Rombo jumla ya Wilaya sita ndio wanaosimama kidete kusimamia Mlima Kilimanjaro, ndio ambao wanaenda kuzima moto, moto ukiwaka, ndio ambao wamekatazwa kukata mbao, ndio ambao wamekatazwa kuokota hata kuni, lakini wananchi hawa hawapati hata senti tano kutokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimekuwa Mbunge mwaka 2005 tumeungana Wabunge wote wa Kilimanjaro na Arusha bila kujali itikadi zetu kusema kwamba Halmashauri hizi na Wilaya hizi zinastahili kupata mgao majibu tunayopewa hapa ni kwamba Kilimanjaro ni Hifadhi ya Taifa, ni hifadhi ya dunia siyo Hifadhi ya Kilimanjaro wala Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa mimi ni Mbunge ninayetokana na Chama cha Mapinduzi na mimi nina mapenzi makubwa kwa Chama cha Mapinduzi, lakini napenda niseme hisia mbili hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hisia ya kwanza ya wananchi wa Kilimanjaro na Arusha ambayo ndio walenzi wa Mlima Kilimanjaro ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii na siyo tu Waziri aliyepo au viongozi waliopo sasa hivi tangu enzi na enzi, tangu tumeanza mchakato wa kuomba kwamba Wilaya hizi zisaidiwe, ziangaliwe Wizara hii imeamua kwa makusudi kuwanyima wananchi mapato yanayotokana na mlima huu, hiyo ndio hisia ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hisia ya pili ni kwamba wananchi hawa wanaamini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu akiamua leo wananchi hawa watapata mapato ya mlima huu kama vile ambavyo wengine katika maeneo ya migodi wanapata mapato hayo. Nataka niliache hili kwa sababu kama tunapenda kuendelea kupata mapato kutokana na mlima huu ni vizuri tukawaangalia wale ambao ni walenzi na nimeshawasema hapa ni wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naomba niungane na aliyepita kushauri ili kuboresha uchumi wetu na kwa maana hiyo mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri hapa umuhimu wa Tanzania kuanzisha kitu kinaitwa *Economic Intelligence Unit* (Kitengo cha Utafiti wa Mambo ya Kiintelijensia ya Uchumi). Haiwezekani nchi hii ikawa na utajiri wote tulionao wa madini, wa nishati, wa maliasili mbalimbali, wa ardhi kubwa na tukafanikiwa kuufanya uchumi ukasaidia nchi yetu mapato yakapatikana bila kuwa na kitengo cha Intelijensia ya uchumi. Nchi zote ambazo tunazisifu leo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zimefanikiwa kwa sababu zimekuwa na kitengo cha namna hiyo. Sasa sasa hivi tunaongelea kuhusu gesi, tunaongelea kuhusu madini mbalimbali, tunaongelea hata kuhusu utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliotutangulia na ambao kila wakati tunasema kwamba wamefika mbele ni kwa sababu wamekuwa na kitengo imara kabisa ambacho kinaangalia nani anaingia na nani anatoka katika maeneo haya ambayo yanazalisha katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo napenda nishauri ni suala la Benki za Maendeleo ya Wananchi. Nilisema kidogo wakati uliopita, leo napenda niongee jinsi ambavyo benki hizi zinasaidia kuongeza bajeti, kuongeza mapato ya Serikali na kwa maana hiyo kufanya uchumi wetu uweze kuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote ambazo zimeendelea, nenda Amerika leo hii benki nyingi zaidi ni zile za wananchi kuliko benki za biashara. Hata Marekani kuna benki za wananchi na zinasaidia mtu hata yule mdogo kabisa aweze kushiriki katika suala la uchumi.

Sasa hivi tunaongelea kuhusu kurasimisha uchumi mambo ya MKURABITA yatafanikiwa vizuri zaidi kama tutawafanya Watanzania wa kawaida waliopo vijijini na waliopo mijini na ambao wanafanya shughuli ambazo siyo rasmi waweze kushiriki uchumi rasmi na namna mojawapo ni pamoja na kuwasaidia waweze kushiriki katika mambo ya biashara ya fedha yaani mablenki yenyewe. Haiwezekani mablenki ya Tanzania zaidi ya 52 yakawa karibu yote ni ya kigeni halafu tukakaa hapa, tukaamini kwamba eti kuna siku Watanzania watakaa wamiliki uchumi wao, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mablenki haya yanakuja kufanya biashara Tanzania na yanapeleka fedha kwa wale ambao wana hisa ambao ni wageni kwa sababu hapa kuna faida inayopatikana.

Sasa ninachosikitika ni kwamba Benki Kuu kwa kweli imeweka utaratibu ambao unakuwa ni mgumu sana kwa wananchi wa kawaida kuweza kuanzisha benki za wananchi na nitoe mfano Moshi Vijiji. Sisi Moshi Vijijini tulitaka kuanza Benki ya Maendeleo. Tumekwenda Benki Kuu tukaambiwa kwamba tafuteni milioni 250 mtaanza Benki ya Wananchi, tukatafuta, tukapata tukaambiwa kwamba aaah Benki Kuu imeongeza mpaka bilioni moja. Tukaenda kutafuta bilioni moja, tukapata bilioni moja tukaambiwa kwamba hapana imeongezwa mpaka bilioni mbili, tumekwenda kwa wananchi, wananchi hawakutuamini tena, wananchi hawajaongeza ile fedha, wamesema haiwezekani mnakuja kila wakati mnaongeza na benki haianzishwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barua ya tarehe 2/6 kutoka kwa Gavana kuja kwetu ambaye nimshukuru huyu mama ametusaidia sana pamoja na kwamba hatuandikii barua lakini ametusaidia sana, inasema kwamba msingeweza kuanzisha benki bila kuwa na bilioni mbili na nusu.

Kwa hiyo kile kiwango ambacho tuliambiwa tutafute bilioni mbili hata kama tungepata tungeambiwa kwamba hamja-qualify kwa sababu tungeambiwa ni bilioni mbili na nusu tena. Mimi nadhani kuna masharti ambayo yanawekwa ya kuwazuia Watanzania wa kawaida kuanzisha benki hizi, lakini niseme hivi zipo benki za wananchi ambazo zina mtaji wa milioni 400, shilingi milioni 555 zinafanya vizuri, hazijaingia hasara yoyote na walioweka hisa pale wanafurahia kabisa kupata huduma katika benki hizi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa hivi benki nyingine ikitaka kuanzishwa lazima muwe na bilioni 2.5 jambo hilo halieleweki napenda nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ndugu yangu Mheshimiwa Malima aliyenijibu juzi akasema kwamba haiwezekani, lakini mimi nafikiri inawezekana kabisa. Mliangalie kwa undani, Benki Kuu ipo chini ya Wizara ya Fedha tuone uwezekano wa kuwasaidia Watanzania waweze kuendesha Benki za Maendeleo kwa sababu ndiyo njia nzuri ya kuongeza mapato ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne Tume ya Mipango. Mimi napenda niseme wazi nafahamu baadhi ya wataalamu wa Tume ya Mipango ni wataalamu waliobobea kabisa wakiongozwa na mwalimu wangu Profesa Dkt. Mpango na inafanya kazi nzuri ya ajabu. Lakini kwa kweli kabisa Tume ya Mipango haijapata meno ya kutosha kufanya kazi yake. Hizi nchi ambazo tunazisifu leo kwamba zina uchumi ambao umebobea ni kwamba *The Minister for Economy* ndio mwenye *power* kubwa *is one of the most senior Ministers* kwa sababu Tume yake ikishapanga mipango hakuna mtu anakuja tena kubadilisha mipango ile.

Sasa hapa kwetu tuna Tume ya Mipango ambayo kwa kweli napenda niite ni Tume ya Ushauri zaidi kuliko Tume ya Mipango kwa sababu ikipanga lazima tena mtu mwingine akaamue kama inawezekana ama haiwezekani, kwa hiyo yale mawazo yao yanakuwa kama ni ushauri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Tume ya Mipango tumeambiwa hapa kwenye Bunge hili Tukufu kwamba kuanzia mwaka jana tungekuwa tunatumia trilioni 8.5 kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo kila mwaka. Mimi na wewe ni mashuhuda kwamba hizo fedha hatujazipata, tulisema tu hapa Bungeni kujifurahisha, lakini halikufanikiwa kwa sababu kile ambacho kimeshauriwa na Tume ya Mipango hakikutekelwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho napenda niongee kuhusu pensheni ya wazee. Mimi nimepewa taarifa na wazee kutoka Moshi na Kilimanjaro kwa ujumla wanalilia pensheni ya wazee. Kwanza ni ndogo sana shilingi 50,000/= kwa wale ambao walikuwa wamechangia, lakini vilevile kuna wale wengine ambao hawakuwa kwenye mashirika haya nao wanauliza kwamba je, Serikali haina mpango wa kuwaangalia baada ya kustaafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuwa pensheni ya wazee inapokuwa ndogo ndivyo unavyokatisha watu tamaa kulipa kodi wakijua kwamba hata ukilipa kodi ukistaafu hakuna ambacho utakipata tena. Kwa hiyo, mimi nataka niseme kwamba pamoja na kilio cha wazee nishauri kwamba ukiongeza ile pensheni ya wazee ikawa nzuri kidogo ni kwamba sisi wazee wa kesho unatutia moyo wa kuendelea kulipa kodi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chami nakushukuru sana muda haupo upande wako malizia.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, na nimshukuru Waziri wa Fedha ametangaza kwamba pensheni inaongezeka ila wazee walikuwa wanaomba kujua ni kiasi gani kimeweza kuongezeka.

Baada ya maneno hayo mimi napenda kuungana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa umahiri na Naibu Mawaziri wake nawashukuru sana kwa kazi yao, napenda kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mawazo haya niliyoyatoa wazingatie, tumeyatoa kwa nia nzuri ya kusaidia na siyo kubomoa ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chami. Mheshimiwa Rajab.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa ndogo kwa niaba ya Halmashauri ambazo zinazunguka hifadhi zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na Mheshimiwa ambaye kaka alivyosema kwamba ni Kilimanjaro tu ndiyo ambayo haifaidiki na ile Hifadhi. Ukweli ni kwamba hakuna Halmashauri ambayo inafaidika moja kwa moja na hizi Hifadhi. Mfano Halmashauri ya Babati ambayo ipo pale Tarangire hawapati hata senti tano ambayo inatokana na mapato ambayo yako pale wanayapata Tarangire, lakini wanachokifanya ni ujanja wa kusema kwamba wanaushirikiano wa ujirani mwema kitu ambacho kwa kweli hakileti tija na faida na ukiangalia gharama ambazo Halmashauri husika zinakuwa zinaingia kutokana na hifadhi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niweke sawa kwamba Hifadhi zote hazitoi mgao kwa Halmashauri ambazo zinazizunguka. Naomba hili Serikali kama ni kujibu au kulichukua basi walichukulie kwa nchi nzima.

NAIBU SPIKA: Mimi nikushukuru sana Mheshimiwa ni ukweli kabisa sera ya kutoa fedha za TANAPA kwa Halmashauri haipo, kilichopo ni sera ya ujirani mwema kutegemea na miradi iliyopo na TANAPA imesaidia sana.

Kwa hiyo wananchi wa Kilimanjaro wasione kama vile wamebaguliwa wao ni kwa nchi nzima na siyo wao peke yao.

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza ningependa nimshukuru ndugu yangu Mbarouk kwa kuliona hilo kwa sababu jambo hili hata Bagamoyo tunalalamikia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kaka yangu Mwigulu na ndugu yangu Bwana Malima kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya lakini pamoja na hilo pia nitumie nafasi hii kumpa pole rafiki yangu, Mwenyekiti wangu wa Kata ya Lugoba Bwana Jumanne Chiboko Mataluma ambaye anaogua kwa kweli hali yake tuendeleo kumuomba Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nigusie maeneo machache ambayo ninafikiri ninaweza nikatumia nafasi hii kutoa ushauri pia kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika dunia tunayoishi leo ambayo moja ya tatizo kubwa tunalopambana nalo ni urasimu, ukiritimba uliokithiri hasa katika utendaji wa kazi za Serikali, kurudisha shughuli za malipo za Halmashauri zote kwa mtu mmoja anaitwa *Paymaster General* hili jambo si sawa. *(Makofi)*

Mimi nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika eneo hili nilikuwa sijaelewa, nilikuwa nafikiri ingekuwa ni vizuri wakati Mheshimiwa Waziri anajaribu kufunga mjadala huu angetueleza nini hasa nia ya kurudisha malipo haya yafanywe na mtu mmoja? Maana katika dunia ya leo tunazungumza *decentralization of economy* hawa wenzetu wanaturudisha katika *centralization of payment* jambo ambalo halijaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nataka nizungumze masuala ya SACCOS na *microfinances*. Ninavyoamini mimi vyombo hivi vimeanzishwa nia kubwa ni kuendeleo kusaidia wananchi wanyonge ambao wanahitaji kukopeshwa kitu kidogo ili waweze kujikomboa katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mahitaji yao ya kila siku na katika shida zao. Lakini mfumo uliopo ambao unamlazimisha huyu mwananchi anayetaka kuanzisha SACCOS aende kukopa benki, ambapo kule kuna riba kubwa na anapokuja kufanya malipo yale naye kwa kutambua kwamba ana deni la kulipa inamlazimu yeye naye anaongeze kidogo ili mambo yakae vizuri kule benki na katika mfuko wake, imejikuta sasa nia nzuri ya kusaidia wanyonge hawa haitekelezi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo imeendea baadhi ya SACCOS zimekufa sasa na benki bado zinaendelea kupata shida sana katika ku-recover fedha zao. Sasa mimi kwangu natambua kwamba ipo juhudi zinafanyika za upande Serikali kuweka sawa sheria hii, lakini bado napenda nisisitize kwamba ni muhimu sana wanapoleta sheria hii katika yale mafungu ya watu wanaotakiwa kusamehewa kodi basi *microfinances* na SACCOS nazo ziangaliwe ili ziweze kuwa na mzigo wa kusaidia wananchi baada ya kugeuka kuwa nao wanatafuta fedha kwa ajili ya kulipa madeni kule benki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nilitaka nizungumzie jambo la PPP. Niipongeze Serikali kwa hatua zinazoendelea za kuhakikisha kwamba wanatuletea Muswada huu ili tuweze kuona jinsi gani tunaweza kuweka mambo yetu vizuri. Hii ndiyo tiba ya miradi yote ambayo inakwama maana leo hii Serikali inahangaika kwamba tunataka fedha, fedha mara hazitoshi, zimeletwa fedha, mara fedha hizo zinaonekana kwamba kuna maeneo mengine muhimu zaidi yapelekwe. Mimi nafikiri sasa umefika muda muafaka wa kuletwa kwa sheria hii mapema haraka iwezekanavyo ili mambo yakae vizuri, ili wananchi na *private sector in particular* ziweze kushiriki katika mchakato huu wa kuleta maendeleo katika nchi hii. Ninaamini kwamba patakapofanikiwa kuletwa vitu hivi basi hata zile barabara za kutoka Dar es Salaam kuja Chalinze zitakaa vizuri, hakutakuwa na shida tena kwa sababu *private sector* itakuwa imekuwa *engaged* na mambo mazuri yatakuwa yamefanyika, siyo tu barabara za Chalinze lakini pia hata Bandari ya Bagamoyo nayo itakamilika katika muda muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia jambo hili la ushirikishwaji nakuja katika jambo la msamaha wa kodi. Ni kweli tunahitaji kupunguzwa kwa misamaha ya kodi, lakini angalizo langu ni kwamba lazima tujielekeze katika kuangalia ni maeneo gani ambayo tunataka misamaha hii ifanyike, kwa sababu siamini kwamba katika kila sehemu tunaweza tukafanya misamaha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tukumbuke kwamba misamaha hii inalenga sana katika ku-*encourage investors* waje wafanye *investment* katika nchi yetu. Maana tunatambua kwamba pia tunalo tatizo la mitaji katika uwekezaji wetu. Lakini tunapofanya misamaha ya kodi tukumbuke pia hii ni njia nyingine yak *u-discourage investment* kuja nchini kwetu. *In return* kama walivyosema ndugu zangu waliotangulia mimi siyo mchumi lakini hesabu za kiuchumi zinaonyesha kwamba sasa tunataka tuigeuze nchi yetu kuwa soko la bidhaa za nje maana leo hii kwa mfano tuna viwanda kama sikosei viwili kama siyo vitatu vya mabati. Tanzania leo hii tuna operesheni ondoa tembe sijui Singida huko, mabati yanayotengenezwa katika viwanda vyetu hivi hayawezi kutengeneza au kufunika Wilaya ya Manyoni peke yake, halafu leo hii tunaambiwa kwamba watu wanataka tuseme tuondoe hiyo misamaha kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependelea sana kwa upande wangu na ni wazo langu Mheshimiwa Waziri anapokuja kufunga mjadala huu angetoa majibu sahihi katika hili, jambo si kuondoa misamaha moja kwa moja lakini nafikiri tuainishe ni maeneo gani ambayo tunataka tuwezeshe ili iweze kutusaidia kuondoa au kuweka vizuri mazingira ya kiuwekezaji nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo nilipenda nichangie jambo la kilimo. Nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anachangia na bajeti ya Wizara ya Fedha ilivyoeleza inaonekana katika nchi yetu hapa kilimo kinachangia asilimia nne tu ya Pato la Taifa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, linalonichekesha kidogo hapa nchi yetu yote ni mashamba, nchi nzima hii ni shamba, maeneo pekee ambayo unaweza usikute mashamba kwa wingi labda ni mikoa ya Dar es Salaam na Arusha labda, lakini Moshi, nchi nzima hii eneo lote hili ni watu wanalima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kilimo chetu kinachangia asilimia nne ya Pato la Taifa, usalama wetu uko wapi? Leo hii tuna tatizo, SUMA JKT walikuwa wanaagiza matrekta, matrekta yale hayaagizwi tena, tatizo hakuna fedha.

Mimi nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa sisi wengine ni wakulima basi hizi fedha za kwenda SUMA JKT ili matrekta yaje wananchi wangu wanaotokea kule Kilemela, Msata, Kihangaiko, Mbwewe na maeneo mengine yote yanayozunguka Wilaya ya Bagamoyo basi nao waweze kupata na kufanya kilimo ule uti wa mgongo kama ilivyo kauli mbiu yetu katika maendeleo iweze kuonekana kwa vitendo. Lakini hii kusema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, lakini kumbe uti wa mgongo wenyewe ni asilimia nne ya mchango wa maendeleo katika Taifa hili, hili jambo kwa kweli si jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoamini huenda hizi *figure* labda wamekosea labda walitaka kusema asilimia 40, lakini kusema asilimia nne labda kama Mheshimiwa Waziri anaweza akawa kauli nzuri za kutuambia kuhusu jambo hilo.

Lakini pamoja na hilo ningependa pia niipongeze Serikali kwa juhudi kubwa zinazofanyika za kuhakikisha kwamba hali ya kiuchumi ya nchi inaendelea kukua. Lakini pamoja na hilo ningependekeza au ni wazo langu kwa Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake waliangalie pia tusiwe tunazungumza lugha ya kukua uchumi kwa Serikali wakati wananchi wetu bado wanaishi katika mazingira magumu. Mazingira lazima yafanane, hatuwezi kuwa hakuna *correlation* ya kukua kwa uchumi na maisha ya watu, bado shida zimeendelea kuwepo, mahitaji ya kupatikana kwa umeme katika vijiji vyetu bado ni makubwa sana, mahitaji ya kupatikana kwa dawa katika zahanati na vituo vya afya katika Tarafa ya Chalinze, Tarafa ya Lugoba na Tarafa ya Miyono, bado ni makubwa sana. Sasa tunapoambiwa leo hii kwamba uchumi wa nchi umekua halafu dawa bado hazipatikana katika vituo vyetu vya afya hivi, bado tunaendelea kupata shida ya kutafsiri vizuri nini maana ya ukuaji wa uchumi *as against* maendeleo ya watu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ningependa sana kuunga mkono hoja, lakini kuendelea kutia moyo Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwamba bado Jimbo la Chalinze na wananchi wake tupo nao bega kwa bega na tunaendelea kuwakaribisha tuendeleo kushirikiana katika maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, tunakushukuru sana umedhihirisha umahiri mkubwa katika uwasilishaji wako ama kweli wazungu walisema ukweli *like father like son*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Haroub Shamis atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu. *(Kicheko)*

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kutoa mchango wangu katika bajeti hii kuu ya Serikali ya mwaka unaotukabili wa 2014/2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kabla ya kuanza mchango wangu nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah kwa rehema zake na neema alizonineemesha mimi na familia yangu pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya shukrani hizo nataka nitoe pole niungane na Rais Jakaya Kikwete kuwapa pole Wazanzibar na Watanzania na wafia wa msiba ule wa bomu uliotokea Zanzibar juzi usiku baada ya *Salatil Inshai* pale Msikiti wa Darajani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachangia bajeti hii ya trilioni 19.85 ya mwaka huu fedha unatukubali ambazo kati ya hizo shilingi trilioni 13.4 zitakuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 6.4 zitakuwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna kitendawili kikubwa sana na kitendawili hiki amekithibitisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mzee wangu Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge aliposema kwamba na ninaomba kunukuu; "pamoja na Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa Bunge katika mchakato wa bajeti bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonyesha utayari wa kupokea ushauri katika maeneo ambayo Kamati imekuwa ikitoa hususan eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya." (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii fedha ambazo zitatumika kwa matumizi ya kawaida zina ziada kuliko makusanyo ya ndani. Kwa hiyo, hapo ndio ninapoona kwamba bajeti hii haitotekelezeka na napata wasiwasi sana kwamba vipi bajeti hii itatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nakisi ya zaidi ya trilioni 1.2 ambayo hizo ni kwa fedha ya matumizi ya ndani tu ya kawaida tu. Nakisi ya makusanyo ya ndani ni trilioni 1.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, inaonyesha kwamba fedha ambazo zitakopwa au misaada zitatumika kwa matumizi ya kawaida jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa nchi yetu.

Lakini pia bajeti hii ina tatizo la kutekelezeka kwa sababu Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dada yangu Mheshimiwa Saada na Mheshimiwa Waziri wa Uchumi na Mipango Mheshimiwa Wasira walipowasilisha bajeti zao hizi walisema kama bajeti hii imezingatia Ilani ya Uchaguzi wa CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo ndipo wasiwasi wangu unapozidi kwamba bajeti hii itashindwa kutekelezeka, kwa sababu Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mwaka mmoja tu baada ya kuingia madarakani mwaka 1996 alifanya uungwana akasema kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM haitekelezeki, sasa hapa na bajeti kama hizi inakuwa mtihani na mimi pia leo mwaka 2014 nathibitisha maneno yale aliyoyasema Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa kwamba Ilani ya CCM haitekelezeki. Kwa sababu Mheshimiwa Rais wangu mpenzi Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati tarehe 31 Desemba, 2010 akihutubia Taifa kuukaribisha mwaka mpaya alisema naomba nimnukuu alisema; "Kwa kushirikiana na sekta binafsi, ndani ya miezi 36 ijayo TANESCO watakamilisha ujenzi vituo vya kuzalisha umeme Kinyerezi megawati 240, Somangafungu megawati 230, Mnazi Bay Mtwara megawati 300 na Kiwira megawati 200. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kwamba sasa hivi wakati nimesema katika Bunge lako hili kuzungumza ni miezi 42 tangu maneno haya ameyasema imeshapita miezi 36. Sasa nataka Waheshimiwa Mawaziri hapa wakija watuambie kama bajeti hii waliyowasilisha imezingatia kwa kiasi gani utekelezaji wa Ilani ya CCM na ndiyo maana nikasema bajeti haitotekelezeka. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mtwara waliulizia juu ya jambo hilo kwamba Rais alituhidi kwamba tutajengewa hapa umeme kwa kipindi hiki umeme wa megawati 300 lakini baada ya kuuliza majibu yao waliyopelekewa ni kupelekewa na jeshi la kuwatandika, sasa sijui hii ndiyo llani ya Uchaguzi wa CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaloliona ni kwamba bajeti hii haiendani na malengo ya ukuaji wa uchumi ya Dira ya 2025. Malengo ya ukuaji wa uchumi wa Dira ya 2025 yanataka uchumi ukue kwa asilimia 10 ili tuweze kuondokana na hapa tulipo kuwa nchi hii ni nchi yenye uchumi duni na kuwa *medium income country* ambayo itatoka katika kipato cha sasa hivi cha Mtanzania cha dola 700 kwa mwaka mpaka kufikia dola 3000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukuaji wa uchumi ni asilimia 0.1 kwa mwaka, mwaka jana ulikua kwa asilimia 6.9 na mwaka huu tunaomalizia uchumi tumeambiwa umekua kwa asilimia 7. Sasa kwa ukuaji wa uchumi huu wa asilimia 0.1 kwa mwaka tutahitaji miaka 30 ili tuweze kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 10 na ikiwa uchumi huo utakwenda kwa ukuaji huu wa asilimia 0.1 kwa mwaka, lakini ikiwa itatokezea mwaka mmoja ikawa haukukua basi miaka 10 itazidi na sasa hivi tumebakia miaka 30 lakini sasa hivi tumebakia na miaka 10 kufikia dira ambayo ya 2025 ambayo inataka nchi iwe imefika katika lengo hilo la uchumi wa kati ambao wananchi tunaambiwa watakuwa na pato la dola 3000 kwa mwaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ndiyo linalonipa wasiwasi na kuona kwamba Serikali inadanganya wananchi na si jambo nzuri. Inatakiwa Serikali kwa sababu kama nilivyowahi kusema siku za nyuma, Serikali ni mlezi inatakiwa iseme maneno ya kweli kwa watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalosababisha kwamba uchumi ushindwe kukua katika Taifa letu ni kwamba wafanyakazi wa Serikali au watendaji wa Serikali hawafanyi kazi, ni *business as usually*, wanakaa maofisini huko wanatanua tu na mashangingi basi na hawa Mawaziri hawa dada yangu na wadogo zangu wale hawana ubavu wa kusimamia hili jambo kama alivyosema Mheshimiwa Ntukamazina kwamba kusimamia *Treasury* si lele mama na mimi kwa kweli namuonea huruma kwa mzigo huo wametishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kiburi wanakipata wapi watendaji kuwa hawataki kufanya kazi, kwa sababu hili Bunge letu sasa hivi limekuwa kibogoyo, halina meno. Kwa hiyo watendaji wanafanya bajeti *just copy and paste*, yale yale kila siku vyanzo vya kodi ni bia, sigara, pilipili. Sasa kweli tutakwenda lakini laiti kama Bunge hili lingekuwa lina meno barabara, Bunge linafanya kazi kama Bunge ya kuisimamia Serikali, likawa linashika nafasi yake, basi tungeweza kuisaidia Serikali kukusanya mapato kwa sababu mapato hayawezi kukusanywa bila ya watu kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo ninalolisema kwamba watu hawataki kufanya kazi Serikalini wamekalia ufisadi, rushwa na ubadhirifu tu ninao ushahidi, yupo mtu mmoja alinipigia simu juzi analalamika kwamba Wizara ya Ardhi kaomba ku-renew hati anadaiwa atoe rushwa ya shilingi 1,200,000/= ku-renew hati, mtu mwingine kaniambia anataka kupimiwa kiwanja chake ambacho kimeshapimwa *just* kuonyeshwa tu zile *beacon* zake vizuri kwa sababu watu katika ujenzi wanaingiliana anadaiwa rushwa ya shilingi ya 1,200,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na Mawaziri wanayajua mambo haya lakini wanashindwa kuwasimamia watendaji wao kufanya kazi kwa sababu Mawaziri ni sehemu ya Bunge na wao wanakuwa kule nadhani sijui, lakini labda na kule na wao wananyanyapaliwa. Lakini mimi ninachokishauri hapa Bunge lifanye kazi kama Bunge kwa nguvu ya Bunge kwa pamoja ili kuisaidia Serikali kusimamia iweze kufanya kazi yake, bila ya kusimamiwa hakuna kitakachofanyika. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine hapa dada yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kwamba na hili pia linathibitisha kwamba watu hawataki kufanya kazi. Kasema hivi sasa Serikali ina mpango wa kununua vifaa ambavyo vitadhibiti ubora wa miradi ya maendeleo, vitahakiki. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba hivi kuna kifaa kitakachofanya kazi bila ya mtu na kifaa gani?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Haroub. Baada ya Mheshimiwa Dalali Kafumu...

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mchangiaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Mheshimiwa Dalali Kafumu.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwanza kwa kunipa nafasi hii nami niwe mchangiaji kama Wabunge wenzangu.

Nawapongeza Waziri na vijana Naibu Mawaziri, vijana majembe hawa kwa kazi nzuri wanayofanya kulihudumia Taifa letu. Ni kazi kubwa kweli kufanya shughuli katika nchi inayoendelea yenye changamoto nyingi, lakini tunawashukuru kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Naomba kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuweza kuwalipa wananchi waliokuwa wanadai fedha kwa sababu ya kupisha mradi mkubwa wa kupeleka umeme kule Shinyanga. Nashukuru sana Wizara ya Nishati na Madini kwa kufanya kazi hiyo, naomba basi ikamilishe wale wengine ambao walirukwa nao waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichangie mambo mawili tu kwenye bajeti hii.

Jambo la kwanza ni bajeti isiyotosheleza ambayo tumekuwa tukiipata katika Bunge lako. Kwa miaka mingi kabisa tumekuwa tunapanga bajeti lakini mwisho bajeti inakuwa haitoshelezi, miradi mingi haitekelezwi kama walivyosema Wabunge wengine. Tumekuwa na utaratibu huu kwa muda mrefu, haitekelezeki kwa sababu fedha hazitoshi, fedha za maendeleo wale wachangiaji wa maendeleo ndugu zetu wanatuletea fedha wakati mwingine mwisho, mwisho au hawaleti kabisa wakati mwingine wanaahidi lakini hawaleti.

Pia tumekuwa na fedha chache kwa sababu hatukusanyi kodi vizuri na Wabunge wengi wamesema kwa kweli ukusanyaji wa kodi wa mapato katika Taifa letu haukidhi mahitaji yetu. Kwa hiyo, Wabunge wengi wamependekeza kwa kweli tuimarishe ukusanyaji wa kodi.

Moja ya maeneo ambayo na mimi nawaunga mkono ni kukusanya kodi ya majengo katika nchi yetu. Tuna majengo mengi kweli kwenye miji ambayo hayapo hata kwenye *database*, kwenye Halmashauri zetu kule unakuta watu wengi wana majumba lakini hawako kwenye *database*. Hebu tuimarishe jambo hili tunaweza kupata fedha ya kutosha kidogo.

Jambo lingine ukwepaji wa kodi. Wananchi wa Tanzania, wafanyabiashara na sisi wengi hatuoni kama ni wajibu wetu wa kupeleka kodi. Nchi zilizoendelea mtu anajipeleka mwenyewe kulipa kodi, Serikali ikichelewa anakwenda mwenyewe. Sasa na sisi hebu tuimarishe hii elimu tuone kwamba sisi wote tunastahili kulipa kodi. Tukirekebisha jambo hili watu wote wakalipa kodi vizuri tunaweza tukapata fedha ya kuhimili bajeti yetu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nililotaka kusema ni suala la kukuza uchumi. Namshukuru sana Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, focus yake kubwa ilikuwa ni kuinua uchumi wa nchi. Ukiinua uchumi wa nchi utapata shughuli nyingi na kodi itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, focus ya msingi zaidi ilikuwa ni kuhakikisha tunakuza *foreign direct investment* katika nchi yetu. Tualike wawekezaji waje, tuache huo mtindo wa kuwaita wezi. Nchi zote duniani zilizoendelea hata nchi kubwa hizi kama Marekani zinategemea zimealika sana wawekezaji kutoka nje. Nina *statistics* hapa zinasema nchi ya kwanza kwa *FDI* katika dunia ni Marekani ya pili ni Uingereza, zaidi ya trilioni 1.5 inaletwa kutoka nje na nchi zote za Ulaya zile ndiyo za kwanza katika *FDI*. Katika nchi za Afrika ni *South Africa*, inawezekeza sana, inawalika wawekezaji, wana mazingira mazuri na wanaenda wanawezekeza. Uchumi unakuwa, wawekezaji ni wa muhimu kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba hawa wawekezaji wakija ni lazima kujenga mazingira ya wawekezaji wa ndani nao washirikiane na hao ili kuongeza kitu tunachoita *local content*. Nchi hizi ni nzuri sana na China ni ya mfano. Kwa hiyo, ni vizuri tukajenga uchumi kwa kuruhusu *free market economy*, tushiriki kwenye uchumi huu wa dunia. Tusipofanya hivyo, tutashindwa kupata fedha kwa ajili ya kuendesha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni miradi ambayo haipati fedha, limekuwa ni tatizo kubwa sana. Mradi mmoja wapo ni ujenzi wa Daraja la Mbutu kule Igunga. Tulianza mwaka 2012 mpaka sasa hivi tunasuasua hatujamaliza. Naiomba Serikali daraja hili ni la muhimu sana kwa wananchi wa Igunga. Hebu tupeleke fedha basi pamoja na uchache wa fedha zetu tupeleke tulimalizie hili, mwaka 2015 iko hapa karibu karibu, tumalize hili daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni mradi wa kupeleka maji katika Mkoa wa Tabora kutoka Ziwa Victoria. Huu mradi ni ukombozi kwa kupeleka maji katika Mkoa wetu na hasa Wilaya ya Igunga. Wilaya ya Igunga niliwahi kusema hapa mapema ni Wilaya ya mbugani, maji ya chini yapo sehemu chache sana kwa sababu ya jiolojia yake, ni ziwa lililokauka na chini hakuna maji. Kwa hiyo, tunahitaji huu mradi utusaidie kama Wilaya kame tuweze kupata maji ya kutosha kwa ajili ya Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema tena naishukuru Serikali sana kwa kuwahudumia wananchi wa Igunga kwenye mambo mengi sitaweza kutaja miradi mingi, lakini tuna miradi mingi, lakini tuna miradi ya maji, tumeahidiwa umeme, tumeahidiwa minara na yote wakandarasi naona wanajitokeza wanafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono bajeti hii tuweze kuitekeleza na ushauri wa Wabunge huu tuliopoleka, basi Serikali uchukueni muweze kukamilisha shughuli yenu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu. Mchangiaji wetu wa mwisho asubuhi ya leo atakuwa ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mungu kupata fursa hii ya kuchangia bajeti ya Serikali.

Hata hivyo, kabla sijaenda kwenye hoja zangu nilizozipanga niliwasikia wakubwa wengine jana akiwemo Mheshimiwa Mbowe wanasema kwamba mwakani watakuwa upande

Nakala ya Mtandao (Online Document)

huu, kwa maana ya kwamba mwakani watahamia CCM, tunawakaribisha sana, warudi, maana kuwa upande huu bila kuhamia CCM ni kufanya vichekesho. Kwa hiyo, kuna mpango wa viongozi wa Kambi Kuu ya Upinzani kuhamia CCM, tunawakaribisha sana akiwemo Waziri Kivuli hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna tatizo lingine ambalo hapa Mheshimiwa Mwigulu fanya kazi, hii habari ya *scarf* watu waachane nayo kwa sababu sasa hivi utanafanya mambo ya kitaifa kama wanapenda wavae na wao wala hakuna shida. Mtu yoyote akiamua kuvaa *scarf* kama Mwigulu alivyovyaa anaruhusiwa kuvaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge, hiyo nilikuwa natoa kama utangulizi tu na umesikia jamaa wamepiga kelele hapa. Nimemsikia hapa rafiki yangu anapiga kelele, dawa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukusanya mapato, Serikali tunaiuomba ikusanye kodi. Kukusanya kodi unajua ukienda hata kwenye maduka unachekesha, kuna mtu mwingine anasema unataka risiti ya aina gani? Risiti lazima iwe moja tu, kama tunataka kukusanya kodi risiti iwe moja na tujue kabisa kwamba Serikali inapata mapato yake kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ni namna ya kusimamia Mfuko Mkuu. Mfuko Mkuu ukitoboka madhara yake ni makubwa sana. Nchi yetu sasa hivi uadilifu ni mdogo sana, unaweza kuona hata wakati fulani magazeti yaliwahi kuandika kwenye gazeti la Raia Mwema, fundi viatu mmoja kuna mtu alisahau begi lake pale akaenda akaifungua akakuta ina fedha, baadaye akaenda polisi akamtangazia mwenyewe. Mwisho wa siku Serikali haikumuita, haikumsomesha, watu kama watu wale ndiyo walipaswa kufanya kazi Hazina. Maana ni mwaminifu hata katika hali ngumu ya maisha aliyonayo. Sasa unajikuta asubuhi tena mgambo wameenda kuvunja banda lake na yeye mwenyewe ametolewa, yaani hatuwezi kulea watu wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza malezi na Serikali ianze kulea watu kulingana na umuhimu wao kule wanakotoka. Haiwezekani umchukue mtu anayekuja kuomba kazi kwa ajili ya kuiba. Mtu anakuja hapa anamtafuta Mbunge, bwana nitafutie kazi TRA, ukiuliza kwa nini, anajibu kule unatoka haraka. Yaani mawazo yake kabla hajapata hiyo kazi ni kwenda kuiba, ni kitu kigumu sana hicho. Serikali ianze kuchuja watu nani akae kwenye sehemu hii, uaminifu wake ukoje tangu kwao alikozaliwa. Haya mambo wanafanya, hawaajiri tu watu. Hii tabia ya kuajiri watu kwenye maeneo muhimu watu ambao siyo waadilifu inaumiza sana watu wengine walioko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu unaweza kumkuta kapata kazi miaka miwili tu maendeleo yake ni makubwa na ndiyo maana wakija kuandika ripoti wanaandika uchumi unakuwa kwa *speed*, lakini uchumi hau-*reflect* watu waliopo vijijini. Tukiwa tunazungumza tuangalie na hali ya nchi. Tumekwenda kule na Mheshimiwa Mwigulu nchini China, tumekuta China wanajenga Jimbo linaitwa Yunnan, kwa hiyo nguvu zote wameelekeza kule. Serikali huwezi kujua wakati gani inajenga mkoa gani na wakati gani inajenga mkoa huu. Hatuwezi kwenda kwa utaratibu huu. Lazima tuwe na utaratibu wa kuangalia vipaumbele na maeneo ya kupeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumzia mjini, tunazungumza mijini kwa sababu Wabunge asilimia kubwa tunaishi huko, lakini mimi Mbunge ninayekaa kijiji ndugu zangu kuna matatizo makubwa, kwa Wabunge na baadhi ya Wabunge wenzangu wanaokaa vijijini, ni tofauti na ninyi mnaokaa mjini. Mbunge kijijini yeye ndiye mzikaji, yeye ndiyo anauguza na yeye

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ndiyo anafanya kila kitu, ni tofauti na Wabunge ambao mnaishi mjini. Watu hawaelewi Mbunge anafanya shughuli gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mkikusanya kodi, mkaigawa vizuri, mkaisimamia, ikafanya kazi, hebu angalia utaratibu wetu wa malipo. Mfuko wa sementi unaonululiwa 15,000/= Serikali inanunua 18,000/= mpaka 20,000/= kwa sababu tu inachelewa kulipa. Kwa nini ichelewe kulipa wakati yenyewe ndio imepanga? Kwa hiyo, Tume yetu ya Mipango pamoja na Bajeti viendane sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kuhusu Pato la Taifa na mgawanyo na kukua kwa...

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mishahara. Unaweza kushangaa daktari mweye digrii mshahara wake na muuguzi mwenye digrii tofauti laki nne na wote wana digrii hawa, haiwezekani. Tunajua kabisa kwamba wapo madaktari ambao hawapimi damu, anapima mtu mwingine, daktari yeye anaandika dawa tu, lakini shughuli yote, daktari anafanya mambo mawili, kuandika dawa na kupima mtu amekufa basi, na kufanya vitu vingine na kuujua ugojwa na nini, lakini muuguzi anayeteseka na huyu mgonjwa tangu ameletwa pale, anakesha naye, anamuogesha, anazunguka naye mpaka anamfia, tofauti yake ni laki nne nzima, hebu tuzazame hilo. Tuweke Tume vizuri ipange mishahara kulingana na uzito wa kazi za watu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake mimi hapa nashangaa, tatizo lako wewe bwana mimi nitakugeukia, nitakuponda hapa halafu utachanganikiwa, mimi nakuheshimu niache bwana, unajua shida kubwa ya Ndesamburo yeye ni Mzee wa Kanisa lakini anaanza kupotosha maadili. Mimi ni mkristo mwenzako nachangia hapa, nyamaza kimya, utapewa nafasi utaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, hawa ndiyo wamezoea wanacheza wanaita *disturb marking*, wanakaba kwa ku-*disturb* ili upotee lengo, lakini mimi nimeshazoea hiyo, nina uzoefu mkubwa. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tudumishe utaratibu wa kukusanya fedha na kuzigawa sawa, tuwatendee haki, tunaposema kuimarisha nimeona hapa makusanyo mnavyokusanya. Mkikusanya fedha nyingi zaidi Wizara ya Fedha, katika bajeti hii mkapeleka kwenye Wizara vizuri, nawahakikishia shida ya maji itaondoka, shida ya nishati ya umeme itaondoka, shida ya barabara itaondoka, sasa tutageukia barabara za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia Peru tumekwenda nje sasa hivi, SACCOS ya machinga ndiyo inajenga miji mikuu ya nchi, sisi tuna watu chungu mzima hapa tunashindwa kuwaweka vizuri hapa, tunashindwa kuwakopesha, tunashindwa kuwasimamia, kazi yetu uchumi unakua, uchumi unakua. Mchumi yeyote ambaye hata jirani yake hajaweza kumsaidia, uchumi wake hauna maana yoyote. Ulichosomea uchumi kitu gani kama hata jirani yako nyumba ya tembe inataka kumua wewe una ghorofa. Unasikia ufahari gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuboreshe, tunapozungumzia habari ya kupeleka maendeleo vijijini. Vijijini ndiyo kuna Watanzania wengi wanaishi huko na sisi wengine wote tumetoka vijijini wala si tusijifanye watu wa mjini sana. Vijijini tukifungua barabara tukapeleka zahanati, tukapeleka dawa, tukapeleka umeme maendeleo yatakuwa makubwa kwa sababu wengi tuliop hapa ni watoto wa maskini, tatizo tunajisahau tu. Tukishaingia humu ndani tunajisahau tunafikiri haya ni maeneo ya kudumu haya, hapana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusukume maendeleo kwenye vijiji walipo Watanzania. Akinamama wajawazito wanashindwa kujifungua kwa sababu umeme hakuna, kwa sababu *operation* haiwezekani, kwa sababu mazingira hayaruhusu, haiwezekani. Tukiweka maendeleo vijijini tuna uhakika wa kuokoa maisha ya watu, tuna uhakika nchi yetu hata hawa walipa kodi ambao ni wazalishaji wakuu watachangia maendeleo kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njoo kwenye mazao, watu wanazungumzia pamba, lakini ukija Dodoma hapa zabibu inalimwa kama matunda pori, haina sheria yoyote, hakuna mtu anashughulika nayo mpaka sasa hivi kuna baadhi ya wakulima wamegeuka wanalima ufuta. Serikali isiposimamia hatuwezi kupata. Ukisimamia kilimo, kilimo peke yake kinatosha kuchangia sekta kuu na mambo yakaenda. Lakini kwa sababu tunakidharau watu wanalima kwa mkono na imekuwa adhabu hata kuishi vijijini, ndiyo maana unaona mzunguko wetu wa maendeleo unakwenda unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka niseme kuwa kuna *risk allowance* kazini, madaktari pale nilikuwa Milembe, mgojwa wa akili ameua mtu huko, analetwa pale amefungwa pingu na askari wana bunduki. Wakishafika pale wanamuachia daktari ambaye hana bunduki, hana chochote. Daktari anahojiana naye mgonjwa anamjeruhi, hakuna *risk allowance*, haiwezekani. Kama polisi amekuja naye na bunduki, huyu daktari unayemuachia mgonjwa wa aina hiyo bila kitu chochote yeye anafanyaje kazi? Serikali tazameni hilo na ndiyo maana nikasema hivi inakuwaje kwenye miji mikuu vitu vya namna hiyo ndiyo vinakuja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma mnaweka jela ya kunyonga watu, Dodoma hospitali ya vichaa, hivi hamuwezi mkaviondoa hivi mkapeleka Kilimanjaro ili na sisi mkatuletea vitu vya maana? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kilimanjaro hakuna hiyo.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Kwa wale ndugu zangu wa Kongwa huyu ndiyo Livingstone Lusinde mliyemlea kule akiwa kaiwa Katibu Msaidizi wa CCM Wilaya na sasa ni Mheshimiwa Mbunge hapa na ametutetea kweli kweli kwa kweli. Maana Dodoma hapa, basi nisiongeze.

Hata Halmashauri zetu za Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Waziri Mkuu baadhi ya watumishi wengi toka mikoa mbalimbali wakishaonekana kidogo, basi wanahamishiwa kuwa karibu na hospitali hii. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Halmashauri zetu mahesabu yake yanakuwa na taabu ninyi hamjajua sababu ni hiyo tu. Lakini na sisi tunawapokea hatuna tatizo maana tunajua lazima tuendane na hali halisi ya nchi.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru, uchangiaji unaendelea jioni tutakuwa na Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimwia Dkt. Haji Mponda, Mheshimiwa Mama Batenga, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimwia Dkt. Goodluck Ole-Medeye na wengine. Niwahakikishie wale wote ambao mpo kwenye orodha mtapata nafasi ya kuzungumza leo jioni.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hatua hii naomba basi nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili leo jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 06.56 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Majadiliano yanaendelea, tuanze na mchangiaji wa kwanza, Dkt. Hadji Mponda na wengine nitawataja kadri tunavyoendelea. Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda anza!

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya hadi kuwa na uwezo wa kusimama leo, angalau nami nichangie hotuba ya Mawaziri hawa wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza tena Mawaziri hawa wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mawasiliano na Uratibu) Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa Saada Mkuya, Waziri wa Fedha na Manaibu wake, kwa kazi nzuri ambayo wametuonyesha, wameianza vizuri na mwelekeo, wana uwezo wa kututenda haki sisi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, naomba nianze kwa kuuliza swali. Swali hili siyo langu, swali hili limetoka kwa wana Ulanga Magharibi, kutoka Tarafa Lupilo, Tarafa ya Mtimbila, Tarafa ya Malinyi na Tarafa ya Ngwelanga. Wameniliza, sina jibu; na ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, unapofanya hitimisho lako, basi ungetoa ufafanuzi. Wanapata wakati mgumu hawa!

Hotuba imeeleza kwamba, kuongezeka kwa pato la nchi, uchumi, umeenda kwa asilimia saba na tumeongoza katika *East Africa*, wenzetu wa Kenya wako asilimia sita, Uganda tano, kitu kama hicho, lakini wamekuja kuangalia, bajeti yetu tunazungumzia Shilingi trilion 19, wakati Wakenya pato lao linakua kidogo kidogo, bajeti yao ni mara mbili, wamefika Shilingi trilion 34 na Uganda wametuzidi sisi. Sasa wanaangalia, sisi tuko wengi, ardhi kubwa, watu zaidi, raslimali tunazo nyingi, kuna tatizo gani hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wenzangu wamezungumza sana suala la ukusanyaji wa rasilimali au mapato ya ndani, na hiki ni kilio kwa miaka yote, karibuni toka mimi nimeingia kwenye Bunge hili, na hata kabla sijaja hapa, Wabunge wanaiielekeza Serikali; jamani bado, kipato kiko chini. Majibu yanayokuja na Serikali yanaridhia, lakini bado zinatakiwa jitihada za zaidi, vinginevyo tutaendelea kulalamika, sungura mdogo, sungura mdogo, baadaye hatuwatendei haki Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mojawapo ya changamoto ambazo nimezisoma katika hotuba ni kutokamilika kwa urasishaji wa sekta isiyo rasmi. Sasa hii, tunaomba Serikali, mkazanie, mpaka lini? Mimi nilikuwa na wazo, nililitoa mwaka 2013 naomba nirudie tena. Hili zoezi la *National ID*, kama litaongezewa speed, litasaidia sana katika zoezi hili kwa kuwasaidia kupata hali halisi ya walipa kodi kwamba ni akina nani hasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niungane na Kamati ya Bajeti na ile *Chenge One* kwamba vyanzo vya pato bado ni vilevile; ubunifu, bado tunaubiri kwenu, lakini taarifa ya Serikali ni kwamba pamoja na maoni ambayo mmepewa, maoni nje ya Kamati ya Bajeti, lakini vilevile hata vyombo vya habari, vimeshiriki sana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nimesoma, *comments* hasa za wahariri, nawapongeza sana kwa Magazeti yote, wamechambua kwa kina bajeti hii na kuonyesha udhaifu huu na kueleleza wapi tunaweza tukaongeza vyanzo hivi. Naomba basi Serikali mfanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa Taifa wa Maendeleo, imeelekeza huu mradi wa ukanda wa SAGCOT, mradi huu kama kweli utasimamiwa, unaweza ukatatua tatizo ambalo tunazungumzia kwamba bado tuna kipato cha chini na bado tuna mfumuko wa bei, hasa mazao ya chakula, kama vile mchele na sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nina wasiwasi na ninaomba Serikali mnisikilize kwa makini sana, kwamba mwelekeo na jitihada mnazofanya katika mradi wa SAGCOT, changamoto mojawapo katika maeneo ambayo mmeyalenga, kwa mfano, kutoka lile bonde la Kilombero, bado kuna miundombinu ambayo hairidhishi na Serikali mmejipanga kwamba mko kwenye utaratibu mzuri wa kuweka barabara ya lami kuanzia Kidatu mpaka Kilosa Mpeto, Londo Lumecha mpaka Songea. Lakini hizi hadithi ni za muda mrefu, sasa hivi ni mwaka karibu wa nne! Bado tunawasikiliza kwamba mchakato unaendelea; tumekwama, tunasubiri *no objection*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *no objection* mpaka lini? Nakumbuka mwezi wa Tisa tulizungumzia hiyo hiyo *no objection*. Sasa tunaiomba Serikali, msisitize zaidi, mmalizie hii barabara, iwe hicho kiwango cha lami, ndiyo huo mradi wa SAGCOT unaweza ukawa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto nyingine katika hiyo miundombinu, ni daraja la mto Kilombero. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ameelezea, lakini sijaona kwenye mpango kama mmeweka utaratibu wa kulimalizia lile daraja. Sababu fedha mliyoweka ni Shilingi bilioni 7.5 tu, wakati bado kuna nakisi ya Shilingi bilioni 35 na karibu imebaki miezi saba sasa hivi kumaliza lile daraja. Sasa kweli hili daraja litakwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapooonea hapa, kama tungekuwa na uwezo wa kuangalia hali halisi kule kwenye Mto Kilombero, leo siku ya pili, magari yamekwama, hayaendi Ulanga, wala hayatoki Ulanga; kivuko kile kimechoka, kimeharibika, wamama wako pale wanateseka na magari karibu 300. Sasa hizo ndiyo changamoto, tunaomba muweke kwenye huo mpango, hili daraja liishe jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha *Volume One*, cha *Financial Revenue and Statement*, ukurasa wa 162, kimewapa maelekezo Mkoa wa Morogoro, Halmshauri zake kutengeneza pato la ndani Shilingi bilioni 19. Niichukulie tu Wilaya ya Ulanga, pato lake la ndani linatokana na kilimo cha mpunga na kilimo hiki kinafanyika katika maeneo ambayo sasa hivi wananchi wanazuia. Maeneo haya yanaitwa *buffer zone*, ni mpaka kati ya pori tengefu la bonde la mto Kilombero na ardhi ya kijiji.

Maeneo haya miaka mingi wananchi wanayatumia; maeneo haya wananchi kule wanaishi kihalali, vijiji karibu 18 vimesajiliwa.

Nimeiomba Serikali, na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ana nia nzuri, lakini naomba niwakumbushe tena kwa sababu toka ametoa dokezo lake tarehe 17, Aprili, leo ni siku 60 lakini Mawaziri wanne hawa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Waziri wa Maliasili, lakini hawajakaa pamoja na kuangalia namna gani wanaweza wakatimiza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie; tunachokiomba, sasa unakaribia mwezi wa saba, matayarisho ya kilimo kwenye hayo maeneo ya SAGCOT yanataka kuanza. Mheshimiwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waziri wa Maliasili na Utalii, sheria namba (5) ya mwaka 2009, imempa mamlaka ya kutoa matumizi angalau ya muda kwenye hiyo *buffer zone*, lakini mpaka leo bado anaweka katika mazingira magumu, wananchi hawa kila siku wana wasiwasi kama watalima au hawalimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali, hasa huyu Mheshimiwa Waziri, aandike tu hilo agizo, kwamba wananchi sasa waendeleo kulima na kuishi maeneo yale wakati mchakato unafanyika rasmi kuirudisha ile ardhi kwenye Serikali ya Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Rajabu!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Ibara ya 68 (7), naomba mwongozo wako; kwa sababu tunaendelea na majadiliano, na inaonekana meza kuu ya Serikali, kwa maana ya Waziri Mkuu, inabidi mwongozo wangu sasa hivi ukatike kwa sababu yataari, Waziri mmoja ameshakaa katika nafasi yake. Nakushukuru!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Samia kwa kutoa majibu mwafaka kwa wakati.

Baada ya Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, sasa atafuata Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa Betty Machangu ajiandae. Mheshimiwa Batenga!

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika hoja iliyopo Mezani. Kama walivyozungumza wazungumzaji wengi, nami pia ningependa niwapongeze Mawaziri waliowasilisha hotuba zao, lakini zaidi sana, nampongeza Mheshimiwa Saada Mkuya, ameonyesha ujasili mkubwa, ukomavu, lakini zaidi sana, kujiamini. Hakuna jambo kubwa kuliko kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hayo yote niliyoyasema, naomba pia awe msikivu na kupokea ushauri na kuutumia ushauri huo kwa kadri ambavyo utaweza kufanikisha kazi yake. Nikitambua kwamba, vijana alionao pembeni yake ni mahiri sana, ni wataalamu, nawaamini. Wakiongozwa na Waziri wa mipango, mambo yote ni sawia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba, sijui vigezo vilivyotumika kuteua Sekta za kuingia kwenye *BRN*, alizingatia nini, lakini mimi naona kwamba sekta muhimu ambayo imeachwa katika *BRN*, ni afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya binafsi mimi na wale hasa ninaowawakilisha (wanawake), tunafikiri kwamba *BRN* hii ingeingizwa na afya katika mpango huo. Kwa sababu tunayaona matatizo makubwa sana katika Sekta ya Afya hasa unapoangalia uzazi salama. Mazingira ya akina mama kujifungua ni magumu sana katika maeneo mengi hasa ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuleta mtoto duniani, ni jukumu zito sana, bahati nzuri wapo wengine ambao hawatawahi, yaani kupata uzoefu huo, kwa hiyo, wamshukuru

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mungu kwamba hakuwapa jukumu hilo. Kwa hiyo, niwaombe tu, watuenzi sisi na watupigie salute kwa kazi ngumu hiyo ambayo wanawake wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lekule Laizer ananiangalia, sasa nilikuwa namwomba, aje afanye majaribio aone; atakimbia! *(Kicheko/Makofi)*

Sasa mama huyu, sisi tumewahamasisha kwamba kipindi cha kujifungua waende hospitali. Lakini Hospitali, katika Zahanati, Vituo vya Afya vingine, unakuta hakuna vitanda vya kutosha. Wazazi wawili wanalala kitanda kimoja, pengine hata watatu! Sasa hii kwa kweli ndiyo maana nilikuwa nasema, basi afya ingeingia katika BRN. Hivyo kuhakikisha kwamba, Zahanati zinakuwa katika mazingira mazuri, zina watumishi wa kutosha, zina vifaa vya kutosha na madawa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine, wanawake wanakufa au na mtoto wote wanakufa wakati wa kujifungua kutokana tu na kukosa dawa zile za kuzuia kutokwa damu nyingi. Sasa haya mambo kwenye BRN, mimi nadhani ilikuwa ni vizuri sana na yenyewe iangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sijui wataingiza lini? Labda baada ya huu mpango wa kwanza kuisha ndiyo itaingizwa; lakini, mimi sioni kwamba tusebiri hiyo. Tuwaonee huruma akina mama! Nimesema tuwaenzi, tuwapende, tuone kwamba jukumu wanalolifanya kwa kweli ni zito, na kubwa. *(Makofi)*

Nimesema ambaye hajui, akafanye majaribio! Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe, katika kipindi hiki, tujaribu kuangalia ni namna gani tunaweza kuboresha mazingira ya akina mama kujifungua. *(Makofi)*

Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kuna jengo kubwa sana linajengwa, lakini lina miaka sijui karibu sita au saba, linajengwa haliishi, kwa nini? Ni kwa sababu ya kutowaenzi akina mama katika jukumu lao hili la kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hapo tu, ni maeneo mengi, kwa hiyo, niliona siwezi hili nikakaa nalo rohani, niliseme, kwa sababu nisipolisema ningebakia na deni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilikuwa nataka kuzungumzia malipo ya pensheni. Malipo ya pensheni ni madogo sana kiasi kwamba hayakidhi mahitaji, kwa sababu huyu anayelipwa kidogo ni yule aliyekuwa anapata mshahara mdogo. Kwa hiyo, malipo yake yanakuwa ni madogo. Lakini nitoe mfano kwa Wanajeshi, Wanajeshi wale wa ngazi za chini, wanastaafu katika umri mdogo, miaka 45. Miaka 45 anakuwa bado ana majukumu ya kulea na kusomesha. Sasa anapostaafu na kupewa pensheni kidogo, inamweka katika majaribu. Lakini izingatiwe kwamba Mwanajeshi huyu, akishakuwa Mwakajeshi ni mpaka kufa, yuko katika Jeshi la Akiba. Likitokea la kutokea, lazima aingie kwenye mapambano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, sasa tusiwaweke katika kuwajaribu katika uzalendo wao. Kwa hiyo, tuwape pensheni ya kutosha ili waweze kuendelea kukaa na kuzingatia maadili yao ya kijeshi na maadili yao ya ulinzi wa Taifa. Kwa hiyo, nawasemea Wanajeshi kwa sababu wapo wengi ninaowafahamu, na wengi ukiwaona wanakuwa katika hali ambayo hairidhishi. *(Makofi)*

Nikizingatia pia kwamba wapo na wastaafu wengine ambao pensheni yao ni ndogo. Sasa ningependekeza, kama wanavyolipwa Marais na wastaafu, Mawaziri Wakuu, basi angalau wapate kima cha chini cha pensheni, yaani sawa na kima cha mshahara.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Batenga, nakushukuru sana. Muda hauko upande wetu. Baada ya Mheshimiwa Elizabeth Batenga, sasa ni Mheshimiwa Betty Machangu, na Mheshimiwa Vincent Nyerere ajiandae.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi. Naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kupunguza kodi kutoka kwenye miashahara ya wafanyakazi. Naishauri Serikali kwamba kiwango walichopunguza cha asilimia moja ni kidogo, na laiti kama mwaka wa kesho wanaweza kupunguza ikafikia kama 9%.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Serikali kwa kukubali kupunguza misamaha ya kodi. Naomba sasa CAG awakague wale ambao watapata misamaha hii kwa ajili ya kujua kama misamaha imetumika vizuri. Lakini naipongeza pia Serikali kwa kuondoa *excise duty* katika hela inayokuwa *transferred* kwenye mabenki, badala yake wameweka asilimia 10 kwa yale mabenki ambayo yanafanya hizi *transfer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu kubwa ni kwamba hii asilimia kumi isije ikarudishwa kwa mlaji na haya mabenki. Kwa hiyo, nawaomba Serikali wasimamie hii kodi isije ikawa *indirectly passed over to the customer*, yaani wateja tukawa tunalipia ile kodi ambayo mabenki wamekatwa *ten percent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye mikopo. Serikali imekuwa inakopa mikopo ambayo ni *external non concessional loans*, hii ni mikopo ya biashara ambayo inategemewa iwe ni kwa ajili ya maendeleo, na maendeleo haya hasa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kule vijijini. Lakini mikopo hii inavyokuwa inakosekana inaathiri sana sekta muhimu kama umeme kwa sababu sekta hii ndiyo tunategemea isaidie pato letu la uchumi liweze kusogea badala ya 7% liwe 7.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu walitegemea kukopa Dola 700 lakini wamepata Dola 400 ambayo ni kama 58%. Naomba Serikali ituambie, hiki kilichoko kwenye bajeti hii ya sasa hivi kina uhalisia na kwamba hela zitapatikana kwa ajili ya utekelezaji uliopangwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye sehemu ya pili kuhusu *BRN*. Ukurasa wa 19 mpaka 20 umeongea kuhusu *BRN*. Naipongeza Serikali kwamba imetoa hela kama Shilingi bilioni 1.5 ambayo ni asilimia 92 ya fedha kupeleka kwenye *BRN*. Naomba niwapongeze sana Serikali. Lakini hii ni *supply side*, kwamba hii ni hela ambayo imetoka Serikalini, matokeo je? Sijona mahali ambapo kuna asilimia ya mchanganuo ya vile vigezo vya mafanikio, yaani *performance indicators* ambavyo asilimia imeonesha kwamba hili limefanikiwa kiasi hiki na hili limekuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuulizia: Je, kuna *analysis* ya kutosha? Matokeo tunayotegemea ni nini? Tujue kwamba kuna Mawaziri ambao waliweka sahihi kwa ajili ya hii *BRN*, na hawa Mawaziri tutawategemea baadaye watoe tathmini ya kina kwa yale ambayo wameyapata hasa watakapokuwa wana-*present* makadirio ya Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawa Mawaziri hawatapewa pesa za kutosha na wafanyakazi wa kutosha, itabidi Wabunge tuanze kugombana nao. Kwa hiyo, naomba Serikali iwawezeshe ili waweze kupata kweli faida na kujua faida ya hii *BRN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu reli ya kati. Uchumi wa nchi hii utaimarika sana tukijenga reli ya kati, lakini watu wanasema mtajengaje hakuna pesa? Lakini

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tunasema Serikali ya Tanzania imegundua *cubic feet* trilioni 50.5 za gesi ambayo wanasema thamani yake inawezekana ikawa ni zaidi ya Dola za Kimarekani trilioni 11. Mimi nikasema hawa kampuni ya *Ophir* ambayo imechukua mkataba na Serikali kwamba kwenye mauzo asilimia 75 itakuwa ni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wao wamechukua asilimia 20 ya *shares* zao; *share* tu, wala siyo gesi, lakini wakapata *1.3 billion Dollars*, kwa nini Serikali isiuze kiasi cha hizi *shares* zake kidogo za mauzo, yaani tukafanya *forward selling* kwa ajili ya kuuza hizo *shares* zetu 75 ambazo tunategemea gesi ili tupate hela za kujenga reli. Tukipata hiyo *1.3 billion Dollars* tunaweza kujanga reli mpya ikafika mpaka Isaka.?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo haliwezekani, basi kwa vile gesi ni ya kweli, tutoe *collateral*, tukope, tuendeleo kukopa. Waheshimiwa Wabunge, tunalalamikia kukopa, lakini kukopa siyo vibaya. Wataalamu wa pesa wanasema *debt money is cheaper than equity*; kwamba hela ya mkopo ni nzuri zaidi kuliko hela yako mwenyewe. Basi tutoe *collateral* ya kitalu kimojawapo au *shares* hizi tujenge reli. Maana ukiendelea kutia viraka tunadidimiza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujenga reli, maana yake tungeweka *dry port* kwenye eneo la Magharibi ya Tanzania na mizigo mingi ya nchi za jirani ingekwenda. Kwa hiyo, tungeweza tukatengeneza uchumi wetu ukawa mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongee kuhusu vitambulisho. Hakuna namna Serikali itaongeza wigo wa kodi kama Vitambulisho vya Taifa visipokuwa tayari. Ni lazima kila mtu apate kitambulisho ili TRA sasa waweze kumjua ni nani wamfuatilie, waweze kufanya *assessment* ya kutosha na kuweza kukusanya kodi. Lakini tukasema ni watu wa Dar es Salaam, watu wa Arusha watu wa Miji mikubwa wanalipa kodi na wafanyakazi; hatuwezi kupanua wigo wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ikikusanya kodi vizuri mwisho wa siku hata zile *rate*, viwango vya kodi tunavyolipa vinaweza vikapungua. Kwa hiyo, naomba Serikali ilione hili na iwape NIDA hela ya kutosha kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kuhusu PPP, wenzengu wameongea, na mimi pia nashangaa kigugumizi gani, ni miaka minane PPP, Sheria ya PPP namba 18 tumeitengeneza lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea. Kuna wakati Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji alisema kunahitajika utafiti, lakini naomba basi hiyo sheria ije Bungeni irekebishwe na huo utafiti uwe umeshafanyika na kanuni ziwe zimeshawekwa tuendeleo. Uchumi wa nchi hii utaendelezwa na sekta binafsi na siyo Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kidogo kuhusu leseni. Nadhani ni kifungu cha 96 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tuliiondoa *nuisance taxes*, zile kodi ndogo ndogo ambazo zilikuwa zinamsumbua mwananchi na Serikali inatumia gharama nyingi kwenye kukusanya hii hela ndogo.

Kule Kilimanjaro tunasema unauza ng'ombe kwa ajili ya kuongea kesi ya kuku, ambacho nadhani Serikali haitaki kufanya hivyo. Sasa nina hofu kweli kwa huu ulipaji wa leseni. Kama wajasiriamali wadogo wadogo tutakuwa tunawafuatilia, mara nyingi wanafunga yale maduka wanaauza jioni. Wakifunga yale maduka, wao hawapati na Serikali hawapati. Tutakuwa tumefanya nini?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iangalie vizuri sana, hizi leseni wanazosema zinalipwa, leseni za biashara ni leseni za namna gani; na ni leseni za nani? Ni za wafanyabishara wa kiwango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nishukuru kwa hilo, yangu ndiyo yalikuwa machache hayo, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu. Nakushukuru sana. Mheshimiwa Vincent Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha kisasa kabisa kwa kutumia *ipad*. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Chenge kwa kuwa muwazi kutueleza kwamba Serikali haisikii, lakini nampongeza zaidi Waziri Kivuli kwa kuonesha mwelekeo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefika hapa kwa sababu ya nidhamu. Serikali imeanza kuogopa kufanya biashara kwa sababu inaogopa watu wake hawana nidhamu. Leo Serikali mnatuambia hamwezi kuanzisha viwanda, ni kwa sababu ya uoga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia magari ya Serikali peke yake, ukaangalia idadi ya magurudumu, yaani matairi, tukawa na viwanda vya matairi soko la ndani linatosha. Nenda kaangalie magari ya abiria, magari ya mizigo na pikipiki. Tufikie hatua kama Taifa tuwaambie watu wa nje hatuhitaji biadha zenu, tunahitaji viwanda vyenu, na iwe kauli mbiu ya nchi kwa muda wa miaka michache tu, tutabadilisha tatizo la ajira, tupunguze kuleta biadha tuwaombe walete viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la PPP lazima tuwe waangalifu. Kuna mambo ambayo lazima Serikali ifanye yenyewe. Ukichukua barabara, ukabinafsisha ukampa mtu wa nje, halafu leo Mtanzania akatozwa kodi kwenye kutumia barabara ya nchi yake, nchi hii haitakalika. Kwa hiyo, ni lazima tuwe waangalifu sana katika vitu ambavyo tunataka kubinafsisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani siyo kwamba hatuna watu wa kufanya kazi hii, hebu niambie mtu kama Mohamed Keissy, leo akimaliza Ubunge ukampa Shirika la Umma kuna mtu ataiba? *(Kicheko)*

Wapo watu wanaoweza wakafanya kazi nchi hii, hatuwezi kusema hawapo! Angalia liliyokuwa Shirika la Nyumba, mmempa kijana mmoja simfahamu, lakini leo Shirika la nyumba linakwenda. Tumekaa tunaogopana; hapa chenji ya rada ilikuja, walioiba wapo, tunakaa tunachekeana, hakuna adhabu! Mimi nadhani kama biadha za kichina ni *fake*, basi tuchukue sheria zao, tuachane na biadha zao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la ukaguzi wa magari, alisema hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba anayo *data*, magari yaliyotumika ndiyo yamesababisha ajali na yameua watu wengi. Nadhani aliyemletea *data* hii hana nia nzuri na yeye. Magari yaliyoua watu wengi ni mabasi na mabasi yameingia mapya. Kwa hiyo, magari mapya yameua watu wengi. Mimi nilikuwa nadhani suala la ajali, ukitaka kutuambia kwamba magari maze ndiyo yanasababisha ajali; juzi mama Tibaijuka amepata ajali, na ni Waziri, anatembelea gari jipya! Kwa hiyo, zile *data* nadhani dada yangu kaangalie vizuri, siyo kweli.

Masuala ya kuchafua mazingira, hayo yanajulikana. Tunaweza tukawa na *conversion kit* kutoka kwenye *diesel* kwenda kwenye gesi, na vitu vingine kama mtavisamehe kodi kwa ajili ya kuokoa mazingira.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka hapa kuna Mawaziri waliachia ngazi zao kwa sababu ya ukaguzi wa magari nje, tukategemea taratibu zitabadilika, lakini matokeo yake mlitubadilishia sura za Mawaziri badala ya kubadilisha utaratibu. Ukaguzi wa magari uko vile vile, hayakaguliwi, watu bado wanapiga hela. Haijulikani! Sasa hivi nikimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa, gari moja kukagua ni Shilingi ngapi na nchi inapata Shilingi ngapi katika kila gari, sidhani kama anajua! Kama anajua aje atuambie halafu mimi kesho nimletee data.

Wakati ule walikusanya Dola milioni nane; ni Dola milioni mbili peke yake zilikuja Tanzania. Tulitegemea kwamba kwa sababu tuna vijana wengi wamesoma VETA, tuna *Vehicle inspectors* wa kutosha, tutafanya kazi ya ukaguzi nje na ndani. Tungekuwa tumefanya hivi tangu mapema, leo msingekuwa mnasumbuka kutafuta pesa ya Polisi kwa ajili ya *Ration Allowance*. Ni fedha nyingi sana za ukaguzi wa magari!

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tumekuwa na *Regulatory Authorities* nyingi kweli kweli zinafanya kazi. Kuna *TFDA*, sijui kuna nini, kila moja ina Mkurugenzi wake ina watu wake wengi. Unganisheni, punguzeni hawa watu, wafanye kazi kwa pamoja, wawekwe *under one roof*, wakafanye kazi pale bandarini na kwenye *border point*, tupunguzie watu wetu mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hivyo mtang'ang'ana; kama tutaamua kubanana na *Regulatory Authorities*, zikapunguza wingi wa wafanyakazi, zikafanya kazi muda wa kutosha bila kuathiri kodi, tutajikuta Serikali haiathiriki kikodi, lakini Mtanzania wa kawaida anapunguziwa mzigo. Kwa sababu mfanyabiashara siku zote bei yake anapanga baada ya kuangalia *cost* tangu amenunua mpaka amefikisha dukani kwake au sehemu anayouzia ndipo anapanga bei.

Kwa hiyo, kama kuna *Regulatory Authorities* nyingi, tena ukitaka vichekesho, nenda ukaangalie watu wanaoingiza *container* za vyakula. *TFDA* akija *sample* anachukua gunia; wakija sijui nani *sample* wanachukua gunia; yule mfanyabiashara anachokifanya, yeye anaangalia ni magunia mangapi yametoka kwenye kontena zake, anaweka *cost* zake mpaka mwisho halafu mwisho kabisa anakwenda kumbandikia mtumiaji wa mwisho gharama zote hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri sasa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent, *sample* gunia!

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Kwa sababu hujawahi kufanya biashara, huwezi kujua hiyo! Kama una wasiwasi, nenda kawaulize. Sukari, mtu badala ya kuchota kijiko cha sukari kwenda kupima *sample*, anachukua gunia zima na halirudi. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Sasa Madaktari nao wakianza kuchukua madebe ya damu, si binadamu wataisha! Endelea Mzee, hiyo *sample* babu kubwa hiyo! (Kicheko)

MJUMBE FULANI: Hazirudi!

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi inanisikitisha sana kuona hata Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anaomba fedha za kodi kulisha wafungwa. Mimi ningekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, mwaka wa kwanza ningepomba matrekta kwa sababu yapo maeneo ya Magereza, wapo wafungwa walihukumiwa kazi ngumu, wanalala tu! Walitakuwa walime, wazalishe! Wanaweza wakawa na chakula cha kutosha kwa wao na ziada kwenye mashule na Vyuo na nyingine tukauza na wakafanya kazi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

nyingine, wakalima kwa ajili ya biashara. Lakini leo wanalala, wanakula, anakuja Waziri hapa anaomba fedha ya kulisha mtu ambaye ameniibia mimi, fedha niliyokatwa mimi nimlishe tena, tunekwenda wapi? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani, mwambie Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, anataka matrekta mangapi? Atuambie ana wataalam wangapi? Kuna wafungwa wamehukumiwa kazi ngumu, wakazalishe walishane wenyewe ili fedha ya kulisha wafungwa tusimwone Waziri wa Mambo ya Ndani anakuja kuomba hapa. Halafu hawa Mawaziri wenye *Regulatory Authorities* tuwe na utaratibu, kabla ninyi hamjasoma bajeti yenu, waje watuambie Wizara yao imeleta kiasi gasi, siyo wanaomba tu, wanachukua wanakwenda! Halafu wamekuwa wanaomba fedha in *public* lakini wakirudi hawatuambii wametumiaje, wamepata ngapi? Kila mwaka wanaomba tu wanachukua wanakwenda na hatujui nini kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima turudishe nidhamu kama ilivyokuwa mwanzo. Hivi Serikali eti inaogopa kufanya biashara! Watu mliowabinafsishia viwanda; hawana jeshi, hawana usalama wa Taifa, hawana Posili, wanaweza kusimamia biashara zao! Ninyi Serikali wenye vitu vyote hivi mnashindwa nini? Turekebishe sheria, tuongeze Magereza, mtu aamue. Aidha, afungwe au aje asimamie twende mbele. Siyo hivi tunavyofanya. Tutabaki tunalalamika! Mimi nilalamike, Spika alalamike, Ridhiwani naye analalamika! Sasa nchi inakwenda wapi? *(Kicheko)*

MJUMBE FULANI: Akakae na baba yake sebuleni kule!

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mvutano wa manunuzi ya mashine za kibaiolojia...

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Ni ya kwanza hiyo! Nashangaa Wizara ya Mambo ya Ndani wanataka kununua mashine kwa ajili ya kuchukua alama za kibaiolojia kwa vitambulisho vya Taifa, halafu hawa wa Tume ya Uchaguzi, pia wanakuja kuomba fedha kwa ajili ya kazi hiyo hiyo tena. Tunanunua mara mbili kwa ajili ya nini? Mimi nilikuwa nadhani viwepo vifaa vya Serikali; kama wamekwisha nunua Wizara ya Mambo ya Ndani, tuwaachie kazi hiyo, halafu Tume ya Uchaguzi wakihitaji, watumie hivyo hivyo! Tunakuwa na vitu vingine; unajua vitu vingine tunapigwa kwenye manunuzi!

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuzuia utengenezaji wa Kalenda. Lakini amezuia utengenezaji wa kalenda, wenzake wamebuni vikao. Lazima Idara za Serikali na Wizara tuwe tunajua ni vikao vingapi kwa mwaka? Wanahudhuria wangapi? Posho ni Shilingi ngapi? Wewe unazuia Kalenda, wenzako wanatengeneza vikao; idadi ya vikao vinaongezeka, kwa hiyo, wizi uko pale pale! *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani katika majumuisho yako, toa maagizo tu; tunataka kila Wizara na Idara zake watuambie vikao kwa mwaka ni vingapi, wahudhuriaji ni wangapi na posho ni kiasi gani. Leo unakwenda kwenye Ofisi ya Serikali eti unaambiwa wamekwenda kwenye kikao cha kukumbushana sijui mambo ya UKIMWI. Leo hii kuna mtu yuko Serikalini hajui UKIMWI unaambukizwaje? Posho, Shilingi milioni! Hebu tuache vitu ambavyo vinaturudisha nyuma, tuangalie kwenda mbele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Vincent Nyerere. Mheshimiwa Said Juma Nkumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kuunga mkono hoja, lakini nataka nimwambie mdogo wangu Mheshimiwa Vincent hapo, kwamba amesema Mheshimiwa Waziri Kivuli ameanza kutoa mwelekeo; kivuli ni kivuli tu! Hakuna kivuli kinachoweza kutoa mwelekeo, maana kivuli kinategemea jua liko wapi! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile asubuhi nimemsikia Mheshimiwa Khatib, anasema yeye kazi yake ni kutema tu! Anakohoa na kutema! Nimeshtuka! Nikiangalia siha yake, hafanani na hiyo! Sasa nilikuwa naomba, labda tumsaidie. Lakini vile vile akitema, afukie kwa sababu atatuharibia mazingira, maana kila mahali kama unatema tu, kila mahali, ni tatizo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Wizara na Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Lakini nimpongeze kwa dhati kabisa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kinana kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi akisaidiana na Waheshimiwa Wabunge wake katika Majimbo husika. *(Makofi)*

Nimesikia kelele zinapigwa, ooh Katibu Mkuu kwa nini anafuatilia? Nataka tukumbushane; Serikali iliyoko madarakani ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, unapompata Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, anayefuatilia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi lazima tumshukuru na tumpongeze sana. Sasa wale wanaolalamika, waendeleo kusubiri miaka sijui mingapi ijayo; Mungu pisha mbali, lakini kwa sababu nina hakika Serikali hii itaendelea kubaki ndani ya mikono ya Chama cha Mapinduzi, tutaendelea kuwapa Watendaji Wazuri kuendelea kuhakikisha kwamba CCM inaendelea kuhakikisha ilani yake inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Afya kwamba baada tu ya Mheshimiwa Katibu Mkuu kupita na kusikiliza malalamiko ya wananchi, akisaidiana na Waheshimiwa Wabunge, hasa katika Mkoa wa Tabora, Wizara ya Afya imechukua hatua mara moja kufuatilia kila mahali ambako kumetolewa malalamiko.

Nilikuwa naomba Wizara nyingine ziige utaratibu wa namna hii. Mnaposikia kwamba, kuna matatizo, nendeni. Nendeni mkaone hayo matatizo, maana wengine wanalalamika, ooh, hakuna kuingiliwa utendaji hapa! Huyo anayekwenda kukagua utekelezaji wa Ilani, ndiye mwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Wewe unalalamika nini? Kazi yako ni kwenda kufuatilia na kutatua kero hizo! Kwa hiyo, nawapongeza sana Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Sikonge, endeeleni na utaratibu wa kufuatilia ile Miadi ya Afri, mhakikishe imekamilika. Lakini vilevile uhaba wa watumishi mhakikishe na yenyewe mmeitolea ufumbuzi. Mnafanya vizuri sana Serikali kwa Walimu kwa sasa, lakini tunayo matatizo kwa Watumishi katika nchi nzima. Kwa watumishi wa Kilimo, kwa Watumishi wa Afya, tujitahidi sana katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Serikali hii inapoteza mapato mengi sana kwa kuendelea kutotolea ufumbuzi tatizo la wagufaji na wakulima kuendelea kuwa na migogoro. Wafugaji wakiwezesha, wakawa na maeneo ya kuchungia Mifugo yao. Wakawa na Maeneo ya Maji, wanaweza wakazalisha na kwa namna moja ama nyingine wakasaidia mapato katika Taifa letu. Lakini wakulima na wenyewe wawezeshe, waweze kulima vizuri, waweze kuzalisha vya kutosha ili waweze kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo hili nilikuwa naiomba sana Serikali sikivu hii ya Chama cha Mapinduzi, zipo Hifadhi, nami natoa hili kama eneo moja tu. Migogoro hii iko mingi tu, lakini ziko hifadhi ambazo tayari zilikwishakosa kabisa hadhi ya kuendelea kuitwa Hifadhi za Taifa. Yako baadhi ya maeneo mengine unaweza kwenda kuwinda hata wiki nzima unatafuta Sungura humpati. Lakini bado inaitwa Hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba, Waheshimiwa Wabunge wameshasema hapa mara nyingi, yako baadhi ya maeneo, hebu Serikali iyaone. Kwanza, kuendelea kulinda Hifadhi kwa eneo kubwa sana, ambalo hamna uwezo nalo, mnapoteza fedha nyingi sana kwenye kulinda, lakini vile vile Askari tulionao ni wachache. Kwa nini Serikali isione baadhi ya maeneo ambayo Hifadhi hizi zimekosa hadhi, kuwapa wakulima, kuwapa wafugaji waweze kushughulika na masuala ya kiuchumi ambayo yataweza kulipatia Taifa letu rasilimali? Nilikuwa naiomba sana Serikali katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni maji. Hii ni agenda kubwa sana, mwaka 2010 Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni lazima kwa namna moja au nyingine iendelee kuzingatia. Wananchi wanahitaji Maji. Lakini kwenye jambo hili, kwa nia njema nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi nzuri anayoifanya akishirikiana na Naibu, pamoja na Wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajika sasa Serikalini ni kuiwezesha Wizara hii iweze kupita kila mahali ili kukamilisha ahadi ambazo Chama cha Mapinduzi kimezitoa, kutekeleza hili kunahitaji fedha. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iendeleze jitihada za kuhakikisha kwamba miradi ya maji inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sikonge nawaomba sana Bwawa lile la Ulyanyama liishe. Maji kwenye eneo la Kitunda, tumalize tatizo la maji kwa wananchi wetu na tatizo la maji kwenye eneo la Kiyombo. Nawapongeza sana kwa mradi ule wa maji ambao unaendelea kukamilika katika eneo la Mibono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda vile vile nimpongeze kwa dharti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kauli yake aliyotoa alipokwenda Tabora hivi karibuni, kwa kuliagiza Jeshi la Polisi lianze sasa kufanya kazi ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo na malalamiko ya Wakulima wa Tumbaku wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naiomba Serikali, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais, ametoa agizo hili Tabora, basi ni vizuri, maana mmemsikia Mheshimiwa Kawawa analalamika; ukienda kwa Wakulima wa Pamba, na wenyewe bado wanaendelea kulalamika; ukienda kwa Mheshimiwa Mrema kule Vunjo, wakulima wa Kahawa wanalalamika; watu wa Lindi wanalalamika! Mazao yetu makuu bado yanaendelea kulalamikiwa sana na Wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Serikali, pamoja na kauli aliyotoa Mheshimiwa Rais, Serikali ichukue sasa kama hii ni kauli ya kuanza kuwasaka watu wote ambao wanatumia nafasi zao za ushirika, nafasi zao za Uongozi katika kuhujumu mali za wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, ili tutafute ufumbuzi sasa wa kuhakiokisha jambo hili linaisha haraka, tumepitisha sheria hapa ya mwaka 2013 inayohusu Vyama vya Ushirika. Halitakuwa jambo jema sana tunapitisha sheria, halafu tunaendelea kukaa miaka miwili, mitatu. Tumepitisha sheria, Kanuni zitengenezwe kwa haraka zianze kufanya kazi. Huo ndiyo utakaokuwa ufumbuzi wa kutatua matatizo ya wakulima wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiswa Nabu Spika, baada ya maneno haya, naendelea kuomba tena kuunga mkono. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuiwezeshe Wizara hii ili iweze kuziwezesha Wizara nyingine ili tuweze kufanya mafanikio ambayo Chama cha Mapinduzi, imeendlea kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaendelea kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Said Juma Nkumba kwa mchango wako. Mheshimiwa huyu anatoka kwenye eneo ambalo wale Wanyamwezi wana matatizo ya Kilimo, kiasi ambacho Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM alipokwenda huko alitoa machozi.

Sasa namwita Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kutambua watu waliofanya kazi kubwa sana katika maandalizi ya Bajeti hii, ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya, amekabidhiwa jukumu la kuongoza Wizara hii mwishoni mwa mwezi Januari, 2014. Ni miezi michache sana imepita toka amechukua kazi hii. Lakini kazi aliyofanya yeye pamoja na timu yake ya Manibu Mawaziri, Mheshimiwa Adam Malima, na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, pamoja na Makatibu Wakuu, Dkt. Likwelile na wenzake; ni kazi kubwa sana, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane ukweli kwamba muda waliokuwa nao ni mfupi sana wao kuweza kurekebisha upungufu wa aliyokuwepo katika *system*, na hivyo maoni mbali mbali ambayo yametolewa na Kamati, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge waliochangia yanatokana na hali hiyo. Kwa hivyo hiyo haituzui sisi kutambua kwamba kwa muda mfupi waliokuwepo wamefanyakazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi ni mjumbe wa kamati ya Bajeti, hivyo sina budi kuunga mkono taarifa ya Kamati hiyo. Baada ya kusema hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu kwa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2014/2015. Naomba nianzie suala la Sera za Kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo aina mbili za Sera za Kifedha. Tunayo ile tunayoiita *Physical Policy* na tunayoiita *Monitory Policy*. *Physical Policy* katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona kwa kiasi kikubwa kwa kweli amejitahidi sana kuona ni namna gani Sera hizo za Kiuchumi, na kifedha zitachangia ukuaji wa uchumi wetu. Lakini yako maeneo ambayo mimi kwa imani yangu, kama zingetazamwa kwa undani zaidi tungeliweza kuchangia vizuri zaidi katika ujenzi wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya malengo ya *Physical Policy* ni kuchochea ukuaji uchumi. Ili kuchochea ukuaji wa uchumi ni lazima tuangalie; moja ya vitu vinavyotazamwa ni kodi. Kodi kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonyesha, zitaongezeka. Kwa maana ya kwamba Misamaha ya Kodi itapungua na hasa kwa wawekezaji ambao tumewaita, tumewavutia waje watusaidie kuwekeza ili uchumi wetu upate kukua.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza, hili ni suala la Kodi ya Mapato ya Mfanyakazi, yaani *Pay As You Earn*. Kwa *Principle* za kiuchumi, unapowapunguzia watu kodi, maana yake ni kwamba unawafanya wawe na fedha nyingi zaidi katika mifuko yao ambazo watatumia ama kuwekeza au kutunza familia na kuweza kufanya shughuli nyingine ambazo wanahitaji fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumempunguza kodi kwenye mshahara wa mfanyakazi kwa asilimia moja. Mimi natoa wito kwa Mheshimiwa Waziri, afikirie upya suala hili. Tupunguze kodi ya mapato ya mfanyakazi, angalau ifikie asilimia tisa. Kama tutashindwa kupunguza zaidi, lakini angalau ifikie asilimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika hili suala la kodi, tarehe 11 Desemba, 2012, Mheshimiwa Waziri alikuwa miongoni mwa Viongozi wa Serikali waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu pale Kibada Kigamboni, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliagiza, Waziri wa Fedha atazame upya Sheria ya VAT ili nyumba za gharama nafuu zinazojengwa na Shirika la Nyumba na kuuzwa kwa wananchi wa kipato cha kati na cha chini, ama kiondolewe kabisa VAT, au kipunguziwe kodi hiyo. Kwa masikitiko makubwa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja na hata Muswada wa Sheria ya VAT, hilo halijatazamwa. Naomba sana kauli za Mheshimiwa Rais wetu, maagizo yake tuyaheshimu, tuyafanyie kazi kwa sababu anatoa kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi na Watumishi wa Serikali walipouziwa nyumba, hawakukatwa kodi yoyote. Hawakutozwa kodi! Kwa nini wananchi hawa wa kipato cha chini wasiwezeshe nao kumiliki nyumba kwa gharama nafuu kama tulivyofanya kwa Viongozi wa Serikali? Naomba sana tulitazame hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Monitory Policy* huangalia mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Tunaangalia kwa mfano *inflation*, tunaangalia ukuaji wa uchumi; hizi *elements*, halafu tunaangalia na *Consumer Price Index*. Tunalinganisha hizo na kuona ni namna gani basi tutaweza kurekebisha *factors* nyingine zinazoongoza uchumi ili uchumi wetu uweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado riba inayotozwa na Mabenki ni kubwa sana. *The Monitory Policy has not address this issue*. Wakati umefika sasa, kwamba kama kweli tunataka kuwawezesha wananchi, Watanzania kuwekeza katika miradi ya maendeleo, ni lazima tupunguze riba inayotozwa na Mabenki, ambapo hili liko ndani ya uwezo wa Benki Kuu. Naomba sana hili tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia suala la matumizi ya Serikali na mikopo ya Serikali, kwamba Mikopo imekuwa mingi. Mimi sioni tatizo kama Serikali itakopa na kuwekeza ili kukuza uchumi! Naunga mkono kwamba wakope kwa ajili ya kukuza uchumi ili mradi kwamba deni liwe linavumilika. Lakini siwezi kuunga mkono ukopaji kwa ajili ya Uwekezaji usio na tija. Siwezi kuunga mkono!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba Serikali ituambie mwaka 2009/2010, tulikuwa na mdororo wa uchumi duniani, Marekani pamoja na nchi za Ulaya, zikaanzisha kitu kilichoitwa *Economic Stimulus Package*, Taasisi zilizokuwa zimeathiriwa zikapewa fedha na Serikali. Kwa nchi za wenzetu; Ulaya na Marekani, Serikali ilichukua hisa kwenye Taasisi hizo. Sasa hivi uchumi wao umeimarika, Serikali inianza kuuza Hisa zake kutoka kwenye Taasisi hizo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuelezwwe, *impact* ya uwekezaji katika Taasisi ambazo Serikali imetoa fedha kupitia *Stimulus Package* ambazo naamini tulikopa, karibu Shilingi trilioni mbili tulizowekeza kule, tunahitaji maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Uchumi Endelevu. Hatutaweza kujenga Uchumi Endelevu, kama Serikali haisaidii wananchi wake waweze kuwekeze. Ni lazima tuwawezeshe wananchi, hasa walioko vijijini wanaolima. Lazima tuwape pembejeo kwa gharama nafuu. Serikali igharamie. Marekani imeweza kujenga uchumi endelevu kwa sababu imetengeneza mazingira ya wananchi kuwekeza, kuvuna na kuweza kuuza ndani ya nchi, hivyo Marekani kupunguza kutegemea vitu vinavyotoka nje ya nchi. Lazima na sisi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhsu miundombinu. Reli tuliyonayo kama tusingelitawaliwa na Mjerumani na Mwingireza, tusingekuwa na reli nchi hii. Ukiacha reli ya Uhuru, tangu tupate uhuru hatujajenga reli. Tumejenga hiyo reli ya Uhuru ambayo tumesaidiwa na Mchina, tumejenga kilomita chache sana ya Manyoni kwenda Singida. Hiyo haitoshi! Naomba Serikali sasa ihakikishe inawekeza kwenye Reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara Vijijini. Tumekuwa tukikazana sana kujenga barabara Mijini. Barabara za Vijijini hali ni mbaya sana. Lazima tuwekeze kwenye ujenzi wa barabara vijijini. Wananchi wa Vijijini ndio wanaotulisha sisi tulioko Mjini. Lakini hata namna ya kusafirisha mazao wanayozalisha, hawana kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali izitizame barabara hizi, hususan katika Jimbo langu mimi, Mheshimiwa Rais alituhidi barabara mbili za lami. Tunaomba barabara hizo zijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni vyanzo vipya vya mapato. Viko vyanzo vingi. Kwa sababu ya muda, nashauri, tuanzishe tozo kwa maana ya mrabaha kwa Uvuvi wa Bahari Kuu. Sasa hivi ushuru wa leseni ni Dola 34,000, kwa leseni tunayoita *Liner*. Nashauri tutoze mrabaha wa angalau asilimi moja. Kiasi wanachopata wavuvi hawa ambao ni wa Kimataifa, ni kubwa sana, wachangia maendeleo ya uchumi wetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nitawasilisha maoni mengine kwa maandishi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye. Kama nilivyosema, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae. Mheshimiwa Chiku Abwao!

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niseme kwamba kazi yetu sisi *opposition* ni kujitahidi kuhakikisha tunaboresha utendaji wa Serikali kwa kuikosoa pale ambapo tunaamini kwamba haitendi vizuri. Siku kama tutakaa hapa tuanze kuipongeza tu Serikali ina maana kazi itakuwa imekwisha. Vilevile ieleweke kwamba tunapokosoa, haina maana hatuthamini kazi inayofanyika, kazi inayofanyika ipo; lakini kwa kuwa upungufu ni mwingi, na muda tunaopewa kuchangia ni mfupi, inabidi tukazie yale ambayo tunaamini tukiyasema yataleta tija.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kukaa hapa na kutuponda sisi kila tunapojaribu kuwasaidia kuboresha Serikali, ili kuleta ufanisi, hamtutendei haki. Ni wajibu wetu na ni haki yetu na ndiyo kazi iliyotuleta hapa kuhakikisha kwamba Serikali iliyopo madarakani inawajibika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba niwapongeze sana Wasemaji wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Esther Matiko. Kwa kweli wametuwakilisha vizuri sana, hotuba hizi ni hotuba ambazo zimewasilishwa kwa lengo jema kabisa na zinafaa. Naomba sana Waheshimiwa Mawaziri mzipokee na mzifanyie kazi. Lengo letu ni kuleta ufanisi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Andrew Chenge na Kamati yake ya Bajeti. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri! Wanafanya kazi nzuri kuanzia *Chenge One*, mpaka sasa sijui tuiite *Chenge Two*, lakini ukweli ni kwamba wanaleta mapendekezo mazuri sana, na wanaonekana kabisa wanafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha pale inapofikia Mwenyekiti wa Kamati anakuja kusikitika ndani ya Bunge hapa kwamba mapendekezo yote ambayo anayaleta hayafanyiwi kazi. Lakini mimi bado narudi kwake, pamoja na kumpongeza na ninakubali anafanya kazi na Kamati yake, lakini kama unalalamika, mapendekezo unayopendekeza hayafanyiwi kazi, wakati huo huo unaiunga mkono Bajeti na unaileta hapa Bungeni, haitusaidii. Tufikie mahali tuboreshe Bajeti, ili itakapokuja kweli ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha Bajeti katika awamu iliyopita, Bajeti ya mwaka 2012/2013 haikufanya kazi; na sasa hivi tunaletewa Bajeti ambayo, inaonyesha mwanzo kabisa kwamba haitafanikiwa, kwa sababu tunaweka Bajeti kubwa ambayo pesa hatuna. Tunategemea kwamba tutapata. Wakati huo huo tunategemea kwa vyanzo ambavyo mimi naamini kabisa havitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha sasa hivi kwa Watanzania ni magumu sana. Uvutaji wa sigara umepungua, wanywaji wa bia wamepungua, hakuna fedha ya *luxury* ambayo mtu anaweza kwenda akakaa mahali akastarehe. Tunategemea kupata kodi kwenye bidhaa ambazo watu wanazitumia kwa starehe na starehe zenyewe wamezipunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina *night club* Iringa, biashara ni mbaya kweli kweli! Hakuna hela ya *luxury* watu kwenda kutumia kwa starehe. Hata madereva *taxi* wenyewe wanalia, wanalala tu pale *club* nje na magari yao, hakuna watu. Leo tunategemea sigara na bia, *juice* na soda; kila bajeti tunategemea hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa na utajiri wa kuzungumzwa tu. Tuna maliasili nyingi, nchi yetu ina madini ya kila aina, lakini tunashindwa kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha kutokana na utajiri tulionao, tunategemea kuwakamua wananchi tu sasa washindwe hata kutoka nje wakaenda kwenye *bar* wakastarehe ama washindwe hata kufanya sherehe ndogo ndogo tu kwa familia zao. Maisha yanazidi kuwa magumu na rasimali tumezikalia hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi nasikitika sana! Serikali yetu hii inaonyesha kwamba hatupendi sana kujituma kufanya kazi, matokeo yake tunataka kazi tufanyiwe tuletewe faida ndipo tuendeshe Taifa letu. Inatakiwa sasa tubadilike! Haya madini ambayo tunayalilia kila siku, ni kweli, mtanijibu kwamba tumebanwa na mikataba, tulishasaini mikataba, hatuwezi kuibadilisha kwa sasa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ni kweli hatuwezi leo kukiuka mikataba ambayo tayari tulishaingia, lakini nchi yetu ina madini bado kila sehemu; kwa nini haya maeneo tuliyobinafsisha ambayo tumewapa wawekezaji tuyaache yafanye kazi hizo kwa utaratibu huo; lakini sehemu nyingine ambazo wawekezaji hawajafika, tuzishike wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukijisifu kwamba nchi yetu inakopesheka, sawa, basi tukope hiyo mitambo mikubwa, tuchimbe wenyewe madini, tuajiri watu badala ya kuleta wawekezaji waje wachimbe madini yetu ambayo siku zote wanatuambia kwamba hawapati faida. Kwa nini hatupendi kujipa kazi wenyewe tukajiwajibisha ili tupate pesa kwa nguvu zetu na jasho letu sisi wenyewe kwa kufanya kazi, wakati tulalamika nchi yetu ni maskini, ajira hazitoshi? Ajira zipo hatutaki kuzitengeneza; tunategemea kutengenezewa ajira. Hii haitawezekana!

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wa nchi hii hatuwezi kuutoa kwa kutegemea wageni, na kwa vyovyote vile hawatakuwa na nia njema kuhakikisha wanatutajirisha sisi ili tuweze kufanikisha bajeti zetu. Siku zote watatukwamisha ili tuendelee kuwa masikini, tuendelee kuwaomba. Inatia mashaka sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini wakati mwingine, nafikia mahali najiaminisha nikiangalia matukio mbalimbali ambayo yamekuwa yakifanyika hasa wakati wa chaguzi mbalimbali, matendo ambayo yanafanyika katika nchi hii kuwapawapa vijisenti watu wakati wa chaguzi, naona kama unatengenezwa huu umasikini ili Watanzania waendelee kuwa masikini, waendelee kuwa ni watu wa kuombaomba, watu wa kusikitika, wasio na uwezo kwa kuhofia kwamba wakiwa na uwezo hawatahongoeka na mtatolewa madarakani. Inatia mashaka!

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa tunatengenezewa umasikini katika nchi hii wakati nchi ina mali chungu nzima! Sina matatizo sana na Mawaziri wa Fedha waliopo sasa hivi, na kwa kifupi hata katika hotuba yao wamejitahidi kwani inaonyesha bado wana nia njema ya kutaka kupambana na hali hii ngumu. Lakini ukweli ni kwamba kwa staili hii ya kutegemea bia, sigara na soda hatutafika!

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa tubadilike, tuangalie ni namna gani tuushike uchumi wetu kwa kuutengeneza sisi wenyewe, siyo kwa kuwategemea wafadhili au wawekezaji. Hili ndiyo suala ambalo tunatakiwa tuumize vichwa na tufanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Spika, aliunda Kamati ya Bajeti baada ya malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba tunapitisha bajeti ambazo hazitekelezeki.

Kwa hiyo, tukaona ni vizuri tukawa na Kamati ambayo itafanya kazi kwa kina kuangalia ni matatizo gani ambayo yanakwamisha bajeti, ambayo yanatufanya sisi uchumi wetu unazidi kuwa chini, ambayo inawafanya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa kila siku wanalalamika hapa! Ikaonekana ni bora iundwe Kamati ya Bajeti ili iweze kufanyia kazi kwa sera ya bajeti kuhakikisha kwamba bajeti yetu inavyopangwa iweze kutekelezeka. Lakini wanatoa ushauri mzuri, hawasilizwi, haiheshimiki ni kuumizana vichwa tu! Hii haiwezekani! Hapo sisi tukisema, mnasema ooh, tunawaponda. Hatuna sababu ya kuwaponda, ninyi ni viongozi wetu na ninyi ndiyo mmeshika Serikali, hilo lazima liheshimike, lakini tunataka mwajibike!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka kusikilia kila siku umasikini, umasikini; tunajisifu habari ya kukopa, kukopa, kukopa! Kukopa siyo sifa! Ingawa kuna Mbunge mmoja anasema eti pesa ya kukopa ni nzuri zaidi. Pesa ya kukopa haina heshima! Pesa ya kukopa haisitiri mambo mengine! Wengine hatukuzoea kutamka maneno yasiyopendeza. (Kicheko)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba pesa ya kukopa haina heshima! Lakini pia bila kukopa hatuwezi kuendelea! Tukope ili tuweze kufanikiwa, tukope ili tuanzishe viwanda! Tukianzisha viwanda hata kilio cha ajira kitakwisha! Wananchi vijijini wana hali ngumu sana, maisha ni magumu, lakini sisi kila siku tunasema pato la Taifa linakua; linakua kwa nani? Mtanzania wa kawaida hatuelewi, anatuona sisi ni wendawazimu tu! Haelewi kabisa, kwa sababu akilinganisha tulipotoka na tunakokwenda anaona kila kunapokucha ni ukali tu wa maisha! Watu sasa hivi wana maisha magumu, ukienda vijijini unaogopa! Majimbo yanatisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya ziara Ismani, wananchi wa Ismani wanalia sana. Wamenituma kabisa, wanajua hawatetewi, hawana mtetezi hapa! Wanasema kwamba niwaambie Serikali waangalie, wamechoka hata kupewa misaada ya mahindi wakati wa njaa! Wanachotaka na wenyewe waboreshewe maisha yao. Tatizo la maji ni kubwa sana katika Jimbo la Ismani. Tatizo la maji ni kubwa sana Ismani! *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnacheka, lakini mkienda Jimbo la Ismani mkalitambelea, mtaniunga mkono. Ni Jimbo kavu, ni Jimbo lenye shida, Jimbo lenye taabu! Maji ya shida, sehemu ya umeme hakuna, umeme upo pale pale Mteru! Wananchi wa Ismani wanalia. Tunajisifu kukopa, basi tukope tuwaendeleze wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ismani pamoja na kwamba tuliahidiwa kwamba pameboreshwa; nikisema Ismani, najibiwa kama mzaha hapa kwa sababu Mbunge anayehusika na Ismani ni Waziri. Lakini tuache mambo hayo, mimi ninavyoongea sina ugomvi na mtu, nazungumza kwa nia njema kama Mbunge wa Mkoa wa Iringa ambaye nimeamua kuwasaidia watu wa Ismani. Sina ugomvi kabisa na Mheshimiwa Waziri! Lakini ninachotaka mimi ni wananchi wa Ismani wapate unafuu wa maisha na wao waone raha ya nchi yao, wapate maji na wao kwa raha, na wao waishi kama watu ambao wana thamani. Watu wa Ismani wametupwa na Serikali, wamesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali pamoja na mambo mengi inayofanya, lakini kwa Ismani hainufaiki kwa kweli! Hainufaiki kabisa Ismani! Ismani imepata bahati sana ya kuwa na Mbunge wa muda mrefu sana, lakini ukweli ni kwamba katika Jimbo; Majimbo ya Iringa yote ukiyatembelea, hakuna Jimbo ambalo huwa linanitua uchungu na kunisononesha kama Jimbo la Ismani. Ni Jimbo ambalo kutokana na bahati waliyoipata kuwa na Mbunge ambaye ameshika madaraka muda mrefu, amekuwa Waziri wa Wizara mbalimbali, ni Jimbo ambalo lingekuwa ni la mfano katika Mkoa wa Iringa!

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkuya, mama yangu, naomba kila kitakachopangwa kwa Jimbo la Ismani kipewe kipaumbele.

MJUMBE FULANI: *Declare interest!*

MHE. CHIKU A. ABWAO: Liwekewe kipaumbele ili wananchi wale na wao wale matunda ya uhuru wa nchi yao!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naipongeza Serikali kwa jinsi walivyojitahidi kutengeneza barabara, lakini bahati mbaya barabara zetu pamoja na gharama kubwa tunayoitumia zinachakaa haraka sana kwa magari mazito ya mizigo. Mimi nafikiri, badala ya kuendelea kutengeneza barabara, tungeshika luku kwanza hapo, tutengeneze reli ili mizigo mikubwa yote ipite kwenye reli. Haya magari makubwa yanayoleta mizigo yanatuharibia sana barabara. Hata ukipita hapa, kwa mfano, unakwenda Mwanza, angalia malori yanavyopita,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

magari makubwa ya mizigo mazito, yaani unaona kabisa barabara zinaelemewa, kwenye lami nyingine mpaka zinatitia.

Kwa hiyo, tusimamisha kwanza suala la barabara ili barabara zetu hizi zinazotengenezwa ziweze kudumu muda mrefu. Pesa nyingi za bajeti zinatengwa kwenye barabara! Mnajitahidi, lakini sasa barabara inatengenezwa lakini haidumu.

Kwa hiyo, tunakuwa tunazidi kuharibu rasimali zetu wakati tungeweza kuboresha reli, mizigo mingi ikapita kwa njia ya reli, barabara zikaendelea kudumu kwa muda mrefu ili zile zinazoongezeka zionekane. Lakini siku zote tunakwenda mbele, tunarudi nyuma, kwa sababu unatengeneza kilomita kadhaa, unarudi tena kurekebisha matatizo ya barabara nyingine zilizokwishaharibika. Kwa hiyo, inakuwa ni kupoteza pesa, pamoja na kwamba nia siyo kupoteza pesa, nia ni kujenga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tumechoka kuwa masikini! Kwa kweli, kama Serikali haiwezi kuwa na mikakati mizuri ya kujenga na kuhakikisha inadumisha kile kinachofanyika, tutaendelea kulalamika siku zote, na malalamishi hayataatusaidia. Tunataka tuboreshe uchumi wetu kwa kuonekana kwa macho, siyo kwa kuonekana kwa kusoma kwenye vitabu. Leo Watanzania wako hoi, hoi, hoi, lakini watu mnafanya kazi usiku na mchana. Lakini mtu hawezi kusema kwamba inafanyika kazi hapa kwa sababu hakuna tija ambayo inaonekana wazi. Tunapata shida sasa hivi; vijana wanahangaika, hawana pa kushika..

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza hapa juu ya vijana Wamachinga; kila tunapojaribu kuzungumza kwamba Serikali iangalie utaratibu gani itawasaidia hawa Wamachinga ili waweze kufanya kazi zao, hawa vijana ni watu wa kuchumia tumbo tu; anatafuta hela leo, anakula kesho; au pengine anakula siku hiyo, kesho anaamka hana kitu. Lakini bado hatuwawekei mazingira mazuri, imekuwa tunawafukuza fukuza tu, wamekuwa kama yatima katika nchi yao, kitu ambacho siyo kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunataka Mji uwe msafi, lakini hivi uchafu ni watu? Kwa nini tusiwawekee mazingira mazuri basi wakafanya hata biashara za usiku, za jioni kwenye maeneo ambayo wanaamini wao watafanya biashara? Siku za Jumapili au na Jumamosi wafanye biashara. Nao wakijua kwamba wamewekewa utaratibu mzuri hatutagombana nao! Watakuwa wana imani kwamba sasa hivi nipo likizo, acha wengine wafanye biashara zao, jioni na sisi tufanye biashara zetu, tukimaliza wafanye usafi, nchi yetu inasonga mbele.

MJUMBE FULANI: Muda, muda!

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. Naomba niliyoyasema yazingatiwe!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba kama Mbunge anachangia, tumpe tu nafasi yake.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ahmed Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nikupongeze wewe binafsi kwa utendaji wako mzuri sana wa kuliendesha Bunge letu Tukufu. Vilevile, nimpongeze mama yetu Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake na wote ambao

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wako chini ya Taasisi yake kwa hotuba nzuri kabisa. Mimi sitaki kulaumu sana, lakini nataka kuboresha na kutoa mapendekezo.

Kwanza ni lazima ni-*declare interest* kwamba mimi ni mfanyabiashara na vilevile ni mfanyabiashara wa magari na nina uzoefu na mambo ya magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nianze katika hotuba yake pale kwenye magari kwamba gari lolote litakalopita miaka nane ni lazima liwe na ushuru wa nyongeza wa asilimia 25.

Mimi nafikiri hiyo siyo sahihi na wala siyo sawa, wengi wa Watanzania uwezo wao; ukiona gari *new model* Tanzania, ukiambiwa hapa pana *Harrier new model*, ukiambiwa hapa pana gani yoyote *new model*, ujue tayari imeshapita miaka tisa mpaka kumi. Ndiyo *new model* kwa Watanzania kulingana na uwezo wa wananchi wetu wa Tanzania. Sasa utakapomwambia mtu kwamba gari hili likiwa chakavu zaidi ndiyo alipe ushuru zaidi, mimi sioni mantiki yake hapo. (Makofi)

Mimi nafikiri uchakavu wa gari hauji kutokana na miaka mingapi ya gari, unakuja kutokana na kwamba limetumika muda gani. Kwa sababu ni sawasawa na gari la Mbunge au Waziri. Gari la Mbunge litakwenda Jimboni kwake, labda litarudi mahali pake. Gari la Waziri litatembea Tanzania nzima.

Kwa hiyo, gari ya Waziri inaweza ikawa mwaka mmoja ni sawasawa na limefanya kazi miaka kumi. Sasa huu uchakavu unakujaje? Au tunataka tuwe watu tu wa kiwango cha juu, tunataka magari *latest*? Lakini hatuwezi kuzungumzia kwamba eti uchakavu ni miaka nane. Gari linaweza kuwa ni la miaka nane lakini wakati mwingine ina kilomita 20,000, bado mpya!

Kwa hiyo, nafikiri kuwe na haja tu ya kuangalia. Kama wanataka uchakavu, basi waangalie hili gari limetumika kiasi gani? Hata gari likiwa limetumika mwaka mmoja, kama limekwenda kilomita nyingi, nalo halifai, maana yake litaharibu mazingira. Lakini siyo kusema kwamba eti gari lina miaka nane ndiyo limechakaa, gari lenye miaka mitatu halijachakaa. Hii siyo kweli! Hii sikubaliani nayo kabisa! Tuangalie limetumika muda gani? Ndiyo uchakavu wake!

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, inaonekana tunawapenda sana Watanzania. Kama tunawapenda Watanzania walete magari mapya, basi tushushe kodi kwenye magari mapya ili walete magari mapya. Mwone hapa! Watu wataingiza magari mapya. Badala ya kuongezea kule asilimia 25 kwenye magari chakavu, basi tutoe asilimia fulani kwenye magari mpaya ili watu walete magari mapya! Lakini siyo kwamba eti gari likiwa chakavu zaidi na ushuru unakuwa mkubwa zaidi. Hii mimi sikubaliani nayo kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kodi zinazotowza kwenye simu, ni asilimia 17. Ukiangalia katika Jumuiya ya *East Africa Kenya* ndio wanatoza zaidi, ni asilimia 12, sisi tupo asilimia 17. Kwa kweli asilimia 17 kwa mwananchi wa kawaida ni asilimia kubwa sana! Kwa hiyo, ni lazima tuangalie hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa hapa pana *REA*, pana maji, *education* na pana vitu vingi, lakini tuangalie hiyo! Tunaweza tukatafuta mbinu za aina nyingine mbadala; na hata wenzetu wa Upinzani, mama yangu hapa aliyemaliza kuzungumza, kalalamika sana, kasema hii bajeti ni ya *juice*, sigara na pombe. Itaendelea kuwa hivyo hivyo kama tunakuwa walalamikaji halafu hatutoi *plan*, au ikija *plan*, ndiyo wa kwanza tunakwenda tena tunapiga kelele kwenye majukwaa kwamba wananchi mnaonewa! Hapana wananchi kuonewa, tutoe *plan*. Kama wenzetu wakileta, hivi sisi tuweke iwe vipi? (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba badala ya kwenye *excise duty* ina maana inamgusa kila mtu anayetumia simu. Tuweke kwamba watakaokuwa wanaongea na simu labda kwa mwezi anayepita Sh. 50,000/= basi yeye achajiwe kodi fulani maana yake huyo tayari ni tajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu anatumia simu mpaka Sh. 500,000/= au Sh. 600,000/= eti unamtetea asichajiwe Sh. 2,000/=. Hivi kweli kwa akili ya kawaida inakuja hiyo? Mtu anaongea kwa Sh. 2,000,000/=. unakataa asichajiwe kodi, haiwezekani kitu kama hicho! Ndiyo maana nasema, tusiendeshe Bunge kisiasa, tuendeshe kiuchumi zaidi, kwani uchumi wa nchi unaendeshwa kitaalamu zaidi kuliko kisiasa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri tuangalie kodi mpya, yeyote atakayefika kiwango fulani labda kuanzia Sh. 60,000/= kwenda mbele huko achajiwe kodi Fulani, na hawa watu wa chini *excise duty* ishuke na vitu vingine vyote vishuke. *Excise duty* ni karibia asilimia 12, zishuke! Lakini kwa wale wanaotumia zaidi, wachajiwe zaidi ili kuangalia watu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi Pikipiki. Hizi pikipiki ukiangali hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zimebadilishwa usajili. Sasa badala ya namba za gari kuanzia T zitaanzia TZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni sababu, kama ni kwa ajili ya kuondoa uhalifu na watu kubadilisha namba kwenda kwenye magari sasa turudie ule mfumo wetu wa zamani. Tusitumie TZ tena kwa sababu TZ haijulikani ikiwa Kongwa, Gairo, Kahama au Zanzibar inajulikana tu ni ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tutumie namba zetu za zamani zile zile! Kama gari ni ya Morogoro, isajiliwe kwa namba ya MG; kama ni gari ya Dodoma isajiliwe kwa namba ya DO, kama ni Dar es Salaam ni DSM, kama zamani vilevile. Turudishe namba zile zile za Mkoa! Kila pikipiki isajiliwe kwa kutumia namba ya Mkoa, tuache kabisa hii habari ya kutumia TZ, kwa sababu TZ utaanzia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pikipiki zinaingia kila siku! Kwa hiyo, hata namba, hata kama mtu akifanya makosa, zile tarakimu zitakuwa nyingi hata kusoma atashindwa. Maana uanze moja mpaka utafika 300000! Hicho kibao chenyewe cha pikipiki hakitaenea hizo namba. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, tutumie namba za Mkoa. Kila Mkoa uwe na namba yake kama zamani! Tabora walikuwa wanatumia UJ, maana yake Ujiji.

MJUMBE FULANI: Tabora ni TB bwana! Hiyo ni Kigoma!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Kigoma ni UJ. Halafu kuna hili hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nia nzuri ya Wizara ya Fedha ni ni kuongeza nidhamu katika kifungu cha 30 ukurasa wa 13 na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema, mtaipa Mamlaka ya Mapato kila siku moto, kila siku mtailazimisha ikusanye na kila siku mtalazimisha wakusanye hata kupita kiwango cha wafanyabiashara, kiasi kwamba hawa wafanyabiashara wadogo na wakubwa wataashindwa kufanya biashara na wote watakuwa wachuuzi, watakuwa Wamachinga. Sasa sijui hiyo kodi mtapata wapi? Ndiyo maana yake! Kwa sababu hamwanganalii kwamba hizi fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zinazokusanywa zinakwenda wapi? Maana yake TRA ni sawasawa na bomba la maji la inchi mbili halafu matumizi ni bomba la maji la inchi 10. Huo ndiyo ukweli wa hali halisi.

Sasa hii mtahangaika tu! Maana yake kila watakapozidi kukusanya na ndiyo zinavyozidi kuliwa, kila siku! Kwa mfano, Halmashauri, lile ni bomba ambalo halina mwisho. Wanakula fedha zote zinakwisha, matokeo yake hayaonekani, mna kazi ya kulalamika tu hapa kwamba hatupati fedha! Hicho kidogo chenyewe kiko wapi? Kinatumka vipi hicho kidogo? nani anasimamia hizo fedha? *(Makofi)*

Nchi hii mimi ninaonea huruma sana kwa kweli, kama pangekuwa na adhabu ya kunyongana kama alivyosema Mheshimiwa Keissy hapa ni bora tu watu wanyongane tu hapa. Mimi naona ingekuwa sahihi kabisa tuwe kama China, maana mnawapa watu mizigo tu. Hizo zinazokusanywa ziko wapi? Ukienda Halmashauri, kila mwaka barabara hiyo hiyo inatengenezwa, kila mwaka zanahati hiyo hiyo na kila mwaka kwenye bajeti ipo hiyo hiyo inahitaji fedha. Hazitosheki hata tuwe na bajeti hapa ya shilingi bilioni 40, matumizi nayo huko kwenye Halmashauri na sehemu zingine yanaongezeka. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa mimi sioni sababu ya kuanza kwanza kutafuta mambo mengi kama tunashindwa kudhibiti matumizi yetu. Matumizi ni makubwa mno na sasa hivi kila mtu anaangalia tumbo lake tu, anakwenda huku na kule. Mtazidi kuwasukuma hawa TRA na TRA watazidi kuwasukuma wafanyabiashara, wafanyabiashara watatoka kwenye mstari watakuwa Wamachinga wote, sasa sijui na wamachinga nao mtapataje kodi kutoka kwao? Mwisho hata hicho kiwango mnachokita kitakuwa hakipo. Tudhibiti matumizi yetu kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mambo mengi sana. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo. Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ninachangia leo ni kuwashangaa Wabunge ambao kila mwaka kazi yao ni kulalamika. Mimi huwa ninashangaa sana, kwa sababu sisi tulioko huku ndani ni Viongozi. Kiongozi ni mtu ambaye si mlalamikaji bali anatatua matatizo. *(Makofi)*

Sasa hapa ndani kuna watu walilalamika mwaka jana, Kamati ya Bajeti na wengine, wakalalamika kwamba, inatakiwa Sheria ya Bajeti itungwe. Mnataka nani awatungie kama ninyi Wabunge mnajua kazi yenu, yaani ni shida sana ku-*deal* na watu wengi ambao kazi yao ni kulalamika! *(Kicheko)*

Wewe kazi yako kama Mbunge ni kutunga sheria. Kama mwaka jana uliwashauri Serikali kwamba, tutunge Sheria ya Bajeti hawajaleta, kwa nini mwaka huu usitunge? Kama unafanya kazi yako ya Kibunge na unafikiria sawasawa kwa nini mwaka huu usiseme tutunge hiyo sharia unalalamika tena? Mwaka juzi ulilalamika na mwaka huu unalalamika; hivi kweli tumetumwa kuja kulalamika hapa? *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Yuko Mbunge anasema mbona hujaleta wewe? *(Kicheko)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Tumeleta Miswada, kuna Kamati ya Bajeti wanakaa huko wanakula shilingi 500,000 kila siku, hakuna kazi ambayo wanafanya. *(Kicheko)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa hapa, hii Kamati nayo lazima tuitazame sana. Hii Kamati inaita mashirika hapa, inajifanya eti inawauliza watalipa kodi shilingi ngapi; wao wanajua ku-*calculate* mambo ya kodi hapa? Kutudanganya, kula fedha bure, hakuna kazi hiyo Kamati inafanya hata sasa hivi wanatupotezea muda. Watu wameshawasilisha taarifa hapa, sasa hivi wako kwenye kikao wanafanya kitu gani? Ni kutafuta namna ya kula shilingi 500,000 kwa siku, wakitoka humu wanaenda kula shilingi 500,000 kule, hakuna kazi wanayofanya huko. Tofauti na malalamiko waliyoyaleta hapa mwaka jana na mwaka huu wameleta malalamiko, hakuna kitu kipya kwenye ile Kamati. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kitu na hata ukasirike sijui usemeje, ndiyo hali halisi. TANAPA wako pale wanajadiliana nao kodi, wale wanajadiliana nao nini? Ni kutengeneza mianya ya rushwa. Wanaita mashirika eti wana-*bargain* nayo, utalipa hivi, sijui nini, hakuna vitu vya namna hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Hili Bunge linasikitisha sana, tunatenga fedha kila mwaka haziendi, *then* tunaongeza bajeti, tunakuja hapa tunaongea, watu wanalalamika, huo siyo Uongozi. Uongozi hapa tungeamua, jamani kwa sababu tumeona hivi tuna- *decide* hivi, siyo kupitisha tena bajeti ambayo ni *unfunded*, huo siyo Uongozi. Wewe unapitisha bajeti, unasifia, hata ukisifia fedha hazipo, hazitoki hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa ni Viongozi gani ambao hawawezi kuonesha njia? Tumewashauri kila siku tukawaambia, watu wamezungumza miaka yote, tumezungumza misamaha ya kodi, tungekuwa tunafanya kazi yetu, tungepitia hapa wala Kamati ya Bajeti isingeleta hayo malalamiko, ingekuwa kutuambia tunapendekeza moja, mbili, tatu, tukaamua misamaha hii tumefuta, maana uwezo tunao. Uwezo tunao sisi unamlalamikia nani? Unasubiri nani afute wakati wewe ndiye Mbunge, tumekuwa hapa tufanye kazi hiyo kwamba, tukiona maeneo ambayo yanapaswa kutozwa kodi tunatoza? Unalalamika, unashangilia badala ya kupunguza ile misamaha ambayo tumeiona. Unalalamika, unapiga makofi, tunapitisha tena hapa. *(Makofi)*

Tumezungumza, hii nchi ni shida sana hasa ninyi mlio wengi, mngekuwa mnaamua, ngoja niwatolee mfano; Nchi ya Ghana hii ni Katiba yao. Mnazungumza kila siku madeni, mapato, wao Serikali ikitaka kukopa nje, hii hapa Katiba, wanaleta Azimio Bungeni linaeleza tunataka tukakope fedha wapi, kiasi gani, kwa masharti gani na kwa sababu ipi. Ninyi ni kusherehekea kakope! Nendeni mkakope, hamjui wanakopa wapi, kwa riba zipi kwa kazi gani; mpo tu mnashangaa shangaa! *(Kicheko)*

Sisi tunawashangaa kwa sababu ninyi Wabunge wa CCM ni wengi na mnashindwa kufanya vitu hivi ambavyo ni vya kutunga sheria hapa hapa. Unatunga tu sheria, hulalamiki. Kiongozi ni mtu unaamua, sasa unalalamika nini? Wenzako wanajiwekea utaratibu, tukiwaambia tubadilishe hivi vitu kwenye Katiba hamtaki. Tunawashangaa sana, sijui ni Viongozi wa namna gani? Ni maajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kwenye hii bajeti, ukurasa wa 62, ukiangalia kwenye mapato ni kwamba, mapato makubwa tunayoyategemea; mikopo ya ndani shilingi trilioni moja, mikopo ya kibiashara, mikopo ya kibajeti, jumla ya mapato ambayo tunayategemea mengi ni mikopo, mikopo, mikopo, karibu shilingi trilioni saba. *Then* matumizi ya hiyo mikopo kulipa madeni. Vyanzo vingi ni kukopa, matumizi yake kulipa madeni, unashangilia, shangilia tu. Nchi hii haiwezi kuendelea! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi; maana ya kuwa na Mihimili mitatu, maana yake ni kwamba, Mhimili mmoja unapo-mess, Mhimili mwingine unaingilia kati. Sasa huu Mhimili

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tumeona kabisa kwamba, wenzetu wame-mess, tumeshauri kodi za majengo (*property tax*) tumeona hawataki, sisi ndiyo tulitakiwa tuingilie kati kutatua hilo tatizo, siyo kuja kulalamika tena hapa, wewe umepewa meno. (*Makofi*)

Haya mambo ya kuendelea Wabunge mnajifanya ni sehemu ya Serikali, tutaendelea kuumiza Wananchi. Tukifanya hivyo msifikirie eti mnakiumiza sijui Chama chenu, ndiyo mtakuwa mnakisaidia Chama chenu, Wananchi watawaona mna akili. (*Kicheko*)

Sasa mnakaa hapa, vitu vya kawaida tumewaambia, Waziri Mkuu alitoa kauli hapa kwamba, ooh tutabadilisha matumizi ya magari na vitu vingine. Tukaona kwamba, kauli zake huwa hazitekelezeki, ni mambo tu ya kupoza poza, vitu gani, ku-*please please*, sijui tuko pamoja na nini. Tungekuja hapa tukatunga tu sheria kwamba, hairuhusiwi Serikali kununua V8, rahisi tu, tunga tu sheria unazuia. Sasa watu wanalalamika ooh, matumizi makubwa, matumizi makubwa, unalalamika nini wakati umepewa meno, umepewa kazi na kila kitu bado hujui kutumia. Sasa hivi tuwasaidie kitu gani, semina mnapewa? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya *Transparency International* imeonesha kwamba, Bunge linaongoza kwa rushwa na rushwa yenyewe ni kwa sababu Wabunge hawafanyi kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, naomba upokee taarifa. Mheshimiwa Rage!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, utazame muda wangu.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia hii Hotuba ya Wapinzani, ukurasa wa 45, wao wamependekeza elimu iwe shilingi trilioni 2.5. Hotuba ya Waziri ni shilingi trilioni 3.5. Sasa tufuate ushauri wao katika hali kama hii jamani?

Hilo tu nilitaka kumfahamisha mdogo wangu. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, unapokea taarifa uendeleo kuchangia dakika zako?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, unajua tunapozungumza haya mambo, kwanza, hizo shilingi trilioni mbili nimezungumza hapa, labda kama hafuatilii au hasikilizi; tumemwambia hizo shilingi trilioni mbili kwanza hazitapatikana, awe anafahamu. Ufahamu kabisa kwamba, tunapitisha kitu hewa, fedha hazitatoka. Walimu wana madeni pale Tabora kwako hawatalipwa, ni lazima ujue hilo. (*Kicheko/Makofi*)

Tunachosema, shilingi trilioni tatu, sisi kama Wapinzani, tunajua kabisa, tuna uhakika fedha zipo, tuna uwezo wa kudhibiti mianya ya rushwa, tuna uwezo wa kukusanya kodi na tuna uwezo wa kupunguza misamaha ya kodi tukafikisha hiyo shilingi trilioni tatu ya elimu. Sasa haya mambo ambayo ninayasema ndiyo Wabunge wa namna hii. (*Kicheko/Makofi*)

Aina ya Wabunge wa namna hii ndiyo ambao wanatufanya nchi yetu isibadilike, kwa sababu nilitegemea atakuwa ameelewa. Ilipaswa aelewe mambo haya, lakini mtu analeta taarifa ambayo, yaani ni mambo ya aibu sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapitisha bajeti Wizara ya Ujenzi ina madeni. Mimi ni Waziri Kivuli wa Ujenzi, unachukua Kitabu cha Hotuba ya Wizara ya Ujenzi, unaandika barabara nyingi sijui kutoka Sumbawanga mpaka wapi itajengwa, unatenga shilingi milioni 700, shilingi bilioni tano, kudanganya danganya Wananchi na Wabunge kwamba, barabara zitajengwa. Nikauliza hapa; Wizara hii kwa mwaka huu inataka kulipa madeni kiasi gani? Hakuna majibu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yaliyotolewa, ni mambo ya ubabaishaji. Sasa kwa kuwa Wabunge tumeona Serikali wanafanya mambo ya ubabaishaji, sisi Wabunge tusiwe wababaishaji, tufanye kazi yetu ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe lile nililoanza nalo, wafuatilie hawa watu wa Kamati ya Bajeti, waache kutupotezea muda kujifanya wanafanya kazi kule wakati hakuna kitu wanachofanya hapa tofauti na kutuletea malalamiko. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Felix Mkosamali, tunakushukuru sana. Alipotutolea Katiba ya Ghana, akasema sijui nani wanakwamisha Katiba; hivi jamani Waheshimiwa akina nani wanakwamisha Katiba Mpya? *(Kicheko)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: CCM!

NAIBU SPIKA: Nani anakwamisha Katiba?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: CCM! *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: UKAWA.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lekule Laizer! Jibu nililolisikia ni UKAWA. *(Kicheko)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: CCM, Katiba ya Wananchi hamuitaki, mnataka Katiba yenu.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Wasira, pamoja na Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri, kwa Hotuba nzuri waliyoitoa ya Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameelezea makusanyo yote ya bajeti na mpaka tumesikia kwamba, ni shilingi trilioni 19.8. Tukikumbuka tulikutoka, mimi nilikuja kwenye Bunge hili makusanyo yakiwa shilingi trilioni 2.5, hivi sasa tumefikia shilingi trilioni 19 na tunakaribia 20. Ningependa kuelezea kwamba, fedha zinazokusanywa siyo chache ni nyingi, tuangalie matumizi ya fedha hizi, kwa sababu hata tukiongeza mapato, tukikusanya zaidi, lakini matumizi yakiwa mabaya bado hali ni mbaya. Mimi nasema matumizi ya fedha katika Serikali hii ni mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha na matatizo yaliyoko vijijini, Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunatofautiana katika Majimbo yetu; kuna wanaotoka mijini ambao barabara zote ni za lami, kila nyumba ina maji, hospitali zipo. Huwezi kulinganisha matatizo ya mjini na matatizo ya Jimbo la Longido au Majimbo yote ya vijijini, ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema Wananchi wachote maji kilomita nne, vijijini bado Wananchi wanachota maji zaidi ya kilomita kumi, bado wanaenda hospitali au zahanati umbali wa kilomita 30 mpaka 40. Naomba Serikali iangalie matumizi, ipunguze OC, kama Waziri Mkuu alivyosema, ipunguze ununuzi wa magari ya kifahari na Viongozi wapunguze ziara za kwenda nje. Serikali itafute shimo ambalo mapato ya Tanzania yanaingia, kuna shimo ambalo halina maana wala faida. Kama ni matumbo ya watu ndiyo yamekuwa shimo tuangalie kwa sababu hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo hayakuguswa kwenye mapato; suala la madini bado ukusanyaji wa mapato ni mdogo. Bado kuna migodi iliyopo kwenye maeneo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Majimbo mengine, ambayo Wananchi hawaoni faida, kwa sababu hawapati hiyo 0.3, ni baadhi ya Wilaya ndiyo wanapata! Sijui ni dhahabu tu, kwa nini Wananchi walioko katika maeneo ya rubi wasipate hiyo 0.3? Kwa nini Halmashauri isipate chochote? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni madeni. Tunachosomewa kila siku hapa ni madeni, kila mara ni madeni, tunasikia madeni na fedha za kulipa madeni. Hivi wakati wa kukopa kwa nini hatuambiwi kwamba, leo Serikali inakopa kiasi fulani, tujadili mkopo huo kuona, kama inawezekana, kama tunakubaliana au hatukubaliani nao. Hivi ni Kamati ipi katika Kamati zetu wanajadili mkopo unaokopwa na Serikali? Ni kwamba, Waziri tu anamka anakwenda kukopa au ni nani anayehusika katika utaratibu huu wa kukopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inatumizwa. Wakati mwingine kwa nini tunaletewa tupitishwe bei ya vitu vidogo vidogo wakati mabilioni ya mikopo yanayokopwa hatuletewi tujadili? Naomba na hilo tuangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchumi. Kukua kwa uchumi isionekane na wataalam, isiwe iko kwenye maandishi, ionekane kukua kwa uchumi mpaka vijijini. Wananchi waone kwamba hali ya uchumi imeboreka, kama Wananchi hawaoni kwamba uchumi umekua, kwa kweli itakuwa ni Wataalam tu ndiyo wanaoona kwamba uchumi umekua lakini vijijini hali bado ni mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la viwanda kwa ajili ya mifugo. Jimbo langu ni la wafugaji, tuna mifugo, lakini kinachonishangaza ni mifugo ya Tanzania kuboresha mapato ya Kenya, lakini haiboreshi, haipo katika bajeti hii tunayoizungumzia. Wakenya ndiyo wanafaidika na mifugo ya Tanzania, kwa sababu wao ndiyo wana viwanda sisi hatuna, wao ndiyo wana masoko. Kila wakati nalalamika kwamba, tunahitaji soko pale Longido kwa sababu ni mpakani ili Wakenya waje kununua mifugo Longido. Inapitishwa kwenye kila Bajeti, lakini tunaambiwa kwamba ni Hazina ndiyo hawatoi fedha. Hivi ni kwa nini? Kwa nini Wakenya wawe na masoko kila siku? Ng'ombe kutoka Tarime, Serengeti, Loliondo, Ngorongoro mpaka Kilimanjaro wote soko ni Kenya. Hivi jamani hamwoni kwamba tunapoteza mapato?

Jimboni kwangu wameboresha mifugo kweli. Kenya wanasema kwenye Halmashauri zao msuzuie ng'ombe wa Longido kuja Kenya kwa sababu ndiyo wanawalisha. Sisi ndiyo tunawalisha Wakenya, kwa sababu hatuna mahali pa kupeleka ng'ombe; kwa nini kiwanda kikubwa kisijengwa pale Arusha? (Makofi)

Mheshimiwa Rais alisema viwanda vitajengwa katika mikoa yote ya wafugaji, lakini hakuna kiwanda hata kimoja kilichojengwa. Hivi viwanda si ndiyo vyanzo vya mapato, viwanda si ndiyo ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mipango. Mipango yetu ni mizuri kweli, tunaweka na vipaumbele, lakini isije ikawa kila mwaka maji ndiyo kipaumbele, kilimo ndiyo kipaumbele, utekelezaji tukitekeleza yale tuliyopanga kwenye vipaumbele vyetu, hayo mengine ndiyo yatakuwa kipaumbele, hayo yatakuwa yamemaliza haya. Ni aibu kila siku suala moja kwenye bajeti kila wakati ndiyo kipaumbele tunachozungumzia. Suala lingine ambalo naona ni hatari ni kushuka kwa thamani ya fedha zetu. Fedha zetu thamani yake ni ndogo kwa kweli bei ya vitu itapanda kila wakati. Naomba Serikali iliangalie jambo hili kwa sababu nalo ni jambo la hatari, ambalo linaweza kila wakati likaleta mfumko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukosefu wa kazi. Watu wengi wamelalamika. Jamani, ukiangalia vijijini, vijana wetu wakimaliza elimu ya vyuo vikuu wanarudi vijijini na wengine wanakwenda kujaribu kufanya biashara ambayo haistahili. Siyo vizuri kuwakuta vijana

Nakala ya Mtandao (Online Document)

waliomaliza vyuo vikuu ndiyo wanachunga ng'ombe, hata wengine ambao hawakusoma wataona ni afadhali wao ambao hawakwenda shule. Ni aibu vijana kumaliza elimu wakakosa ajira wakaenda. Siyo kila mtu anaweza kujijiri. Ndugu zangu kwa sababu kujijiri ni lazima uwe na kipato, uwe na kianzio, sasa utanzia wapi? Mwanafunzi aliyemaliza Chuo Kikuu unamwambia ajijiri atajijiri kwa njia gani? (Makofi)

Naomba suala hili la ajira tulitazame kwa sababu bado ni tatizo kubwa na nadhani kule vijijini ndiyo hakuna kazi. Walioko mijini wanaweza kubangaiza tu wakapata vibarua vya kufanya. Msomi aliyetokea kijijini kwa sababu hajui sehemu nyingine anakujua tu kule kwao na chuo alichosomea, akimaliza anarudi kijijini. Naomba Serikali ianze sasa kutafuta ajira kwa vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna maeneo mengine ambayo Serikali haijatangaza ajira; kuna vijiji vingi sana havina hata Watendaji. Halmashauri zetu kila mwaka tunapata Hati Chafu kwa sababu hatuna Watendaji. Serikali haijatangaza nafasi za Watendaji, kila mwaka inasema waraka utatoka, waraka utatoka; nini kinazuia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niseme hayo machache. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido. Sasa ni Mheshimiwa Grace Kiwelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi!

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kwenye Hotuba hizi mbili zilizowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa kusoma Hotuba yake vizuri, lakini kusoma ni suala moja na utekelezaji ni suala lingine. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake, yako mambo mazuri katika Hotuba yako, tunaomba myafanyie kazi na myasimamie pamoja na vijana uliopewa pamoja na shemeji yangu Mwigulu hapa. (Makofi)

Nazipongeza pia Hotuba zilizotoka za Kambi ya Upinzani, zina mambo mazuri, mkiyafanyia kazi tutaweza kulijenga Taifa letu vizuri. Sisi wote ni Watanzania, mawazo yanahitajika na ndiyo maana tuko hapa. Napongeza maoni ya Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, pamoja na mdogo wangu kusema hakuna wandolifanya, lakini nimeona yapo mambo mazuri, wametoa vyanzo vya mapato vipya, ambavyo ninaamini mkivisimamia vizuri, tutaachana na bajeti ya Fanta, Safari Lager na Sigara Nyota. Kwa hiyo, ninaamini mkifuata yale waliyoyasema na yale Wabunge tuliyoendelea kushauri kuanzia miaka ya nyuma, tutaweza kukuza uchumi wetu vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, Wabunge wenzangu wamesema, hali ya uchumi inaonesha imekua kwa asilimia saba, lakini tunakotoka hali si hivyo. Maisha ya Wananchi kule vijijini ni magumu, Wananchi wana matatizo, hawana maji, yako baadhi ya maeneo wanayo, lakini kuna maeneo mengine hakuna maji kabisa, hawana umeme. Tukikaa hapa kupiga makofi tukisema hali ya uchumi imekua, tutakuwa tunajidanganya sisi wakati wapiga kura wetu kule hali si hivyo. Uchumi umekua kwa baadhi ya watu, lakini wale wa kima cha chini walioko kule vijijini hali zao siyo nzuri. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tuangalie wale Wananchi walioko kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependa kuzungumzia suala la kilimo. Asilimia 80 ya Wananchi wa nchi hii wanajihusisha na kilimo, lakini wengi wako vijijini na wengi ndiyo hao

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tunaoambiwa ni maskini. Kama tunataka kupunguza umaskini wa nchi hii ni lazima tuwekeze kwenye kilimo na tuwekeze kule vijijini tuwakopeshe Wananchi wetu matrekta, tuwape pembejeo kwa wakati ili waweze kulima na tutaweza kupunguza tatizo la ajira. Tukiwekeza kule na tukiweza kuwatimiza haya yote Wananchi wa kule vijijini, hata vijana hawatakimbilila mijini. Tupeleke maji, umeme na tuwape zana za kilimo, vijana watabaki kule watalima na tutakuza uchumi wetu. Kwa hiyo, niombe sana Serikali mfanye hivyo ili tuweze kuondoa tatizo la ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu viwanda. Nchi ambayo haina viwanda haiwezi kuendelea. Tukiweza kufufua viwanda, tulikuwa tuna viwanda vingi vimekufa, Mkoa wangu wa Kilimanjaro tulikuwa tuna viwanda vimekufa, leo Mkoa wetu wa Kilimanjaro tumerudi nyuma sana. Kilimanjaro iliyokuwa miaka 50 iliyopita siyo Kilimanjaro ya leo, hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali tufufue viwanda. Tuiwezeshe *SIDO* iweze kufufua viwanda na hivi viwanda vidogo vidogo vitaweza kupokea mazao kutoka kwa wakulima na kukuza thamani ya mazao ya wakulima wetu. Kwa hiyo, niombe Serikali tuangalie suala la viwanda, tuvifungue viwanda vilivyofungwa, tuwekeze kwenye viwanda vidogo vidogo kule vijijini, itakuza pato la Wananchi wetu na pia itapunguza tatizo la ajira ambalo tunalia nalo hapa kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la afya. Wamesema wenzangu, afya ni jambo muhimu sana katika Taifa. Taifa lenye watu ambao hawana afya hawawezi kufanya kazi na uchumi wetu hautaweza kukua kwa watu ambao hawana afya bora. Cha kushangaza, kwenye mabadiliko makubwa sasa Wizara hii haipo. Tunaomba sana, kule vijijini yako maeneo watu hawapati dawa, hospitali zetu hazina vifaa na hakuna watumishi wa kutosha. Sasa ningeiomba Serikali, kama tunataka Taifa letu liwe na watu wenye nguvu, wenye afya, tuwekeze kwenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na afya, iko Miradi mingi ambayo imefunguliwa ya afya. Mkoa wangu wa Kilimanjaro kila nikisimama hapa siachi kuisemea Hospitali yetu ya Mawenzi. Iko wodi ya wazazi inajengwa pale, amesema mama yangu Batenga kutoka Kagera, akina mama tuwaenzi ndiyo wametuzaa wametufikisha hapa wametulea, jengo lina miaka sita sasa halijakamilika.

Tunaomba watu wa Mipango, tupange basi Miradi michache tutekeleze kwa wakati. Kwa sababu tunapanga Mipango mingi mwisho wa siku haitekelezeki, wakandarasi wanatudai, gharama za ujenzi zinazidi kuwa kubwa, Wananchi wanaendelea kulalamika, mwisho wa siku hatuna cha kuonesha. Niishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi, wekeni Miradi michache mtekeleze kwa wakati, Wananchi waone mnachokifanya. Mkikurupuka kuweka Miradi mingi isiyotekelezeka, Wananchi wataendelea kulalamika kwamba hakuna kinachofanyika, kumbe tunatawanyia fedha kwa Miradi mingi kazi haionekani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka kwenye afya, niende kwenye madeni ya wazabuni. Hiki ni kilio kikubwa sana kwa wazabuni wa ndani, wamefanya kazi hii wamekopa Mabenki wamekuwa wakilisha Majeshi yetu, mashuleni yetu, watoto wetu, wafungwa walioko Magerezani na mahabusu, lakini Serikali imeshindwa kuwalipa. Niombe Serikali hebu lipeni madeni ya Watanzania hawa. Wamejifunga mkanda wamekwenda kukopa na wamepunguza pia tatizo la ajira lakini mwisho wa siku hawalipwi. Mabenki hawajali hawajalipwa au hawajafanya nini nyumba zao zinazuzwa wanarudi kwenye umaskini tunawasaidiaje Watanzania hao? Vilevile mtakapokuja kuwalipa mtawalipa kwa riba kwa kuwacheleweshea malipo yao au mtawalipa tu zile fedha walizokuwa wanawadai?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nawaomba muwaangalie sana hawa wazabuni, kwa sababu walifanya kazi hiyo kwa nia njema, tunawaomba msiwarudishe kwenye umaskini, angalieni jinsi ya kuwasaidia na kuwalipa madeni yao ili waweze kuendelea na biashara wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ucheleweshwaji wa fedha kwenye Halmashauri zetu. Tumekuwa tukipitisha fedha nyingi za kwenda kwenye Halmashauri, tunapiga makofi amesema Mheshimiwa Mkosamali, lakini fedha haziendi kwa wakati, Miradi inachelewa. Tuiombe Serikali zile fedha tunazopitisha hapa ziende kwa wakati ile Miradi Wananchi waliyoichagua kule iweze kutekelezeka. Wananchi hawana maji, yako maeneo machache lakini mengi hakuna maji. Kwa hiyo, tunaomba sana fedha zinazopitishwa hapa kwenda kwenye Halmashauri zifike kwa wakati. Tumechoka Wananchi wanalalamika, sisi tukija huku tunalalamika, ndiyo maana nimesema kwamba, kupitisha bajeti hapa ni jambo maoja lakini utekelezaji ni jambo la muhimu sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali mhakikishe fedha zinazopitishwa zinakwenda kwa wakati na zinafanya kazi kwa ile Miradi iliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu kuondoa kodi ya VAT kwenye nyumba zinazojengwa na *National Housing*. Kama dhamira yetu ni ya kweli, tunataka Watanzania waishi kwenye nyumba bora, waondoke kwenye nyumba za tembe na wanufaike na nyumba hizi zinazojengwa na *National Housing* ni vizuri kodi hii ya VAT ikatoka. Watanzania wameshindwa kuona umuhimu wa *National Housing* kwa kujenga nyumba zile kwa sababu ukiweka kodi ya VAT zile nyumba zinakuwa juu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione suala hili lina umuhimu sana, Watanzania tuwatoe kwenye nyumba za tope na tembe na nyasi nao waweze kuishi kwenye nyumba za vigae na bati. Tuondoe kodi hii tuwawezeshe walimu wetu na wakulima ili nao waweze kuishi kwenye nyumba hizi zinazojengwa *National Housing*. Tusiwaachie tu matajiri wachache wakazinunua na kufanya biashara waendeleo kupata wakati Watanzania wengine wanaendelea kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie tatizo la ajira. Jana Wabunge wamesema hapa, liko tatizo kubwa sana la ajira kwa vijana wetu. Wabunge wengine bado tunaendelea kuzaa, watakua, watakuwa vijana, ajira hakuna. Tuiombe Serikali, kuna kila sababu sasa ya kuliangalia tatizo hili kwa jicho la kipekee. Ni bomu linaloweza kulipuka wakati wowote na sisemei kwa kuwa mimi ni Mpinzani, wakati wowote hasa sisi viongozi tunawategemea hawa vijana, tuhakikishe tunawatafutia ajira. Ajira si za kukaa tu maafisini, nimesema mwanzo, tunaweza tukawakopesha vijana hawa matrekta tukahakikisha kule vijijini wanapata maji na umeme, tuwape pembejeo, tuwakopeshe vitu kwa bei rahisi waweze kujijaji wenyewe, waweze kupata kipato chao cha kila siku. Tusipofanya hivyo, si CHADEMA, si CCM tutanusurika na janga hili la hawa vijana. Ni wengi, tusiwasubirie tu wakati wa Uchaguzi kuwatumia, lakini tuhakikishe tunawafanyia mipango mizuri ya wao waweze kupata kipato, tuache kutoa *T-Shirt* na kofia na shilingi 500, 500 kwa vijana hawa, tuwape mtaji wa kutosha wakafanye kazi kwa sababu wanayo nguvu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Grace Kiwelu, nakushukuru kwa mchango wako. Sasa ni Mheshimiwa Khalfan Aeshi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nimuunge mkono Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa yale aliyoyaongelea. La pili, niwapongeze mapacha watatu; yaani Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake. Mimi naamini kabisa kazi mliyoifanya ni nzuri na ninaamini kabisa mwisho wake utakuwa mzuri. Endeleeni kuwa wamoja, dumisheni upacha huo ili tuweze kusonga mbele.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi narudia pale alipoachia Mheshimiwa Grace Kiwelu, hawa wazabuni, tumekuwa na kero kubwa sana. Mimi naomba ni-*declare interest* kwamba na mimi ni mfanyabiashara na msafirishaji. Wanasumbawanga hususan Wanarukwa wamefilisika, pamoja na Tabora kwa Mheshimiwa Rage. Wamefilisika kwa sababu, mlitupa kazi mwaka jana ya kusafirisha mahindi ya NFRA, lakini leo kila nikimfuata Waziri wa Kilimo, ananiambia nenda kwa Waziri wa Fedha. Nikienda kwa Waziri wa Fedha ananiambia fedha hakuna. (Makofi)

Sasa ukiangalia wako wafanyabiashara wadogo wadogo mmojawapo nitamtolea mfano anaitwa Sultani. Yule amekopa benki, baada ya kukopa benki ameenda kununua magari. Amenunua magari yale ameenda kusafirisha mahindi yale kwa mkopo. Leo hii mwezi wa 12 watu hawajalipwa; sasa hii Serikali kweli ina lengo zuri na hawa watu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilisema hili nilifikishe leo na nitaliongelea kwa uchungu mkubwa sana; haiwezekani mkatupa kazi ndani ya miezi 12 msimlipo mfanyabiashara, mnamuumiza, mnamuua kabisa. Leo hii mfanyabiashara huyo niliyemtaja amekimbia mji, yuko Dar es Salaam kwa madeni; mafuta wanamdai, siji vibarua wanamdai, madereva wanamdai na benki inamdai! Hivi kweli tuna lengo zuri hili la kuwasaidia Wananchi hawa. (Makofi)

Sasa nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu wewe umekuwa kama jalala, kila mtu anaambiwa nenda kwa Waziri wa Fedha. Ninaomba utuhakikishie ni lini hawa watu waliosafirisha mahindi haya watalipwa fedha? Cha kusikitisha zaidi na tender ambayo mlikuwa mnawapa wafanyabiashara wa Mkoa wa Rukwa leo mmewanyang'anya mmerudisha Makao Makuu. Sasa hii jamani ni haki kweli? Watu wanalalamika hapa ajira hakuna, watu wamejiajiri wenyewe na matokeo yake mmewadhulumu. Leo hii riba ya miezi kumi na mbili ni kiasi gani; ni pesa nyingi sana.

Ninaungana na Mheshimiwa Grace Kiwelu; kama kweli Serikali mnakubali hili, basi muwalipe madeni hawa. Yalipeni madeni haya ili hawa watu wawe salama, otherwise, hili ni tatizo kubwa. Nami nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, siwezi kurudi Jimboni kwangu kama hujawalipa madeni hawa wafanyabiashara wetu. Nakuomba sana, chonde chonde. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, madeni hayohayo leo hii wazabuni wakubwa wanaosambaza pembejeo ndani ya Mkoa wa Rukwa na Katavi na Mikoa mingine, hawajalipwa mpaka leo na msimu mpya unaanza. Sasa tunakwenda kwenye msimu mpya msimu za wazamani hawajalipwa; hizo pembejeo zitafikaje kwa wakulima?

Kwa hiyo, kuna vitu inabidi uviangalie sana Mheshimiwa Waziri. Ukienda kwa Waziri wa Kilimo anasema Waziri wa Fedha, ukienda kwa Waziri wa Fedha anakurudisha kwa Waziri wa Kilimo, mara Waziri wa Kilimo hajakamilisha hesabu; sasa jamani, basi tulipeni kidogokidogo, walipeni hawa wau wajipange upya. Leo hii miezi sita, saba, nane hawajalipwa wamefilisika. Wana lengo zuri na Serikali yao, lakini mnawavunja moyo, hawa watu hawawezi kuendelea hata siku moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili lichukue kwa uzito, hawa watu waweze kupata fedha zao waweze kulipa madeni yao. (Makofi)

Suala lingine ninaomba niwapongeze TRA kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini kuna suala lingine ambalo sasa hivi tunalalamika sana kuhusu ubunifu wa mapato ya kukusanya kodi. Kuna suala la TATO, wanalalamika sana na mimi ninaomba nikufikishie Mheshimiwa Waziri japokuwa liliongelea kwenye Kamati naona hamkuliongelea hapo. Kuna hawa wasafirishaji wa mafuta kutoka nje ya nchi; kwa mfano, watu kutoka Kongo, Zambia, Rwanda na Burundi, wanaagiza mafuta yanapita kwenye Bandari yetu. Sisi Serikali au TRA wanawapa siku thelathini

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ili ule mzigo uwe umetoka nje, matokeo yake wasipomaliza kuusafirisha mzigo ule, ule mzigo unakuwa ni *local*.

Sasa tuna athari mbili; la kwanza hawa wasafirishaji wameshahama wamehamia Beira, wengine wamehamia South Africa na wengine sasa hivi wamehamia Mombasa, sasa tunapoteza mapato makubwa sana. Hawa watu tukiwapa siku sitini wanazoomba hazituathiri chochote, lakini leo hii tunawakatalia wanahama wanamahmia Bandari nyingine tunakosa mapato. Leo hii kusafirisha mafuta hayo kwa siku, magari zaidi ya mia mbili, tutapata kodi kubwa, tutauza mafuta ya kwetu, tutapata *fuel levy*, tutapata *Road Toll*, tutapata kila kitu katika haya magari yakisafirisha mafuta hayo sasa haya mmewakimbiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii *PUMA* wamehamia Beira, wamepewa siku 120, lakini *TATO* wanaomba siku 60 tu, leo hii miezi sita na hamtaki kuwasikiliza! Hebu liangalieni hili, wapeni siku 60 mafuta yawe yamekwisha toka nje. Lingine linatuharibia sisi utaratibu mwingine wa *Bulk Procurement*. Leo hii mafuta yale yakikaa siku 30 mnawalazimisha yawe *local*, msimlazimisha mtu auze mafuta hapa mwache alikonunua ayapeleke yanakotakiwa kwenda.

Wapeni siku 60 wasafirisha mafuta yao; watu watapata ajira, magari yatasafirishwa na madereva watapata kazi na watapata mishahara. Mkiwakatalia, hivi sasa Mombasa wamewapa siku 120, kwa hiyo, mafuta ya Rwanda na Burundi sasa hivi yameanza kupita Mombasa. Mkiwakatalia, hawa wote wanaotoka Kongo, kutoka Zambia, wanaagiza mafuta sasa kupitia Beira; matokeo yake sasa hata hiki chanzo tulichokuwa tunapata kidogo hatuwezi kukipata tena. Kwa hiyo, liangalieni hili na mchukue maamuzi.

Niko hapo hapo kwenye suala la mafuta, yale magari 200 au 300 kwa siku yatanunua mafuta Tanzania. Kwa hiyo, lita elfu mbili, mbili kwenye magari mia mbili ni karibu lita milioni mia nne, mia tano huko, tunakosa kodi kwenye hayo mafuta; matokeo yake magari hayo yatahama tena. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, uliangalie vizuri. (*Makofi*)

Suala lingine nitaongelea kuhusu *TBS*, Mheshimiwa Vincent ameliongelea pale. Kwa mara ya kwanza nimeona kumbe na yeye ana akili kidogo. (*Kicheko*)

Hii *TBS* tunapowapa Mawakala kutoka nje tunapoteza fedha nyingi sana. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba ifike wakati tuajiri vijana wetu waende wakakae huko nje, tuchague nchi mbili au tatu za kuanzia mfano. Tuanzie China, Japan au nchi nyingine. Wakiwatoza kule ushuru wa ukaguzi, zile fedha zitaingia kwetu, kwa hiyo, tuanze na nchi chache ili tuweze kukusanya kodi hizo, kuliko kuwapa Mawakala ndani ya milioni mia nane sisi tunapata milioni ishirini. Tukiajiri wa kwetu wakaenda kule wakawa wanakagua, wakilipisha kule kwenye kompyuta huku kwetu tutaona, ule mzigo umekaguliwa kule, umeingiza kiasi kadhaa na ninyi mtapata mapato, kuliko kuwapa mawakala ambao hujui wametoka wapi, wa nchi gani, wananufaika na nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa suala la *TBS* hebu anzeni na nchi chache. Anzeni kwenye zile nchi ambazo zinaleta mizigo mingi sana kuja Tanzania, tuajiri watu wetu wenyewe, tuweke ofisi zetu kule na akikaguliwa kule huku mnajua mnafunga tu mitambo. Siku hizi kuna kila kitu, akikagua kule ikiingia risiti na huku mmeshaona kuwa mmeingiza kiasi kadhaa. Tunapoteza fedha nyingi sana pasipo sababu yoyote ya msingi. (*Makofi*)

La mwisho ni hii Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa habari tulizonazo ni kwamba, kila mwanafunzi anayemaliza *form six* anatakiwa kulipa shilingi elfu thelathini. Sasa mimi ninaona kama ni wizi tu; kila anayemaliza *form six* ni lazima aende Chuo Kikuu; na je, akifeli ile hela yake inakwenda wapi? Kwa hiyo, huu ni wizi wa waziwazi, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

aliangalie hili. Hii ni dhuluma, huwezi kum-charge mtu amemaliza *form six* alipe elfu thelathini kwenye Bodi ya Mikopo; je asipofaulu? Huo ni wizi mwingine ambao ni wa waziwazi. *(Makofi)*

Lingine, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji, amejitahidi sana katika Jimbo langu la Sumbawanga Mjini kuna Miradi ambayo imekalimika. Ipo Miradi mingine kama miwili hivi, ningepomba sasa ndiyo maana nilikuwa ninasema, hili suala la kuchukua wazabuni kutoka nje au Wakandarasi kutoka nje ya Mikoa ni matatizo makubwa. Watu wanachukua watu wa ajabu wanakuja kule Miradi imesimama moja kwa moja; kwa mfano, Mradi wetu wa Chelenganya, mpaka leo mkandarasi alipofika aliacha mabomba akaondoka. Tuna Mradi wetu mwingine wa Malagano kule, ambao unashusha maji Tamasengo – Pito mpaka leo umesimama. Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kama unasikiliza hili, hawa wakandarasi tulionao uwafukuze uwape wakandarasi wengine. *(Makofi)*

Ninaomba nimshukuru Waziri wa Nishati na Madini, kwa kweli Jimbo langu la Sumbawanga Mjini asilimia kubwa tumepata umeme. La pili, nawashukuru Mawaziri wengine wote kwa kujali Mkoa wangu na Jimbo la Sumbawanga Mjini. Sina kero nyingi sana, nina kero chache hizo ambazo ninaomba zifuatiliwe. Mheshimiwa Magufuli, naomba zile barabara mlizotupa, tunashukuru lakini ziende kwa wakati. Zimesimama muda mrefu, lakini mbaya zaidi wakati zimesimama barabara zile hazichongwi, bora wangukuwa wanapitisha hata greda ziweze hata kupitika. Zimeshakuwa mbovu, zina mashimo makubwa, leo ni mwaka wa tatu. Sasa ifike wakati kama zimesimama, tuwaombe hata wale Wakandarasi waweze kuzisafisha hata kidogo ziweze kupitika kwa urahisi; lakini zimeachwa na hazina bajeti yoyote kwa sababu tulitegemea barabara ya lami itajengwa. Tunaomba hilo kwa sababu ni kero kubwa sana na Wananchi wanalalamika. Kwa kuwa suala zima la barabara limesimama, tuwaombe sehemu ile ambayo barabara imesimama basi waweze kukwangua au kupitisha greda iweze kupitika. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na mapacha wake, hebu iangalie Wizara ya Kilimo, ni Wizara nyeti, ndiyo tunasema Kilimo ni Uti wa Mgongo. Wale wanaolalamika hawana ajira, waje Rukwa, tuna mashamba mengi, tuna ardhi kubwa waje walime tutawapa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi, kwa mchango wako. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Amina Mwidau ndiyo anayefuata na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nami nichukue fursa hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, kwa uwasilishaji wake wa bajeti kwa mara ya kwanza kabisa, kwa umahiri mkubwa na ni mwanamke wa pili katika nchi yetu kuwa Waziri wa Fedha. Vilevile niwapongeze Manaibu wake, ninajua ni Wachumi na watamsaidia, kwa sababu wanashirikiana vizuri, niungane na Mheshimiwa Aeshi katika hili. *(Makofi)*

Ndugu zangu, mzigo mliopewa ni mzito, kwa kweli bajeti hii na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wameeleza kuwa haitekelezeki; ni ukweli kabisa na Mheshimiwa Malima unajua. Kwa sababu ukiangalia bajeti ya mwaka jana (2013/2014) ilikuwa ni tatizo, mwaka huu trilioni kumi na tisa nukta sita; hii bajeti haitekelezeki na ninyi mnajua. Makusanyo ya ndani ni madogo kuliko matumizi ya kawaida, hilo sitaki kulirudia kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wameligusia, lakini ni wazi kuwa, Bajeti ya Maendeleo Serikali haichangii kabisa, tunategemea Wahesani na mikopo kutoka ndani na nje. Hili limetuchezesha kweli kwa bajeti ya mwaka jana,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali kufika Machi hapa ilikuwa hoi, kuanzia Desemba mpaka Machi. Machi na Aprili ndiyo angalau hawa Washirika wa Maendeleo wameweza kuchangia trilioni moja nukta moja tu katika pesa ambayo wameahidi. *(Makofi)*

Hili linaturudisha nyuma, ni funzo kwetu kwa nini hatujifunzi? Kile tunachokusanya kwa nini kilekile ndiyo hatuweki bajeti? Hivi hatuwezi kuchukua mifano kwa wenzetu? Hawa Washirika wa Maendeleo na hiyo mikopo mingine yenye masharti, siyo kwamba hawana pesa, wana pesa lakini wanatupa funzo ili na sisi tuweze kufunga mkanda, tuweze kuwa na bajeti yetu. Kama haitoshi kwa nini hatujifunzi kwa Uganda?

Uganda hii leo wana tatizo kubwa sana, hawa Washirika wa Maendeleo, wamewaletea Muswada ambao ni mgumu. Sasa kama hatukubali kubajeti kile ambacho tunakipata na sisi tutapata masharti hayohayo kama waliyopata wenzetu, kwa sababu Uganda ni jirani zetu. Ukiona mwenzako ananyolewa na wewe tia maji. Utakuja Muswada hapa wa kuoana jinsia moja na nini; tutafanya nini? Itakuwa ni hayo hayo, kwa hiyo na sisi tuchukue mifano ya wenzetu, tukubali kubajeti kile kile ambacho tunakipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la nidhamu katika bajeti. Hakuna nidhamu kabisa, nidhamu ni zero, kile ambacho tunakibajeti siyo tunachotumia. Mfano mdogo, tumeona juzi hapa yamezuka Maadhimisho ya Muungano, fedha zilizotumika hazikuwepo kwenye bajeti. Mwaka jana tulipokuwa tukifanya bajeti hamkujua? Hilo kwa sababu lilikuwa suala kubwa sana ndiyo maana limejulikana, kuna mengi ambayo yanazuka ndani ya bajeti. Kwa hiyo, hakuna nidhamu katika matumizi ya bajeti kabisa.

Ndugu zangu hapo mbele, kutokana na umahiri wenu, bado watu wana imani na ninyi, ninategemea haya mtayafanyia kazi, mtapambana, mtafunga mkanda wa chuma ili muweze kupambana na haya.

Niongelee kodi; jamani tunapiga kelele Watanzania hawana utamaduni wa kulipa kodi ni kweli kabisa, lakini tujulize je, Viongozi wanalipa kodi? Kama tunawalalamikia Watanzania hawalipi kodi; Viongozi wanalipa kodi? Tunatakiwa sisi kama Viongozi tuoneshe mfano, kuongoza ni kuonesha mfano. Tunaomba ili Wananchi wawe Wazalendo, waweze kulipa kodi kwa haki kabisa, sisi Viongozi wote wa Serikali kuanzia Wabunge, Mawaziri, mpaka Rais, ile misamaha ya kodi iondolewe, tuoneshe mfano sisi kwanza na Wananchi nao watalipa kodi. *(Makofi)*

Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Waziri, kwa kuchukua hatua kadhaa za kuboresha usimamizi wa fedha za umma na hasa matamko aliyoyatangaza haya ya kupambana na misamaha ya kodi. Japokuwa utapata pingamizi kubwa sana katika hilo, kwa sababu kuna manyangumi katika kodi, lakini kwa kule kutangaza tu basi umechukua hatua. Vilevile ukiangalia misamaha ya kodi, sasa hivi imefikia 3.5% ya Pato la Taifa na ni 10% ya Bajeti ya Serikali, ni kubwa sana. Inabidi Mheshimiwa Waziri kama ulivyoahidi hapa, kwa kweli hili ulifanyie kazi.

Ahadi hizi zilikuwepo hapo nyuma lakini sasa hivi mnachotakiwa ninyi kama timu, mfanye utekelezaji sasa; kwa sababu haya tumeyasikia miaka mingine iliyopita. Vilevile niungane na Serikali kusema kuwa, itatangaza yale majina ambayo yananufaika na misamaha ya kodi. Kutangaza huko kutasaidia kuleta hamasa kwa Wananchi kuweza kushinikiza ili ile misamaha ya kodi iweze kufutwa. Hiyo ni hatua nzuri kwa kuanzia.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), tulitoa agizo kama Kamati kwenye Taarifa yetu kuwa, hii misamaha ikaguliwe na CAG, kwa sababu hizi ni pesa za Serikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tungeweza kukusanya basi ingekuwa ni pesa kamili ya Serikali, kwa hiyo, zikaguliwe kama ambavyo zinakaguliwa fedha za Serikali na vilevile taarifa yake itolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie katika ukuaji wa uchumi. Wabunge wengi wamegusia suala hili. Ukuaji wa Pato la Taifa. Kwa kweli tunawachanganya Wananchi, kwa sababu ni takwimu tu ambazo ndiyo zinzkua, ukienda kwenye uhalisia huko vijijini, hali ni ya hatari. Kama ndugu zangu wa Pangani kwa kweli ukiwaambia ukuaji wa uchumi ni kama unawaonea; kule hakuna maji safi na salama, hali yao ya uchumi ni mbaya, ukiwaelezea kuwa uchumi unakuwa kwao ni kama vile unawaonea. Hakuna uhalisia kabisa na watu wetu wa chini na hili Wabunge wengi sana wamesisitiza.

Suala hili likisemwa, wenzentu upande wa pili mnapiga makofi! Jamani ni kama vile Serikali inawadhikiki Wananchi. Mheshimiwa Waziri ameelezea hapa kuwa, bajeti hii imelenga kupunguza gharama za maisha ya Wananchi, kwa kuendelea na jitihada za kudhibiti na kupunguza mfumko wa bei, kitu ambacho kinaendelea, ni kweli hatukataia kwa hilo.

Wananchi wengi wanaona, gharama za maisha zinapanda siku hadi siku. Ukiangalia kwenye *Household Budget Survey* ya Mwaka 2012, ukilinganisha na Mwaka 2007, kwa kweli bei za vitu zimepanda zaidi ya mara mbili. Kwa hiyo, hii ni hatari. Kwa mtu wa chini yeye anaangalia ule uhalisia wake, ni kitu ambacho siku hadi siku anaki- *apply*. Kwa hiyo, anajua kuwa hii siyo kweli, Serikali inatudhikiki kwa kusema inadhikiki.

Twende na uhalisia, hali halisi za Wananchi wetu. Mwananchi wa kawaida kule anakula mlo mmoja kwa siku, tena mlo wenyewe siyo lishe bora, anakula tu ili kujaza tumbo. Unapomwambia kuwa uchumi unakua, hakuelewi hata kidogo. Kwa hiyo, pia tupunguze kupiga makofi. Tunapigia makofi vitu ambavyo havina uhalisia, tunawatia chuki Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee *Bulk Procurement*, ambayo Mheshimiwa Aeshi ninaona kama aliigusia kidogo. Mheshimiwa Waziri kaeleza kuwa, Serikali imeamua kuzingatia ununuzi wa pamoja kutoka kwa wazalishaji moja kwa moja, anaondoa Mawakala. Hiki ni kitu kizuri na ninakiunga mkono kwa upande mmoja. Tukumbuke siku za nyuma Serikali iliamua kununua mafuta ya petroli na diseli kwa kutumia *Bulk Procurement*. Naomba Mheshimiwa Waziri, atuelezee utaratibu huu umefikia wapi na tumejifunza nini?

Akiweza kutuelezea hilo, basi angalau tutaweza kupata moyo kuwa hili lingine linalotaka kufanyika, japokuwa ni zuri kabisa la kuondosha wale Mawakala kwa sababu angalau bei zitakuwa zimeshuka, tutakuwa tumejifunza kutoka upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye MKUKUTA. ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mwidau, tunakushukuru sana, muda ahuko upande wetu. Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya. atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu. Kabla sijaanza kuchangia, ningependa niseme neno moja; kuna msemu unaoesema kwamba, Viongozi ni kioo cha Taifa au jamii, hivyo basi, ningependa tukumbushane sisi wote ambao tuko humu ndani tuliochaguliwa na wa Wananchi kwamba, tunatakiwa kuwa mfano wa kuigwa na jamii ambayo imetuleta hapa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jamii haijatuleta hapa tuje tulaumiane tu na kutupiana maneno, tuanze kumkashifu hata Kiongozi Mkuu wa Nchi na tuache kutambua hata zile nguvu za Wananchi wanazochangia kuleta maendeleo, tuanze kusema hakuna maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwatendei haki Wananchi. Kwa hiyo, naomba kila mmoja wetu, ana masikio ya kusikia, inapotangazwa Miradi ambayo imefanyika, ana macho ya kuona. Wenzetu wamesafiri kutoka Kilimanjaro wanapita barabara nzuri. Wamesafiri kutoka Rukwa, Mbeya wapi, wamepita kwenye barabara nzuri. Angalau basi hiyo miundombinu ambayo inarahisisha safari zenu hamjaiona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uratibu na Mahusiano), kwa Taarifa yake ya Hali ya Uchumi pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015. Amewasilisha vizuri na mimi naamini kwamba, kila mmoja wetu akitekeleza wajibu wake tutafanikiwa.

Napenda nichukue fursa hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake na Watendaji wake, kwa Bajeti nzuri ambayo wameitengeneza mwaka huu wa 2014. Ninawatakiwa utekelezaji wenye mafanikio na baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, ninaomba nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa utendaji wake mahiri ambao umepelekea Taifa hili kuweza kupata mafanikio katika maendeleo ambayo yanaonekana wazi na kila mtu. Ndiyo sababu tunatambulika kwamba, tumejitahidi sana ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika ya Mashariki. Ukiona vinaelea ujue vimeundwa. Kwa hiyo, vimeundwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete; tutambue hilo. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Wananchi wangu, napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais, alipopita kwenye kampeni za mwaka 2005, aliahidi kwamba, tungepata umeme wa MCC. Halmashauri ya Morogoro ilikuwa haina umeme kwenye maeneo makubwa hasa sehemu za milimani. Hivi sasa tumepata umeme. Wananchi wale wanaomba Vijiji ambavyo bado havijapata umeme, Serikali iendelee na juhudi zake ambazo zimeanza kwa spidi kubwa kupelekea Wananchi umeme kwenye vijiji vya milimani. Wasisahau kwamba, tunaomba umeme ufike kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ambayo yapo Mvaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais, aliahidi kwamba tungepata maji safi. Tumeanza kupata maji kutoka kwenye Mradi wa Chalinze, tunauita *Chalinze II* na wanaita maji ya JK; tunashukuru. Zipo Kata nyingine ambazo bado hazijafikiwa na maji haya, ambazo zimewekwa kwenye Mpango wa *Chalinze III*, lakini bado hatujaona juhudi za kuleta maji. Kwa hiyo, tunaomba wahusika watekeleze hii ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali sana kwa kuona umuhimu wa kutupa daraja katika Mto Mbezi, ambako Wananchi wengi walikuwa wanapoteza maisha katika Tarafa ya Mkuyuni. Daraja limeanza kujengwa, wametupa milioni 550, Wananchi wanasema ahsanteni. Kuna daraja lingine ambalo Mheshimiwa Rais aliahidi katika Kata ya Tununguo kwenye Mto Ruvu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wanakufa pale wengi sana kwa kujeruhiwa na kuliwa na mamba. Kwa hiyo, kwa sababu ni ahadi ya Rais na muda wa kukaa madarakani kwa kipindi hiki unaelekea ukingoni, ninaomba Wizara ya Ujenzi ambayo ilikabidhiwa jukumu hili, iangalie namna ambavyo hii ahadi ambayo kila mtu kwenye lile eneo anasubiri, basi waitekeleze kwa sababu wamesema hawataki kitu kingine wanaomba hilo daraja.

Baada ya kusema hayo sasa, ninaomba nizungumzie mambo mawili, matatu. Naomba Wananchi wa Tanzania tuwakumbushe kwamba, hata Misahafu Mitukufu inazungumzia wajibu wa kulipa kodi. Biblia Takatifu inasema hivi, Bwana Yesu alisema, mpeni Kaizari yaliyo yake ya Kaizari na Mungu yaliyokuwa yake Mungu. Kwa hiyo, basi anayekwepa kulipa kodi anatenda dhambi. Sasa mimi naomba sisi kama Wawakilishi wa Wananchi, tuna wajibu wa kuwahamasisha Wananchi walipe kodi; kwa sababu bila ya kulipa kodi hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nitoe ushauri mmoja kwamba, kulipa kodi ni utamaduni na lazima utamaduni huo ujengeke. Tuanze kuwajengea watoto wetu utamaduni wa kujua kwamba, ulipaji wa kodi unakwenda sambamba na maendeleo. Kwa hiyo, basi naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iangalie namna ambavyo wataingiza kwenye Mtaala wao, kwenye somo la Uraia kwamba, iwe ni *compulsory* watoto wafundishwe umuhimu wa kulipa kodi; na ni kodi gani ambazo Wananchi wanatakiwa kulipa, kusudi watakapotoka kuja kwenye shughuli zao za kawaida wajue wanalazimika kulipa kodi kama ilivyo kwenye nchi nyingine. Mwananchi anaona asipolipa kodi na kujaza fomu yake ya kodi anaogopa.

Sasa sisi tuliweke hilo kwenye mifumo yetu ya malezi ndani ya jamii yetu hususan watoto. Wahenga walisema kwamba samaki mkunje angali mbichi. Sasa hivi hawa ambao wamebobeza katika kukwepa kodi hata tukiwafanyaje hatutaweza kuwabadilisha, lakini tuendeleo kuwapigia kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itambue mchango wa Wananchi katika ujenzi wa miundombinu ya maendeleo katika nchi hii. Katika Bajeti kama hii, tunapozungumza kwamba Serikali imetumia shilingi fulani kwenye maendeleo, sasa jamani kwenye hiyo miradi ya ujenzi wa shule, zahanati na sisi wengine tunaishi milimani wamechangia katika kulima barabara vijijini na kwenye vitongoji. *Je, can't we prize? Hatuwezi tukaweka a prize tag* kwamba, Wananchi wa Tanzania kwenye Mwaka wa Fedha uliopita walichangia kiasi hiki kuisaidia Serikali yao katika kuendeleza Miradi ya Maendeleo?

Kwa namna hii tunawafia moyo kwamba, tunawatambua kama Serikali. Mimi naomba Bajeti inayokuja, Halmashauri zitoe taarifa TAMISEMI kwamba, Wananchi wamejenga Miradi ipi, wamechangia Miradi ipi, nguvu na fedha, yote iletwe tuone kwa pamoja Wananchi wameshirikiana na Serikali yao katika kujiletea maendeleo.

Lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu unafuu wa kodi. Naishukuru Serikali imeona hawa Wananchi wanaofanya kazi wanalipa kodi kubwa, wakaondoa asilimia moja tu. Ukiangalia unaona *impact* yake siyo kubwa sana, kama tumeamua sasa tunakula nguruwe, basi tumle aliyenona. Tuwasaidie hawa Wananchi kwa kupunguza asilimia kubwa kidogo ili ifike angalau asilimia tisa, yule Mwananchi ataona kweli Serikali imemjali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, maisha ni magumu. Mwalimu anaishi kijijini, hawezi kuanzisha hata mradi wowote ule wa kumwezesha kuongeza kipato chake. Kwa hiyo, tukiwapunguza kodi, watafanya kazi yao vizuri, rushwa katika kuandikisha watoto shule haitakuwepo na tutapunguza rushwa katika utoaji wa huduma za afya kule vijijini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, muda siyo huo, kengele ya kwanza.

NAIBU SPIKA: Ya pili Mheshimiwa.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, lakini tuisahau kuvifungua viwanda vya majembe vifunguliwe majembe yapunguziwe ushuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya. Sasa ni Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu.

MHE. CHRISTINA M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa muda huu ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nakubaliana na msemaji aliyepita kwa usemi kwamba, ukiona vyaelea basi vimeundwa. Usemi huu ni wa kweli, nami nawaambia Watanzania kwamba, ukiona Watanzania wanaelea kwenye dimbwi la umaskini, basi dimbwi hili limeundwa na Serikali ya CCM ndiyo imeleta dimbwi hili la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari za kukua kwa uchumi kwa asilimia saba nimeanza kuzisikia tangu nimekuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu na sasa hivi ni mwaka wa nne, uchumi unakua kwa takribani asilimia sita kwenda saba. Wabunge siku zote wamehoji mbona uchumi huu hauonekani ukikua kwa Wananchi?

Watendaji wa Serikali, ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri pale, ni wajanja, wana akili na wanalijua jibu hili. Jibu hili limeendelea kutolewa tangu mimi nimekuwa Mbunge hapa kwamba, uchumi unakua lakini mnajua uchumi huu ni uchumi jumla. Sasa mimi nakuuliza hivi ni Watanzania wangapi wanaelewa habari ya uchumi jumla? Mtanzania wa Kijijini kule kwangu Mahambe nani anajua habari ya uchumi wa jumla?

Jibu lingine la msingi walilonalo watakuueleza kwamba, unajua uchumi hauonekani kuimarisha maisha ya Watanzania, kupunguza umaskini, kwa sababu sekta zinazokua ni zile ambazo hazigusi maisha ya Wananchi. Sasa mimi nawauliza; leo siwaulizi kwa nini asilimia saba ya kukua kwa uchumi hazijaleta nafuu ya maisha; mimi nawauliza kwamba ni kwa nini sekta ambazo hazileti nafuu ya maisha hizo ambazo mnasema zinakua; mawasiliano, ujenzi; kwa nini hamjazifanyia kazi sekta mbazo zinagusa maisha ya Watanzania.

Kwa hiyo, hatutaki jibu kwamba uchumi huu umekua kutokana na sekta ambazo haziwagusi Wananchi ndiyo maana Wananchi wanaendelea kuwa maskini. Nawauliza ni kwa nini hampeleki uchumi kwenye sekta zinazowagusa Wananchi ili Wananchi nao waimbe wimbo wa uchumi unakua?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua ni tatizo la Mipango isiyotekelezeka. Nchi hii ni wazuri kwenye kupanga. Tumewahi kuwa na Mipango mingi; Nguvu Kazi, Siasa ni Kilimo, Mkukuta, Kilimo Kwanza na Matokeo Makubwa Sasa. Mipango ni mingi lakini upi uliowahi kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulizinduliwa tena na Mheshimiwa Rais kwa mbwembwe na sifa na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mliusifia! Leo tunaingia Mwaka wa nne wa utekelezaji wa miaka mitano, haujawahi kutekelezwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mpango ule kwa asilimia mia moja hata kwa mwaka mmoja! Mwaka kesho mtawaambia nini Watanzania? (Makofi)

Leo hii Waheshimiwa Wabunge wa CCM wanaona aibu kuutamka Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mwaka jana baada ya kuona Mpango wa Miaka Mitano hautamkiki tena, mkaleta Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Matokeo Makubwa Sasa, mkatoa asilimia 55 tu ya fedha kwenye Miradi ya Maendeleo iliyopo kwenye hiyo *Big Results Now*. Sasa mnaanza kuionea aibu *Big Results Now* kuitamka, sijui mnabuni kaulimbiu ipi tunaisubiria maana ninyi ni wabunifu na nchi inaendeshwa kwa kaulimbiu! (Makofi)

Vyanzo vya Mapato, Mheshimiwa Waziri wangu Saada, mimi naamini wanawake tunaweza. Umenivunja nguvu ulipokuja na hotuba yako isiyo na vyanzo vya mapato ambavyo Wabunge wote kwa umoja wetu tumekuwa tukivillia siku zote. Mheshimiwa Saada, umekuja na Bajeti ambayo toka siku ya kwanza wewe mwenyewe una uhakika na Naibu Mawaziri wako kwamba, Bajeti yako haitatekelezeka *from day one*. (Makofi)

Mwaka jana tulikuwa na Bajeti ya trilioni 18.2. Unajua mwenyewe kwamba, makusanyo yalifikia asilimia 70 kama mnavyosema mpaka Aprili. Kodi, maduhuli, yalikusanywa kwa asilimia 65, mikopo nayo ilikuja kwa asilimia 55 ya maendeleo. Sasa Mheshimiwa Waziri, ukijua kwamba Bajeti ya trilioni 18.2 haikutetelezeka; unawezaje kuwaambia Watanzania kwamba mwaka huu utakusanya trilioni 19.8?

Dada yangu, ningefikiri kwa sababu wewe ni mwanamke utakuwa na bahati mbaya zaidi, kwa sababu mwisho wa siku utakuja kuambiwa aah, hiyo Bajeti ya Mwanamke mlijua ataweza nini? Mimi nilifikiri utaleta Bajeti halisi inayotekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawadanganya Wananchi, kwa kuwapa matumaini ambayo wakati huo huo tuna uhakika kwamba, hayataetelezeka. Vyanzo ni vile vile kama tulivyoambiwa bia, soda, maji, juisi na sigara. Tunaambiwa sababu ya kuongeza ushuru kwenye bidhaa ya sigara ni kwa sababu eti ya kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Afya kwamba matumizi ya tumbaku si sahihi. Tunajua kwamba, viwanda vya sigara ndiko ambako Serikali inategemea kwa asilimia kubwa kupata kodi yake. Ikiwa sababu ya kuongeza tozo kwenye sigara ni eti kuwalinda Watanzania kutokana na matumizi haramu ya tumbaku; mbona hatujaona mkakati wa kupunguza kilimo cha tumbaku?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo tunajidanganya. Kodi ya tumbaku tunaitamani, huku ndiyo maana tunaongeza kodi. Kama ni afya hilo hatulitamki sana, kwa sababu suala lingekuwa ni afya tungesema kule Tabora acheni kulima tumbaku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mimi nataka niulize, hivi kodi kwenye vinywaji baridi kama soda, juisi na maji madhumuni ya ushuru huu ni nini? Mimi ninajua kwamba, ushuru wa bidhaa huwa unatolewa kama bidhaa hiyo inakusudiwa kupunguzwa matumizi yake, ili walaji wa bidhaa hiyo wasiathirike. Sasa mimi nataka niulize Serikali; je, malengo ya kutoza vinywaji baridi ni kuwazuia Watanzania wasitumie vinywaji hivyo?

Mimi najua maji na juisi vinahitajika. Ninajua pia kwamba, vinywaji vya baridi ndiyo vinatumiwa na Wananchi wa kipato cha chini. Kwa hiyo, niulize Serikali kwamba bidhaa hizi wenyewe sasa wanaziweka kwenye fungu lipi la anasa au matumizi ya lazima?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Vilevile kuongeza ushuru kwenye bidhaa ya bia tumechoka! Hivi Watendaji wetu wamekuwa wachovu kufikiria vyanzo vingine vya mapato ni lazima iwe bia? Viwanda vya Bia sasa hivi wanashindwa kuzalisha kwa kiwango kile kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hata ukienda kwenye sherehe ya harusi, watu wengi wanakunywa maji, wanywaji wa bia siyo wengi kama ilivyokuwa. Sasa unapofikiria utaongeza hela za kodi kwenye bia, wenzio uzalishaji unashuka na sasa ajira na *effect* zingine zitaendelea kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee matumizi ya Serikali. Yameendelea kuwa mabovu na mimi nitoe mfano wa kwanza; safari za Viongozi. Tumeambiwa tumsifu Kiongozi wetu wa Taifa na mimi wala sina tatizo na hilo, lakini matumizi ya safari za Viongozi Wakuu; mwaka jana fungu la safari la Viongozi Wakuu lilikuwa bilioni 15, mwaka huu imeongezeka kutoka bilioni 15 kwenda bilioni 50. Hili ni ongezeko la asilimia 300 na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilidhani Serikali inasikiliza kwamba, watabana matumizi. Sasa badala ya kufikiria kuhoji hivi Kiongozi wetu anaenda hizo safari nyingi zenye gharama kubwa kufanya nini na zina tija gani? Watu wamekuwa *busy* kujitahidi kuongeza fedha ili Wananchi wachangie hizo safari ambazo hatujui tija zake? Sisi tumeelezwa kwamba, Mawaziri nchi hii, Maraisi waliwahi kuwepo na hakuna Rais aliyetumia fedha nyingi kama wakati huu. Kwa hiyo, kama mko wakweli Waheshimiwa Wabunge wa CCM, naomba mlitazame fungu hili, kwa mwaka mmoja zaidi ya asilimia mia tatu zinaongezeka kwa ajili ya Viongozi Wakuu wa Serikali na msafara wa watu usio na idadi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. CHRISTINA M. LISSU: Muda umeisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina, muda umeisha. Nakushukuru sana. Ukishangaa ya Tundu utastaajabu ya Christina. Nilikuona Mheshimiwa Engineer Stella!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa heshima tu niliona pengine mzungumzaji amalize nisifanye *interruption*, lakini nilikuwa natamani kumpa taarifa kwamba, kimsingi, amesema Mpango wa Maendeleo haujafanya chochote. Nikasema kwamba, kwa kweli ni kwa sababu mara nyingi anapewa lifti na Mheshimiwa Ndesamburo kwenye helikopta, kwa hiyo, hawezi kuona vizuri kinachoendelea. *(Kicheko)*

Kuna mambo mengi sana ambayo yamefanyika na mimi binafsi, mfano tu ningependa angalau aanzie hata kutoka hapa Dodoma mpaka Iringa, afike Tunduma, aende mpaka Sumbawanga, aone tofauti kubwa iliyofanyika ndani ya muda wa miaka hii miwili. Hiyo ni sehemu fupi tu, hapo sijamtajia Ruvuma, toka Songea mpaka Mbinga, mpaka Namtumbo na maeneo mengine, ukiacha maji na umeme.

Naomba achukue hiyo taarifa yangu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina kwa dakika moja unaipokea hiyo taarifa?

MHE. CHRISTINA M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, namsikitikia sana Mheshimiwa Manyanya, kwanza, anaitwa Engineer, sasa akafanye mahesabu mwenyewe aniambie kwa miaka mitano ya Mpango wa Maendeleo ni mwaka upi ambao Mpango huo umetekelezwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa asilimia mia moja kama ambavyo Bunge lilipitisha. Aseme; yeye ni msomi, anajua hesabu vizuri kuliko mimi, afanye mahesabu aniambie.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu. Tumalizie kwa kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Jafo, Mbunge wa Kisarawe, ambao ni Bwana Khalfan Siko, Katibu wa Mbunge; usimame, karibu sana.

Ndugu Ibrahim Tuli, Katibu wa Chama cha Walemavu katika Wilaya ya Kisarawe; karibu sana kaka yetu Tuli.

Ndugu Moshi Mohamed, Afisa Miradi wa *JAFO Foundation*; karibu sana.

Wapo pia Wataalamu wa Vyombo vya Usafiri ambao ni watatu; Bwana Abdallah Madeng'a, Bwana Ali Kigongo na Bwana Ali Mkomwa; karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa mjadala wa leo, tutaendelea na mjadala huu kesho. Kwa hiyo, kwa kuwa tumekamilisha kazi zote hapa Mezani zilizopangwa siku ya leo, naomba sasa niwahakikishie wale ambao walitegemea watachangia watachangia kesho.

Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.41 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 18 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*